# ILANI YA UCHAGUZI YA CCM YA MWAKA 2010 – 2015

## UTANGULIZI

1. Katika Uchaguzi wa kushindanisha vyama vingi vya siasa ili kutwaa Dola na kuunda Serikali kila Chama hutarajiwa kuandaa Ilani ya Uchaguzi. Ilani hutafsiri na huelezea Sera za Chama kuhusu maeneo muhimu ya siasa, uchumi na jamii na hutoa maelezo fasaha kuhusu mikakati ya utekelezaji wa sera zinazonadiwa pindi wagombea wake wakifanikiwa kushinda. Aidha hutoa ahadi kwa Wananchi kuhusu mambo ambayo Chama kitaelekeza na kusimamia Serikali kutekeleza. Kwa hiyo Ilani ya Uchaguzi ni Maelezo ya Sera katika kipindi husika, na inalenga kuwaeleza Wananchi ni mambo gani Chama kitafanya iwapo kitashinda Uchaguzi na kuunda Serikali. Ilani hii ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2010 hadi 2015 inalengo hilo hilo.

2. Ilani hii ya CCM imejengeka katika kukiri kwamba changamoto kwa Serikali katika kipindi hiki ni ya Kujenga Uchumi wa Kisasa na Taifa Linalojitegemea. Vile vile CCM inatambua kuwa modenaizesheni ya uchumi na Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ndiyo mikakati sahihi ya kujenga uchumi wa kisasa. Aidha mafanikio ya azma hii unategemea kutambua hali na mazingira ya kisiasa, kiuchumi na kijamii ya karne ya ishirini ya dunia na ya nchi.

## HALI YA DUNIA, MAJUKUMU YALIYOMBELE YETU NA MIKAKATI YA MAENDELEO KWA TANZANIA

### Dunia Ilivyo sasa

3. Dunia ya leo imegawanyika katika nchi za kaskazini na nchi za kusini. Nchi zote za dunia kwa ujumla wake zimeathirika na mtikisiko wa fedha na uchumi. Athari za mtikisiko huo zinaonekana kutofautiana kutoka nchi moja kwenda nchi nyingine. Aidha nchi za Kaskazini zilizoendelea zimeathirika zaidi kuliko nchi za Kusini. Hata hivyo, athari ndogo kwa Nchi ya Kusini huongeza tatizo la Umaskini na changamoto ya ujenzi wa uchumi.

4. Ilani hii ya CCM inatolewa katika mazingira ya hayo. Nchi yetu ni nchi miongoni mwa nchi za Kusini na kwa hiyo mtikisiko mdogo umetuongezea makali ya tatizo letu la msingi la uchumi ulio nyuma.

5. Aidha tatizo la nchi yetu ni la uchumi ulio nyuma na tegemezi. Jitihada zinapaswa kuchukuliwa ili kuondokana na hali hiyo. Katika mazingira ya dunia ya sasa ya kiuchumi na kisiasa, bila kufanya hivyo uchumi wa soko wa dunia, utandawazi na nguvu za kiuchumi za nchi za kaskazini utaendelea kuididimiza nchi yetu katika lindi la umasikini, uchumi duni na tegemezi.

6. Katika kutimiza azma ya kujinasua kutoka mazingira hayo na kuelekeza nchi katika Kujenga Uchumi wa Kisasa na Taifa Linalojitegemea, Ilani hii inajikita katika kuendeleza mchakato wa utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 (SMT), 2020 (SMZ).

**Hali ya Nchi yetu**

7. Pamoja na mafanikio mengi tuliyopata na changamoto zilizojitokeza, tuna fursa kubwa ya kuendelea kujenga uchumi wa kisasa ili kumudu ushindani katika mazingira ya utandawazi na kuongeza tija kwa kasi zaidi. Nchi yetu inatambua kuwa changamoto kubwa inayotukabili ni suala la Mapinduzi ya kilimo, ufugaji, uvuvi na viwanda.

   Tukiyamudu Mapinduzi hayo, uchumi utakuwa wa kisasa unaoweza kuzalisha ziada kubwa ya mali na kutoa huduma za kijamii zilizo bora zaidi kwa manufaa ya wananchi wote. Matokeo yake ni kwamba kila mwaka nchi itazalisha chakula cha kutosha na kuuza nje ziada ili kupata fedha za kigeni.

8. Chama kupitia Dira 2025 (SMT) na 2020 (SMZ), Mwelekeo wa Sera wa Miaka ya Tisini na Mwelekeo wa Sera za CCM Katika Miaka ya 2000 hadi 2010 kimeelekeza suluhisho la kuondokana na hali ya uchumi wetu kuwa nyuma na tegemezi ni kufanya modenaizesheni ya uchumi. Mchakato wa modenaizesheni ya uchumi na kuitoa nchi yenye uchumi tegemezi kuelekea uchumi wa kisasa unahitaji kuzingatia vipaumbele vya msingi vifuatavyo:

   (a) Kutilia mkazo katika matumizi ya maarifa ya kisasa (sayansi na teknolojia).

   (b) Kuandaa raslimali watu katika maarifa na mwelekeo.

(c) Kufanya mapinduzi ya kilimo, ufugaji na uvuvi.

(d) Kufanya mapinduzi ya viwanda ambavyo ndivyo kiongozi wa uchumi wa kisasa.

(e) Mapinduzi katika nishati na miundombinu ya kisasa.

Lengo la msingi katika kukabiliana na vipaumbele hivi ni kuchochea uwezo wa kuongeza uzalishaji, jambo ambalo litawezekana kutokana na kuongezeka kwa ufanisi na tija na ziada kubwa katika uchumi.

**Majukumu ya Msingi**

9. Hatua za msingi kuanzisha mchakato wa Kujenga Uchumi wa Kisasa zilishaanza. Kinachohitajika kwa sasa ni kuongeza kasi, utashi na dhamira ya ujenzi wa uchumi wa kisasai na kwa muda mfupi uliopangwa katika Dira za Maendeleo 2025 na 2020. Chama cha Mapinduzi kinaweka bayana kuwa Ilani ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2010 itajikita katika kuendeleza jitihada na kuanzisha hatua ya mwanzo na ya msingi ya mapinduzi kuelekea modenaizesheni ya uchumi na ujenzi wa uchumi wa kisasa wa Taifa linalojitegemea. Katika kipindi cha Ilani hii 2010-2015 mchakato wa kujenga uchumi wa kisasa utekelezwa katika maeneo yafuatayo:-

(a) Kuimarisha na kuboresha elimu.

(b) Kuandaa raslimali watu katika maarifa na mwelekeo.

(c) Kufanya mapinduzi ya kilimo, ufugaji na uvuvi.

(d) Kufanya mapinduzi ya viwanda.

(e) Kuinua matumizi ya maarifa, yaani sayansi na teknolojia katika uchumi wa nchi.

(f) Upatikanaji wa nishati yenye uhakika na nishati mbadala.

(g) Ujenzi wa miundombinu ya kisasa.

10. Kwa kutekeleza haya, Chama cha Mapinduzi kitakuwa kimeandaa mazingira ya kuondoa unyonge na shida zinazowasibu wananchi wake zinazotokana na umaskini na uchumi ulioduni. Aidha Ilani hii itakuwa kielelezo cha dhamira ya Serikali ya Awamu ya Nne ya kuhakikisha kuwa inaitoa Tanzania kutoka uchumi ulio nyuma na tegemezi na kupambana na umaskini kwa hamasa, dhamira na kasi kubwa.

## SURA YA KWANZA

## MAFANIKIO YA KIUCHUMI NA KIJAMII MIAKA 5 YA SERIKALI YA AWAMU YA NNE

11. Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005-2010, ililenga katika kutekeleza kipindi cha pili na cha mwisho cha Mwelekeo wa Sera za CCM katika miaka ya 2000-2010, na kutekelezwa katika kipindi cha kwanza cha Serikali ya Awamu ya

Nne ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya uongozi wa Rais Jakaya Mrisho Kikwete.

12. Katika kipindi hiki Serikali ilitekeleza kwa mafanikio makubwa Mwelekeo wa Sera za CCM katika miaka ya 2000-2010 na Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya mwaka 2005-2010 kwa kuzingatia Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 na Malengo ya Milenia. Aidha, kutokana na mafanikio hayo Serikali imeweza kuendeleza na kuimarisha huduma za kiuchumi, kijamii na kisiasa.

**Mafanikio ya Kiuchumi**:

13. Katika kipindi hiki Serikali imeweza kutekeleza mipango yake kwa ufanisi mkubwa na kuleta mafanikio ya kiuchumi yafuatayo:-

(a) Ukuaji wa uchumi ulifikia wastani wa asilimia 6.7 mwaka 2010 ukilinganishwa na wastani wa 4.5 mwaka 2005.

(b) Mapato ya ndani ya Serikali yaliongezeka kutoka wastani wa Shilingi Bilioni 177 kwa mwezi mwaka 2005 hadi kufikia wastani wa Shilingi bilioni 390 sawa na ongezeko la zaidi ya mara mbili kwa mwezi mwaka 2010.

(c) Mfumko wa bei ulibaki katika tarakimu moja tangu mwaka 2000 hadi 2007 isipokuwa mwaka 2008 ambapo ulifikia kiwango cha 10.3 kutokana na mtikisiko wa uchumi duniani.

(d) Bajeti ya Sekta ya Kilimo imeongezeka kutoka asilimia 4.5 mwaka 2005 hadi asilimia 7.9 mwaka 2010. Kutokana na umuhimu unaoongezeka wa kilimo cha umwagiliaji nchini kama hatua ya uhakika ya kupambana na njaa, Serikali imechukua hatua za kuimarisha mkakati wa umwagiliaji na miundombinu yake, kwa kuendeleza hekta 289,245 za kilimo na kuweka miundombinu ya umwagiliaji. Hatua hii imeongeza ufanisi wa matumizi ya maji kwa umwagiliaji kutoka asilimia 12 iliyokuwepo kabla na kufikia asilimia 30. Aidha, ufanisi huo umeongeza mavuno ya zao la mpunga kutoka wastani wa tani 1.8 kwa hekta na kufikia tani 5 kwa hekta.

(e) Ukuaji wa Sekta ya Viwanda umeongezeka kutoka asilimia 8.4 mwaka 2005 hadi asilimia 9.9 mwaka 2008.

(f) Sekta ya Madini imekuwa na kuleta mafanikio yafuatayo:-

(i) Kukamilika kwa Sera ya Madini ya mwaka 2009.

(ii) Kuanzishwa kwa Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania.

(iii) Kukamilisha ramani tatu za **kijiolojia** zinazoonyesha uwepo wa madini Tanga, Nachigwea na Liganga.

(iv) Kutengwa kwa maeneo ya wachimbaji wadogo katika maeneo ya Kilindi, Winzo, Mvomelo, Melela, Rwamagaza, Nyarugusu, Maganzo na Mererani. Maeneo hayo yana jumla ya kilometa za mraba 5,876.5.

(v) Mchango wa Sekta ya Madini kwenye pato la Taifa umeongezeka kutoka asilimia 2.4 mwaka 2005 hadi asilimia 2.6 mwaka 2008.

(vi) Mapato ya Serikali kutokana na uchimbaji mkubwa yameongezeka kutoka Sh. 457.4 bilioni mwaka 2005 hadi Sh. 840.0 bilioni mwaka 2008.

(vii) Thamani ya madini yanayouzwa nje imeongezeka kutoka dola za Marekani 727.45 milioni mwaka 2005 hadi dola 1,075.9 milioni mwaka 2008.

(vii) Ajira katika uchimbaji mkubwa imeongezeka kutoka wafanyakazi 7,000 mpaka 13,000.

**Mafanikio katika Sekta ya Miundombinu**

14. Kipindi cha miaka kumi iliyopita cha 2000 – 2010 kimeshuhudia kuwepo kwa ujenzi mkubwa wa miundombinu ya barabara, viwanja vya ndege na madaraja nchini. Miradi yote ya ujenzi ambayo haikukamilishwa kati ya 2000 – 2005 imekamilishwa kati ya 2005 – 2010 na kuanzishwa ujenzi wa miradi mipya. Kitakwimu, ujenzi wa miradi 15 kwa kiwango cha lami yenye jumla ya urefu wa Km. 1,398.6 imekamilishwa katika kipindi cha 2005 - 2010. Aidha, ujenzi ambao unaendelea ni wa miradi 29 ya barabara zenye jumla ya Km. 2,536.4 na wakati huo huo miradi 7 ya barabara yenye jumla ya Km. 1,562 inaendelea kufanyiwa upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi. Hiki ni kielelezo dhahiri cha mafanikio makubwa ambayo yameiweka nchi yetu katika chati ya kuwa na miundombinu ya kisasa ya barabara.

(a) **Barabara**

Serikali imefanikiwa kukamilisha ujenzi wa barabara kama ifuatavyo:-

(i) Dodoma – Manyoni - (127)
(ii) Singida – Shelui - (Km 110)
(iii) Nzega – Ilula na Tinde - Isaka (Km 169)
(iv) Nangurukuru – Mbwemkuru - Mingoyo (Km 190)

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| (v) | Mkurunga | – | Kibiti | - | (Km 121) |
| (vi) | Pugu | – | Kisarawe | - | (Km 6.6) |
| (vii) | Singida | – | Isuna | - | (Km 63) |
| (viii) | Kyamyorwa – Buzirayombo – Geita | | | | (Km 220) |
| (ix) | Kigoma | – | Kidahwe | - | (Km 36) |
| (x) | Chalinze – Morogoro - Melela | | | - | (Km 129) |
| (xi) | Tunduma | – | Songwe | - | (Km 71) |
| (xii) | Dodoma | – | Morogoro | - | (Km 256) |
| (xiii) | Tarakea – Rongai – Kamwanga | | | - | (Km 32) |
| (xiv) | Rombo Mkuu | – | Tarakea | - | (Km 32) |
| (xv) | Geita | – | Busisi | - | (Km 92) |

Miradi ambayo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji ni:-

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| (i) | Manyoni | – | Isuna | - | (Km 54) |
| (ii) | Kagoma | – | Lisahunga | - | (Km 154) |
| (iii) | Tabora – Malagarasi – Uvinza – Kigoma | | | | (Km 364) |
| (iv) | Ndundu | – | Somanga | - | (Km 60) |
| (v) | Arusha | – | Namanga | - | (Km 105) |
| (vi) | Tanga | – | Horohoro | - | (Km 65) |
| (vii) | Mwandiga | – | Manyovu | - | (Km 60) |
| (viii) | Masasi | – | Mangaka | - | (Km 54) |
| (ix) | Singida – Babati – Minjingu | | | - | (Km 224) |

(b) **Bandari**

(i) **Bandari ya Kigoma**

Bandari ya Kigoma imeimarishwa kwa kununua mtambo wa kuondoa mchanga na hivyo kuongeza kina katika bandari hii. Kujengwa kwa Cherezo (docking yard) kunasaidia ukarabati wa meli na hivyo kuongeza usalama wa wasafiri.

(ii) **Bandari ya Kasanga**

Kukamilika ujenzi wa gati la Bandari ya Kasanga ambapo sasa meli mbili zinaweza kutia nanga kwa wakati mmoja.

(iii) **Uchukuzi kwa njia ya maji**

Serikali kupitia Mamlaka ya Bandari (TPA) imeandaa Mpango Kabambe wa Bandari (Ports Master Plan) ambao umebainisha miradi mbalimbali ya uendeshaji na upanuzi wa huduma za bandari.

Serikali imekamilisha uanzishaji wa Wakala za Uwezeshaji wa Biashara na Uchukuzi katika Ukanda wa Kati (Central Corridor Transit Transport Facilitation Agency – TTFA) na Ukanda wa TANZAM (Dar es Salaam Corridor) ambazo zitakuwa zikiratibu huduma za usafirishaji zinazopitishwa nchini mwetu na hivyo kuvutia wafanyabiashara kutumia miundombinu yetu ya uchukuzi na usafirishaji).

(c) **Vivuko**

Kukamilisha ujenzi wa kivuko kipya cha Rugezi katika wilaya ya Ukerewe Mkoa wa Mwanza ambao unaendelea hivi sasa.

**Mafanikio ya Kijamii**

**Elimu**

15. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita Serikali ya CCM imeendelea kufanya upanuzi mkubwa wa elimu katika ngazi zote. Kwa kushirikiana na wananchi na kwa kupitia programu na miradi mbalimbali kama vile MMEM, MMES na MEMKWA yamepatikana mafanikio makubwa kuanzia elimu ya awali, msingi, sekondari, ufundi na mpaka elimu ya juu. Elimu ya Watu Wazima na elimu maalumu nayo imepewa msukumo maalumu.

(a) **Elimu ya Awali**

(i) Idadi ya madarasa ya shule za Awali imeongezeka kutoka 18,455 mwaka 2005 hadi 28,048 mwaka 2009.

(ii) Wanafunzi wa Elimu ya awali wameongezeka kutoka 638,591 mwaka 2005 hadi 873,981 mwaka 2009, wakiwemo wanafunzi 2,146 wenye mahitaji maalumu.

(b) **Shule za Msingi**

(i) Shule za msingi zimeongezeka kutoka 13,679 mwaka 2005 hadi 15,675 mwaka 2009.

(ii) Idadi ya wanafunzi wa shule za msingi imeongezeka kutoka 7,083,063 mwaka 2005 hadi kufikia 8,441,553 mwaka 2009.

(iii) Uandikishaji wa wanafunzi wenye ulemavu umeongezeka kutoka 18,982 mwaka 2005 hadi 27,422 mwaka 2009.

(c) **Sekondari**

(i) Idadi ya shule za sekondari imeongezeka kutoka 1,745 (1,202 za Serikali na 543 zisizo za Serikali) mwaka 2005 hadi shule 4,102 (3,283 za Serikali na 819 zisizo za Serikali) mwaka 2009.

(ii) Uandikishaji wa wanafunzi (kidato cha 1-4) uliongezeka kutoka 401,598 mwaka 2005 hadi 1,401,559 mwaka 2009. Hili ni ongezeko la asilimia 179.

(iii) Serikali imejenga madarasa 11,266, nyumba za walimu 986 na shule za hosteli 52 katika kata 2,575 zilizopo.

(iv) Uandikishaji wa wanafunzi wa kidato cha 5 hadi 6 uongezeka asilimia 0.6 mwaka 2005 hadi asilimia 1.5 mwaka 2009.

(v) Serikali imegharamia elimu ya sekondari kwa wanafunzi 41,211 wanaotoka katika familia zenye kipato duni ambapo jumla ya Shilingi 6,677,537,600 zilitumika katika miaka ya 2006 na 2007.

(d) **Vyuo vya Ufundi**

(i) Udahili wa wanafunzi wa vyuo vya ufundi umeongezeka kutoka 40,059 mwaka 2005/2006 hadi kufikia 48,441 mwaka 2008/2009. Ongezeko hili limechangiwa na kuongezeka kwa vyuo vya ufundi kufikia 210 mwaka 2009 kutoka 183 mwaka 2005.

(ii) Pia vyuo vya ufundi stadi vimeongezeka kutoka 260 mwaka 2005 hadi 932 mwaka 2009.

(e) **Vyuo Vikuu**

(i) Idadi ya vyuo vikuu imeongezeka kutoka 26 mwaka 2005 hadi kufikia 32 mwaka 2009. Kati ya hivyo vipya kimoja ni cha Serikali **kinachojengwa Dodoma ambacho kitakapokamilika kitakuwa na wanafunzi 40,000** na kuwa ndicho kikubwa kuliko vyote nchini.

(ii) Wanafunzi wanaojiunga na vyuo vikuu vilivyopo nchini waliongezeka kutoka 55,296 mwaka 2005/2006 hadi 118,000 mwaka 2009/2010.

(iii) Kati yao wanafunzi 69,250 walipata mikopo ya elimu ya juu.

(iv) Jumla ya fedha zilizotolewa kwa ajili ya mikopo iliongezeka kutoka Tshs. 56.1 bilioni mwaka 2005/2006 hadi Tshs. 243 bilioni mwaka 2010.

(f) **Vyuo vya Ualimu**

(i) Serikali imepanua mafunzo ya walimu na kuishirikisha sekta binafsi.

(ii) Mpaka kufikia mwaka 2009 vyuo 79 nchini vimekuwa vikitoa mafunzo ya ualimu. Kati ya vyuo hivyo 34 ni vya Serikali na 45 ni vya watu na mashirika binafsi.

(iii) Idadi ya walimu wa awali iliongezeka kutoka 11,148 mwaka 2005 na kuwa 16,597 mwaka 2009.

(iv) Walimu wa shule za msingi waliongezeka kutoka 135,013 mwaka 2005 na kufikia 154,895 mwaka 2009.

(v) Idadi ya walimu wapya wa sekondari waliohitimu katika vyuo vikuu hapa nchini imeongezeka kutoka 500 mwaka 2005 hadi 19,124 mwaka 2010 kati yao 7,004 ni wa Diploma na Digrii 12,120.

(vi) Serikali ilitoa Shilingi bilioni 22.5 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba 2,501 za walimu wa shule za sekondari.

(vii) Miundombinu imeongezeka ambapo hadi mwaka 2009 nyumba za walimu 26,848, madarasa 79,102 na matundu ya vyoo 97,603 vimejengwa.

(g) **Vitabu na Vifaa vya Kufundishia**

Kumekuwepo na ongezeko kubwa katika bajeti ya sekta ya elimu ambalo limesaidia katika kukabiliana na tatizo la uhaba wa vitabu na vifaa vya kufundishia.

**Afya**

16. Utoaji wa huduma za Afya uliendelea kuboreshwa kwa kiasi kikubwa na kuleta mafanikio yafuatayo:-

(a) Kutoka mwaka 2005 hadi 2009, jumla ya zahanati 464, vituo vya afya 98 na nyumba za waganga 394 zilijengwa.

(b) Zahanati 1,037, vituo vya afya 285 na hospitali 112 zimekarabatiwa.

(c) Zahanati zimeongezeka kutoka 4,679 mwaka 2006 hadi 5,422 mwaka 2009.

(d) Vituo vya afya vimeongezeka kutoka 526 hadi kufikia 663 mwaka 2009.

(e) Idadi ya Madaktari imeongezeka kutoka 3,528 mwaka 2005 hadi 4,502 mwaka 2010. Vile vile idadi ya Madaktari Wasaidizi imeongezeka kutoka 9,028 hadi 14,017 katika kipindi hicho hicho.

(f) Idadi ya Wauguzi na Wakunga imeongezeka kutoka 18,123 mwaka 2005 hadi 23,886 mwaka 2010.

(g) Chanjo ya watoto dhidi ya kifua kikuu, polio, kifaduro, pepopunda, donda koo na homa ya ini iliongezeka kutoka watoto 1,243,388 mwaka 2005 hadi 1,356,421 mwaka 2009. Aidha, watoto waliopatiwa chanjo ya surua imeongezeka kutoka 1,267,716 hadi 1,455,100 katika kipindi hicho hicho.

(h) Katika kuzuia na kudhibiti malaria Tanzania Bara vyandarua 9,000,000 vyenye viuatilifu vimegawiwa kwa watoto wenye umri wa miaka 5 mwaka 2009/2010 bila malipo. Aidha, vyandarua 4,200,000 vya hati punguzo viliuzwa kwa mama wajawazito.

(i) Vifo vya watoto chini ya miaka 5 vimepungua kutoka 158 kwa kila 1000 mwaka 2005 hadi 75 kwa kila 1000 mwaka 2010.

(j) Aidha, katika kuleta ufanisi wa huduma za afya, mashine za kuchunguza damu, uwezo wa figo na ini pamoja na mashine za X-Ray zimewekwa katika kila hospitali ya wilaya na huduma za maabara zimeimarishwa.

(k) Kitengo cha magonjwa ya moyo kimeanzishwa na upasuaji unafanyika nchini. Aidha, mashine 7 za kusafisha figo zimefungwa na hivyo kuwezesha usafishaji wa figo kufanyika hapa nchini.

(l) Maambukizi ya UKIMWI yamepungua kutoka asilimia 7 na kufikia asilimia 5.

**Maji**

17. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita Serikali imeendeleza juhudi za kuwapatia wananchi wa Tanzania maji safi na salama. Katika kufanya hivyo Serikali imeongozwa na lengo la kuwapatia maji watu wa mijini kwa asilimia 90 na watu wa vijijini kwa asilimia 65. Miongoni mwa mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kipindi hiki ni pamoja na haya yafuatayo:-

(a) Mpaka mwaka 2009 kwa vijijini upatikanaji wa maji ulifikia asilimia 58.3 na mijini asilimia 80.3.

(b) Miradi 138 imekamilika katika wilaya mbalimbali hapa nchini na watu wanapata maji safi na salama. Miradi mingine mingi inaendelea kutekelezwa mijini na vijijini kwa ajili hiyo.

(c) Kukamilika kwa mradi mkubwa wa maji wa Ziwa Victoria. Mradi huu wa aina yake na wa kihistoria unawahakikishia wananchi wenzetu wapato milioni moja wa Mikoa ya Shinyanga na Mwanza kupata maji safi na salama.

(d) Miradi 53 ya maji katika miji mikuu ya wilaya na miji midogo imefanyiwa ukarabati.

(e) Miradi 7 ya taifa na 8 ya miji mikuu ya wilaya imekarabatiwa.

**Usawa wa Jinsia**

18. Kwa kuzingatia Imani ya CCM juu ya usawa wa binadamu na wito wa kimataifa juu ya usawa wa jinsia, Serikali chini ya uongozi wa CCM imeweza kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kuongeza ushiriki wa wanawake katika Bunge, Baraza la Wawakilishi na Madiwani kutoka asilimia 30 hadi 40. Aidha, ushiriki wa wanawake umeongezeka pia katika nafasi mbalimbali za uongozi na utendaji Serikalini na katika Taasisi za Umma.

(b) Kuanzisha Benki ya Wanawake.

(c) Kupitisha Sheria ya Mtoto.

## SURA YA PILI

## KUJENGA MSINGI WA UCHUMI WA KISASA WA TAIFA LINALOJITEGEMEA

19. Mwelekeo wa Sera za CCM katika miaka ya 2010 hadi 2020 umeainisha jukumu kubwa la nchi yetu katika kipindi hiki ni kutekeleza lengo la Dira 2025 la kuleta mapinduzi ya uchumi yatakayoitoa nchi kutoka kwenye dimbwi la uchumi ulio nyuma na tegemezi na kuiingiza katika mkondo wa uchumi wa kisasa wa taifa linalojitegemea. Ili kufikia lengo hili Mwelekeo wa CCM unahimiza Serikali kutekeleza majukumu yafuatayo:-

(a) Kujenga Uchumi wa Kisasa wa Taifa Linalojitegemea, yaani modenaizesheni ya uchumi

(b) Kutekeleza Sera ya Kuwawezesha Wananchi Kiuchumi

(c) Kutekeleza Sera ya Dola Kupanga Mipango na Kusimamia Uchumi

(d) Kuongeza uwezo wa Maarifa (sayansi na teknolojia) katika nchi kwa kutilia mkazo ubora wa Elimu na Raslimali Watu ya Nchi.

(e) Kuweka msingi wa miundombinu ya uchumi wa kisasa kwa kuhakikisha nishati yenye uhakika na uboreshaji wa miundombinu na huduma za kiuchumi kwa jumla.

(f) Kutumia fursa za kijiografia katika kukuza uchumi wa kisasa wa nchi.

(g) Kuhimiza Watanzania kujenga utamaduni wa kufanya kazi

(h) Kuhakikisha uwiano wa mapato ili kujenga amani katika nchi na utulivu wa uchumi na maendeleo

(i) Kuweka methodolojia ya kusimamia utekelezaji wa majukumu haya ili kuhakikisha yanafanikiwa

20. Changamoto za kuibadili nchi yetu kutoka uchumi ulio nyuma na tegemezi kuelekea kwenye uchumi wa kisasa wa taifa linalojitegemea ni nyingi. Uzoefu wa utekelezaji tulioupata katika kipindi cha Mwelekeo wa Miaka 2000 hadi 2010 na kipindi cha Ilani ya Uchaguzi ya 2005 hadi 2010 cha Awamu ya Nne unaonyesha kuwa jukumu hili linapaswa liendelezwe katika kipindi cha Ilani hii kwa kuzingatia:

(a) Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025

(b) Dira ya Maendeleo Zanzibar 2020

(c) Malengo ya Milenia

(d) Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania, **(MKUKUTA)**

(e) Mkakati wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania **(MKURABITA)**

(f) Kilimo Kwanza

21. Ilani hii ya 2010-2015 inalenga kuongeza kasi ya utekelezaji wa mchakato wa kujenga uchumi wa kisasa na taifa linalojitegemea kwa kuwashirikisha na kuwawezesha kiuchumi wananchi.

22. Dhana ya Kujenga Uchumi wa Kisasa inalenga katika modenaizesheni ya uchumi. Modenaizesheni kimsingi ni kuongeza maarifa na matumizi ya sayansi na teknolojia katika sekta za uzalishaji. Modenaizesheni ya uchumi inalenga katika kuongeza uzalishaji, ufanisi na tija katika uchumi hususan katika kilimo, ufugaji, uvuvi na viwanda.

23. Mapinduzi ya kilimo ni msingi wa ukombozi wa uchumi wa nchi yetu. Katika kipindi cha Ilani hii 2010-2015 utekelezaji utaelekezwa katika modenaizesheni ya kilimo kwa kutilia mkazo Programu ya Kilimo Kwanza, upatikanaji fedha za uwekezaji

katika sekta ya kilimo, mbegu bora, zana za kisasa,matumizi ya mbolea, elimu kwa wakulima kuhusu kanuni za kilimo, huduma za ugani, mikopo kwa wakulima, upatikanaji wa masoko, utafiti na matokeo, kuongeza thamani ya mazao ya kilimo.

24. Kufikiwa kwa lengo hili kutategemea sana mchango wa Serikali katika kusimamia mikakati ya kusimamia mapinduzi ya kilimo, ya kuunda Benki ya Kilimo na kutoa msukumo wa kimaeneo, kimkoa na kikanda katika mazao, uwekezaji na masoko.

25. Ufugaji ni moja ya sekta zinazohitaji kusimamiwa ili iweze kuchangia ipasavyo katika uchumi wa kisasa. Katika kipindi cha Ilani 2010-2015 mkazo utaelekezwa katika matumizi ya maarifa katika sekta ya mifugo. Jukumu kuu la msingi katika ufugaji litakuwa ni kuleta mabadiliko yatakayoiondoa sekta hii kutoa uduni wa ufugaji na kuwabadili wafugaji wetu kutoka wafugaji wahamaji. Mkazo utaelekezwa katika kutatua matatizo ya malisho na maji na kuwafikisha wafugaji katika ukulima mchanganyiko na ufugaji wa mabandani wenye tija kubwa, utakaotoa nyama na maziwa bora.

26. Uvuvi ni moja ya sekta za uchumi ambazo hazijapatiwa msukumo wa kutosha. Modenaizesheni katika uvuvi italenga katika kuwapatia maarifa wavuvi yatakayobadili na kuongeza uzalishaji wa samaki. Kuongeza ufanisi na tija na kubadili maisha ya wavuvi ni moja ya mapinduzi yanayolengwa katika Ilani ya 2010-2015. Katika kutekeleza hili Serikali itatilia mkazo uwezeshaji wa wavuvi, kuendeleza viwanda vya samaki, kusimamia uvunaji endelevu wa samaki katika bahari kuu.

27. Modenaizesheni ya uchumi itazingatia umuhimu wa viwanda kuwa ni kiongozi wa uchumi wa kisasa. Katika kuzingatia ukweli huu Ilani hii ya 2010-2015 itatekeleza dhana hiyo kutoa msukumo katika mapinduzi ya viwanda, kuhamasisha maendeleo ya sayansi, teknolojia na uhandisi, viwanda vya msingi, viwanda vya kati na viwanda vidogo.

28. Ufikiaji wa lengo letu kla ujenzi wa uchumi wa kisasa wa Taifa linalojitegemea utategemea sana ushiriki wa wananchi wetu kupitia Sera ya Chama ya Uwezeshaji Wananchi. Sera hii itatekelezwa na kuimarishwa katika kipindi cha Ilani hii kwa Serikali kuendeleza yafuatayo:

(a) Mkakati wa MKURABITA

(b) Ushirika

(c) Mifuko ya Uwezeshaji:-

  (i) Mfuko wa Wajasiriamali Wadogo

  (ii) Mfuko wa Mikopo Makampuni ya Wajasiriamali Wadogo na wa Kati (SMEs)

  (iii) Mfuko wa Pembejeo za Kilimo

  (iv) Mfuko wa Maendeleo ya Jamii

  (v) Benki ya Wanawake

29. Aidha Sera ya Uwezeshaji itapewa msukumo mkubwa ili Watanzania waweze kuwezeshwa kushindana katika uchumi wa dunia na ule wa kanda.

30. Nchi yetu inahitaji uchumi imara na unaokua kwa kasi kubwa na endelevu ili kutatua tatizo letu la umaskini na utegemezi. Ni mapinduzi ya kilimo na viwanda ndiyo yatakayotuhakikishia kufika katika lengo hilo na nchi yetu kuwa na uchumi wa kati.

## SURA YA TATU

## SEKTA ZA UZALISHAJI MALI

### Mapinduzi ya Kilimo

***Kilimo ndio msingi wa uchumi wa kisasa na njia sahihi ya kuutokomeza umasikini.***

31. Chama Cha Mapinduzi kinaamini kwa dhati kwamba kilimo cha kisasa kinachotumia Kanuni na zana bora za kilimo ndio ufunguo wa maendeleo ya uchumi wa nchi yetu. Kilimo cha kisasa kina uwezo wa kutoa mazao mengi zaidi kutoka kila ekari iliyolimwa. Kwa nchi yetu, ziada hiyo ya mazao ina faida kubwa zifuatazo:-

    (a) Kuipatia kila familia, kijiji na Taifa chakula cha kutosha ili kukomesha njaa.

    (b) Kulipatia Taifa mavuno mengi ya kuuza ili kupata fedha za kigeni kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

    (c) Ziada ya mazao huunda mazingira muafaka ya kuanzishwa viwanda vya usindikaji na utengenezaji wa bidhaa za viwandani.

    (d) Familia yenye ziada ya mazao huutokomeza umaskini kwa kuuza ziada hiyo kwenye soko na kupata fedha za kujiletea maendeleo.

32. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita ya utekelezaji wa Ilani ya mwaka 2005-2010, Serikali zetu zilichukua hatua kubwa katika kukipatia kilimo mwelekeo wa

kisasa ili kiondokane na zana duni, mashamba madogo, kutozingatia kanuni bora za kilimo na kuridhika na mavuno ya kujikimu.

33. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo ya utekelezaji wa Ilani ya 2010-2015, Chama kitazielekeza Serikali kutekeleza kwa ukamilifu malengo ya **Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo** (**ASDP**) pamoja na kaulimbiu ya **Kilimo Kwanza** inayotoa msukumo katika kutekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Kuanzisha Benki ya Kilimo yenye uwezo mkubwa ili ianze kuwakopesha wakulima wakubwa na wadogo kwa masharti nafuu.

(b) Kutumia uongozi shirikishi katika kusimamia kilimo na kuwafikishia wakulima vijijini maarifa yanayohusu kanuni za kilimo bora cha mazao wanayolima.

(c) Kuziweka tayari Benki Kuu na Hazina kukipatia kilimo chetu fedha za kutosha kwa kuhakikisha kwamba Bajeti ya Serikali haiwi kizuizi cha maendeleo ya kilimo nchini.

(d) Kuongeza upatikanaji na utumiaji wa pembejeo za kilimo, hususan mbolea, mbegu na miche bora na kuweka mfumo utakaohakikisha upatikanaji wa pembejeo hizo kwa wakulima.

(e) Kuongeza upatikanaji na matumizi ya zana za kilimo kwa kuishirikisha sekta binafsi, kuhamasisha na kuwezesha vikundi vya wakulima, hususan vijana kupata mikopo ya pembejeo na zana za kilimo kutoka kwenye Mfuko wa Pembejeo.

(f) Kuimarisha mashamba ya mbegu ya serikali ili kuongeza uzalishaji wa mbegu bora za mazao ya nafaka, mikunde na mbegu za mafuta na kuzisambaza kwa walengwa ili wazitumie.

(g) Kuhamasisha uzalishaji wa mazao ya kilimo ya aina zote, hususan mazao makuu ya biashara, mazao ya chakula, mboga na matunda, mbegu za mafuta na muhogo ili mavuno makubwa ya kila zao yapatikane ifikapo mwaka 2015 kwa viwango vinavyopimika.

(h) Kuweka msukumo mkubwa wa kilimo cha umwagiliaji maji katika maeneo stahiki ili kuhakikisha kwamba ifikapo mwaka 2015 karibu asilimia 25 ya mahitaji yetu ya chakula inapatikana kwa njia ya kilimo hicho.

(i) Kuimarisha huduma za ugani kwa kuongeza kasi ya kufundisha na kuajiri wataalam wa fani mbalimbali hasa wenye vyeti vya kilimo na kuwaeneza wanakohitajika hasa vijijini na kuwajengea mazingira mazuri ya kazi.

(j) Kuimarisha huduma za udhibiti wa visumbufu na magonjwa ya mimea kwa kujenga uwezo wa kudhibiti visumbufu vya mazao mara vinapojitokeza ili kumwezesha mkulima kupunguza upotevu wa mazao kabla na baada ya mavuno.

(k) Kuhamasisha ujenzi na matumizi ya maghala bora ya kuhifadhia mazao na kutoa mafunzo juu ya teknolojia sahihi za hifadhi bora kwa lengo la kupunguza upotevu wa chakula. Mpango mkakati uandaliwe wa kupanua hifadhi ya mazao ya chakula katika maeneo ya nchi ambako mazao ya chakula yanalimwa kwa wingi.

(l) Kuimarisha usindikaji wa mazao mbalimbali katika ngazi ya kaya ili kuongeza thamani na muda wa matumizi na upatikanaji wa chakula kwa ujumla.

(m) Kupima maeneo ya kilimo na mashamba ya wakulima wapate hati miliki na kuhimiza matumizi bora ya ardhi ili kupunguza migogoro ya kijamii kama vile kati ya wazalishaji wa mazao na wafugaji.

(n) Kusimamia utaratibu wa mashindano ya kilimo kinachozingatia kanuni bora za kilimo kati ya vijiji, kata, tarafa, wilaya na mikoa.

(o) Kuimarisha uongozi wa Vyama vya Ushirika na kuvijengea uwezo kujiendesha kwa ufanisi.

(p) Kuimarisha shughuli za ukaguzi na usimamizi wa Vyama vya Ushirika nchini.

(q) Kuweka kanda zinazoeleweka za mazao ya chakula na ya biashara kwa kuzingita hali ya hewa na uzoefu uliopo. Mazao yanayohusika yalimwe kwa wingi katika kanda hizo.

(r) Kuwezesha Halmashauri 133 kununua vitendea kazi kwa wataalamu ifikapo mwaka 2015.

(s) Kuzalisha mbolea kwa wingi kwa ajili ya mapinduzi ya kilimo tunayoyafanya na kuhamasisha makampuni ya mbolea ili yaingize mbolea kwa wingi kukidhi mahitaji ya tani 385,000 ifikapo mwaka 2015.

**Sekta ya Umwagiliaji**

34. Kutokana na umuhimu wa Sekta ya Umwagiliaji katika kukuza uchumi wa taifa na wa wananchi katika kipindi hiki kwa kuongeza uhakika wa upatikanaji wa chakula nchini, Chama kitaitaka Serikali kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kuendelea kutekeleza umwagiliaji kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo kwa kuongeza eneo lenye miundombinu ya umwagiliaji kutoka hekta 326,492 za Juni 2010 hadi hekta 1,000,000 ifikapo mwaka **2015** na hivyo kujitosheleza kwa zao la mpunga. Sekta binafsi itashirikishwa katika uendelezaji na uwekezaji kwenye kilimo cha umwagiliaji.

(b) Kukamilisha Mkakati na Sheria ya Umwagiliaji.

(c) Kujenga na kukarabati miundombinu ya umwagiliaji kwa wakulima wadogo na wa kati ili kuongeza uzalishaji na ufanisi wa matumizi ya maji;

(d) Kujenga na kukarabati mabwawa ya kuvuna na kuhifadhi maji ya mvua na mito kwa ajili ya umwagiliaji;

(e) Kujenga uwezo wa Taasisi zinazohusika na umwagiliaji katika ngazi ya taifa, Halmashauri na wakulima katika usimamizi na uendeshaji endelevu wa miradi ya umwagiliaji.

(f) Kutoa msukumo mpya katika uanzishwaji wa kituo cha mafunzo na shughuli za utafiti wa umwagiliaji na matumizi bora ya maji.

**Mapinduzi ya Ufugaji**

35. Tanzania hivi sasa inakadiriwa kuwa na ng'ombe milioni 19.1, mbuzi milioni 13.6, kondoo milioni 3.6, nguruwe milioni 1.6 na kuku milioni 56. Kati ya ng'ombe hao, 605,000 ni wa maziwa. Aidha, kati ya kuku hao, 22 milioni ni wa kisasa wakiwemo milioni 8 wa mayai na milioni 14 wakiwa ni wa nyama.

36. Hivyo, bado nchi yetu inafuga ng'ombe 18,496,000 na kuku milioni 34 kwa utaratibu wa jadi likiwemo tatizo sugu la wafugaji kuhamahama wakitafuta malisho na maji.

37. Kutokana na ufugaji huo kuwa wa jadi kwa sehemu kubwa, mchango wa mifugo kwenye uchumi wa Taifa na katika kuutokomeza umasikini bado ni mdogo sana. Kwa mfano, mwaka 2007 sekta ya mifugo ilichangia kwenye pato la Taifa asilimia 4.7 ambapo mwaka 2008 mchango wake ulishuka hadi asilimia 4.6 tu.

38. Katika kipindi cha Ilani hii ya miaka 2010-2015, Chama Cha Mapinduzi kitazielekeza Serikali kuiendeleza sekta ya mifugo kwa ari zaidi, nguvu zaidi na

kasi zaidi ili kuiwezesha kutoa mchango mkubwa kwenye pato la Taifa kwa kuchukua hatua zifuatazo:-

(a) Serikali iandae programu kabambe ya kuendeleza sekta ya mifugo na ufugaji. Programu hiyo ijumuishe pamoja na mambo mengine masuala ya uendelezaji wa maeneo ya malisho, kuchimba na kujenga malambo, mabwawa, majosho na huduma za ugani ili hatimaye wafugaji waondokane na ufugaji wa kuhamahama.

(b) Benki ya Kilimo itakayoanzishwa iwe pia Benki ya Mifugo ili iweze pia kutoa mikopo kwa wasomi wenye nia ya kufuga na kuwawezesha kuingia kwa wingi katika ufugaji wa kisasa.

(c) Kuelimisha wafugaji uwiano kati ya idadi ya mifugo na eneo.

(d) Serikali isimamie kwa ufanisi mkubwa mradi wa kopa ng'ombe, lipa ng'ombe kama hatua ya kueneza ufugaji wa kisasa wenye tija kubwa.

(e) Kuendeleza elimu kwa Wafugaji ili wajue kuwa mifugo waliyonayo ni mali inayoweza kuvunwa katika umri na uzito muafaka unaokidhi mahitaji ya soko, ili kuwaondolea umaskini wao badala ya kuridhika na wingi wa mifugo iliyo duni na maisha ya kuhamahama.

(f) Uzalishaji wa mitamba upanuliwe kwa kiwango kikubwa kwa Serikali kuivutia na kuiwezesha sekta binafsi katika uzalishaji na ufugaji wa kisasa.

(g) Kufufua na kujenga majosho na malambo mapya kwa ajili ya mifugo na kuhimiza uogeshaji endelevu.

(h) Kuimarisha utafiti wa mifugo kwa kuboresha na kuhifadhi kosaafu za mifugo ya asili ili kuongeza uzalishaji na tija.

(i) Kuimarisha huduma za ugani na mafunzo ya wataalamu na wafugaji.

(j) Kuongeza na kuimarisha vituo vya uzalishaji mbegu bora za mifugo na kuhimiza matumizi ya mbegu hizo.

(k) Kuimarisha huduma za afya ya mifugo kwa kudhibiti magonjwa ya mifugo hasa ya milipuko na uanzishwaji wa Maeneo Huru kwa Magonjwa ya Mifugo.

(l) Kuhimiza wafugaji watekeleze kanuni za ufugaji bora na kuingia katika ufugaji endelevu wa kisasa na kibiashara unaozingatia hifadhi ya mazingira.

(m) Kuhamasisha uanzishaji na uimarishaji wa vikundi vya ushirika wa wafugaji.

(n) Kuhamasisha ushirikishwaji wa sekta binafsi katika utoaji wa huduma mbalimbali za mifugo.

**Mapinduzi ya Uvuvi**

39. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi yenye maeneo mengi na makubwa ya maji baridi na maji ya bahari yaliyosheheni rasilimali nyingi za uvuvi ambamo shughuli za uvuvi hufanyika. Nchi yetu ina ukanda wa pwani wenye urefu wa kilometa 1,424 na upana wa maili za majini zipatazo 200. Eneo hilo limegawanyika katika maji ya Kitaifa yenye upana wa maili za majini 12 sawa na kilometa za mraba 64,000 kwa upande mmoja na upande wa pili ni wa Bahari Kuu yenye upana wa maili za majini 188 sawa na kilometa za mraba 223,000.

40. Eneo letu la maji baridi lenye maziwa makubwa 3 na madogo 29 lina jumla ya kilometa za mraba 54,277 ambazo zinaweza kutumika kwa uvuvi. Katika maeneo hayo ya maji baridi na maji ya bahari, mwaka 2008 jumla ya tani 335,024 za samaki zilivuliwa nchini. Kati ya hizo, tani 324,960 sawa na asilimia 97 zilivuliwa na wavuvi wadogo wapato 170,038 sawa na wastani wa tani 1.9 kwa kila mvuvi kwa mwaka. Aidha, tani 10,114 zilizobaki zilivuliwa na meli kubwa katika Bahari Kuu. Sekta ya uvuvi mwaka 2007 ilichangia asilimia 1.6 tu kwa pato la Taifa na asilimia ndogo zaidi ya 1.3 mwaka 2008.

41. Kwa kuzingatia ukubwa wa maeneo yetu ya uvuvi na uwingi wa rasilimali za uvuvi tulizonazo, Chama Cha Mapinduzi katika kipindi cha Ilani hii ya 2010-2015 kitazielekeza Serikali kuiendeleza sekta ya uvuvi ili iwe ya kisasa zaidi na iweze kuchangia kwa kiwango kikubwa kwenye pato la Taifa kwa kuchukua hatua zifuatazo:-

(a) Wizara ianzishe na kuendesha vyuo vyake vya uvuvi ili iweze kuandaa wataalam wengi wa sekta ya uvuvi kukidhi mahitaji yote yanayotakiwa kwa ajili ya kuboresha uvuvi nchini.

(b) Kuweka ulinzi madhubuti wa bahari zetu dhidi ya wavuvi haramu ikiwa ni pamoja na kukamata vyombo vyao vya uvuvi na kuwatoza fidia kwa mujibu wa sheria.

(c) Kuweka na kutekeleza programu yenye malengo yanayopimika mwaka hadi mwaka kuhusu haja ya kuleta mapinduzi ya uvuvi yanayotumia zana na maarifa ya kisasa.

(d) Kuimarisha ushirikishwaji wa jamii na wadau katika ulinzi, usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi.

(e) Kuimarisha miundombinu ya uvuvi kwa kujenga mialo, masoko ya kisasa, vituo vya kutotolea vifaranga vya samaki na maabara.

(f) Kuboresha mazao ya uvuvi kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi.

(g) Kujenga mazingira ya kuvutia uwekezaji katika sekta ya uvuvi hususan ujenzi wa viwanda vya kusindika samaki.

(h) Kuhamasisha wawekezaji wa ndani na wa nje kuwekeza katika uvuvi kwenye Bahari Kuu.

(i) Kuimarisha na kuendeleza uanzishwaji wa maeneo tengefu kwenye maziwa makuu hususani Ziwa Victoria, Tanganyika na Nyasa.

(j) Kuhamasisha uimarishaji na uanzishaji wa vikundi vya ushirika wa wavuvi na wafugaji wa samaki.

(k) Kuimarisha usimamizi wa mazingira katika maeneo ya uvuvi, ukuzaji wa viumbe kwenye maji na maeneo tengefu.

(l) Kuhimiza shughuli mbadala za kiuchumi kwa jamii za wavuvi ili kupunguza shinikizo la uvuvi kwenye maji ya asili na maeneo tengefu.

## Wanyamapori na Misitu

42. Wakati tunapata uhuru mwaka 1961, nchi yetu ilikuwa na misitu mingi ambayo hivi sasa imepungua kutokana na ongezeko kubwa la makazi ya watu na kupanuka kwa kilimo. Aidha, kutokana na ukataji ovyo wa misitu na uwindaji haramu wa wanyamapori, rasilimali hizo zinaweza kutoweka kwenye uso wa nchi yetu na kuleta jangwa kama Taifa halitakuwa makini kiasi cha kutosha katika hifadhi ya misitu na wanyamapori.

43. Umuhimu wa wanyamapori na misitu ambao Taifa limeutambua tangu mwanzo wa uhuru wetu, sasa unazidi kuongezeka siyo tu katika kuvutia watalii nchini lakini pia katika kutunza mazingira yanayotuzunguka ya hewa, udongo na maji ili

nchi yetu iweze kutoa mchango wake stahiki katika kupunguza kasi ya mabadiliko ya tabianchi ambayo yameikumba sayari dunia tunamoishi.

44. Katika kipindi cha Ilani hii, Chama Cha Mapinduzi kitaitaka Serikali ielekeze nguvu zake katika kuhifadhi, kulinda, kuendeleza, kudumisha, kuboresha na kuvuna maliasili ya wanyamapori, misitu na nyuki kwa manufaa ya Taifa kwa kuchukua hatua zifuatazo:-

(a) Kuongeza msukumo katika kuendeleza ufugaji wa nyuki kwa ajili ya kuzalisha asali na nta kibiashara.

(b) Kuweka utaratibu shirikishi wa upandaji miti, uvunaji na udhibiti wa moto. Ushirikishaji huo utakuwa wa sekta binafsi, NGOs na vijiji.

(c) Kuwezesha jamii zinazozunguka maeneo ya hifadhi kunufaika na rasilimali za wanyamapori na misitu.

(d) Kuboresha miundombinu ndani ya mapori ya akiba, hifadhi za wanyamapori na misitu.

(e) Kuendelea kuboresha mazingira ya makazi ya watumishi wanaoishi katika mazingira magumu.

**Utalii**

45. Katika kipindi cha miaka 2005-2010, Serikali chini ya uongozi wa CCM imeitumia Bodi ya Utalii kutangaza kwa bidii vivutio vya utalii tulivyonavyo ndani na nje ya nchi kwa kuandaa, kuchapisha na kusambaza vipeperushi ambapo jumla ya vipeperushi 30,000, nakala 30,000 za filamu, majarida 30,000, DVD 30,000 na taarifa 5,000 zilichapishwa na kusambazwa ikiwa ni pamoja na kushiriki katika maonyesho 21 nje ya nchi. Aidha, vituo vya CNN vilitumika kurusha matangazo ya utalii wetu kwa miezi sita mfululizo tangu Septemba 2007 hadi Februari 2008.

46. Kutokana na juhudi hizo idadi ya watalii wa ndani iliongezeka kutoka wastani wa 436,000 mwaka 2005/2006 hadi 639,000 mwaka 2008/2009. Wakati huo huo idadi ya watalii waliotembeleaTanzania kutoka nchi za Asia iliongezeka kutoka 23,542 mwaka 2006 hadi watalii 26,070 mwaka 2009. Katika masoko ya zamani, idadi ya watalii iliongezeka kutoka 612,754 mwaka 2005 hadi watalii 770,376 mwaka 2008. Sekta ya utalii katika kipindi hicho iliingizia Taifa jumla ya dola za Marekani bilioni 2.8.

47. Katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani hii, Chama kitaielekeza Serikali iendelee kuitangaza hazina ya utalii tuliyonayo kwa mbinu za kisasa ili kukuza zaidi mchango wa utalii kwa pato la Taifa kwa kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kujenga Chuo Cha Utalii ili kuimarisha mafunzo ya hoteli na utalii kwa lengo la kuongeza wingi na ubora wa watumishi wa huduma hizo.

(b) Kukuza mwamko na kuendesha kampeni za kuwashawishi Watanzania kujenga utamaduni wa kutembelea vivutio vya utalii.

(c) Kupanua wigo wa aina za utalii kwa kuendeleza utalii wenye kuhusisha utamaduni, mazingira, makumbusho (historia) na michezo kama vile golfu.

(d) Kujihusisha kwa ukamilifu katika kutangaza fursa za kitalii zilizomo nchini na kuongeza bajeti ya kutangaza utalii ifanane na zile za nchi jirani.

(e) Kufanya juhudi maalumu za kutafuta masoko mapya ya utalii katika nchi zinazoinukia kiuchumi kama vile China na nchi nyingine za Asia.

(f) Kuandaa mikakati ya kuziba mianya ya uvujaji wa mapato ya utalii.

(g) Kuhimiza wawekezaji wa ndani na nje kujenga hoteli za kitalii za hadhi ya nyota 3 hadi 5.

(h) Kuzitathmini hoteli zilizopo na kuzipanga katika madaraja ya nyota zinayostahili. Wakati huo huo kuhakikisha kuwa hoteli zinakuwa katika hali ya unadhifu.

(i) Kuendeleza jitihada za kuhifadhi mazingira katika mbuga za wanyama, misitu fukwe, za bahari na maziwa.

(j) Kuwavutia watalii wa nje kwa kuboresha huduma na uzalishaji wa bidhaa zenye ubora kwa kutumia teknolojia rahisi na za kisasa ili ziwavutie watalii.

(k) Kuhakikisha kuwa kuna usafiri wa uhakika wa ndege ili kuimarisha utalii.

**Mapinduzi ya Viwanda**

48. Katika kipindi cha miaka 2005-2010, Sekta ya viwanda ilitarajiwa kukua kufikia asilimia 15. Ukuaji halisi uliongezeka kutoka asilimia 8.5 mwaka 2005/2006 hadi asilimia 9.9 mwaka 2008/2009. Matatizo ya msingi yaliyosababisha ukuaji wa sekta ya viwanda kuwa na sura hiyo ni pamoja na haya yafuatayo:-

(a) Kukatikakatika mara kwa mara kwa maji na umeme viwandani.

(b) Uwekezaji mdogo kwenye maendeleo ya viwanda, hasa viwanda mama na viwanda vya usindikaji wa mazao ya kilimo.

(c) Uduni wa teknolojia zinazotumiwa na wazalishaji.

(d) Udhaifu wa menejimenti na stadi za biashara na masoko.

49. Katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani hii ya 2010 – 2015, Chama Cha Mapinduzi kitaitaka Serikali iikuze sekta ya viwanda kutoka asilimia 9.9 ya sasa hadi asilimia 15 mwaka 2015 kwa kuweka mazingira mazuri kwa ajili ya maendeleo endelevu ya sekta za viwanda, biashara na masoko kwa kuzingatia mambo yafuatayo:-

(a) Kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi katika uwekezaji na biashara katika soko la ushindani.

(b) Kujenga na kuimarisha ujuzi katika biashara na kuweka msukumo zaidi katika kutumia fursa za masoko.

(c) Kujenga mifumo imara ya viwanda, biashara na masoko yenye kuendeleza na kukuza mauzo nje.

(d) Kuimarisha kifedha Benki ya Rasilimali Tanzania (TIB) ili kiwe chombo madhubuti cha kuchochea mapinduzi ya viwanda nchini kwa kutoa mikopo ya muda mrefu na riba nafuu kwa wawekezaji wakubwa, wa kati na wadogo nchini kote.

(e) Kuwekeza katika mradi wa makaa ya mawe ya Mchuchuma, Chuma cha Liganga na viwanda vya kemikali na mbolea katika Kanda za Maendeleo kikiwemo kiwanda cha mbolea aina ya UREA mkoani Mtwara na kuwezesha kiwanda cha Minjingu kuzalisha mbolea bora ya NPK na MPR ili kufikia lengo lililowekwa.

(f) Kuimarisha uzalishaji mali viwandani kwa kuvifufua na kuviendeleza kwa teknolojia ya kisasa viwanda vyote ambavyo viliuzwa huko nyuma na kisha kutelekezwa.

(g) Kuboresha vivutio kwa ajili ya uwekezaji kwenye viwanda vitakavyotumia malighafi mbalimbali ziliopo nchini vikiwemo viwanda vya nguo, ngozi, usindikaji wa matunda, mbogamboga na usanifu wa madini ya vito.

(h) Kuendelea kuhamasisha uanzishaji na uimarishaji wa Maeneo Maalumu ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje (EPZ) na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi (SEZ).

(i) Kuendelea kutekeleza mkakati unganishi wa kufufua na kuendeleza viwanda vya ngozi.

(j) Kuandaa taarifa kuhusu fursa za uwekezaji katika miradi ya maendeleo ya viwanda nchini.

50. Kuhusu viwanda vidogo, Serikali itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuendeleza programu ya Muunganisho wa Ujasiriamali Vijijini kwa kutoa ushauri, mafunzo, mitaji na huduma za kiufundi kwa wajasiriamali.

(b) Kuongeza mchango wa viwanda vidogo na biashara ndogo (SMEs) katika pato la Taifa kutoka asilimia 33 ya GDP hivi sasa kufikia asilimia 40 mwaka 2015.

(c) Kuendeleza, kuzalisha na kusambaza teknolojia za kuongeza thamani ya mazao kupitia vituo vya SIDO vilivyopo Mbeya, Arusha, Kilimanjaro, Lindi, Iringa na Kigoma.

(d) Kutoa elimu na kuwajengea uwezo wakulima wa kusindika mazao kabla ya kuyauza kama vile usindikaji wa asali, utengenezaji wa mvinyo, utengenezaji wa juisi pamoja na ufungashaji wa bidhaa kwa kutumia teknolojia ya TBS.

(e) Kuwaunganisha wajasiriamali wadogo na makampuni makubwa yaliyotayari kununua bidhaa zao.

(f) Kujenga uwezo wa SIDO na kuwatafutia vyanzo vya fedha ili kuwawezesha kutoa mafunzo ya usindikaji kwa wajasiriamali wadogo. Aidha, Sheria iliyoanzisha SIDO itafanyiwa mapitio ili iendane na mahitaji ya uchumi wa sasa.

(g) Kuendeleza miundombinu ya viwanda vidogo na biashara ndogo.

51. Kuhusu biashara, Serikali itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuhamasisha matumizi ya fursa za masoko ya ndani, kikanda na kimataifa, zikiwemo fursa za masoko ya AGOA, EBA, China, Japan, Canada na India ili kukuza biashara ya nje kwa kiwango kikubwa.

(b) Kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo wajasiriamali kuhusu mbinu za kuyafikia masoko ya nje.

(c) Kuendelea na majadiliano ya ubia wa kiuchumi kati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Ulaya (EU).

(d) Kuendelea na utekelezaji wa uanzishwaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki na kuendelea kutekeleza Itifaki ya Biashara ya Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC).

(e) Kufanya utafiti wa kina juu ya gharama za kufanya biashara nchini kwa lengo la kupunguza gharama hizo na kuchochea ukuaji wa biashara.

52. Kuhusu Mapinduzi ya kilimo, Serikali itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuanzisha vituo vitatu vya biashara vya kanda katika mikoa ya Mwanza, Mbeya na Arusha.

(b) Kuratibu na kuhamasisha ushiriki wa wajasiriamali wa Tanzania katika maonesho ya biashara ya kimataifa ndani na nje ya nchi.

(c) Kufanya utafiti wa masoko na bei ili kupanua wigo wa mahitaji ya masoko ya bidhaa zetu.

(d) Kuanzisha programu ya kuwa na utambulisho wa kitaifa kwa bidhaa.

53. Kuhusu masoko, Serikali itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kukamilisha mkakati wa Sera ya Masoko na Bidhaa za Kilimo.

(b) Kuendeleza miundombinu ya masoko ya mikoa na kuanzisha masoko katika vituo vya mipakani ili kukuza biashara ya ndani na kikanda.

(c) Kutekeleza mkakati wa kukuza mauzo nje na mpango unganishi wa biashara.

(d) Kuendeleza biashara ya ndani ikiwa ni pamoja na kujenga dhana ya kutumia bidhaa zilizozalishwa Tanzania (NUNUA BIDHAA ZA TANZANIA).

(e) Kuboresha na kupanua wigo wa biashara mtandao katika ngazi ya Wilaya, Mkoa hadi Taifa.

(f) Kuwalinda wajasiriamali wa ndani kwa kutoingiza bidhaa mbalimbali kutoka nje ambazo zinaua soko la ndani la bidhaa zao, kwa mfano samani.

(g) Kupanua matumizi ya simu za viganjani katika kutoa taarifa za bei ya mazao na masoko kwa wakati. Aidha, kuangalia uwezekano wa kuanzisha mbao za matangazo katika ngazi ya Wilaya na Mkoa ili kutoa taarifa mbalimbali ikiwemo bei na masoko kwa wakati muafaka.

(h) Kuendeleza mchakato wa kuanzisha Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara.

(i) Kuendeleza miundombinu ya masoko na kuanzisha masoko mipakani kama vile Karagwe, Kigoma, Holili, Horohoro, Namanga, Sumbawanga, Taveta na Tarakea.

(j) Kuendeleza utekelezaji wa Mfuko wa Stakabadhi za Mazao Ghalani.

(k) Kushirikiana na Sekta Binafsi katika kubuni na kutekeleza mikakati ya masoko ya ndani, kikanda na kimataifa.

(l) Kuendeleza na kuboresha mfumo wa ukusanyaji, uhifadhi, uchambuzi na usambazaji wa taarifa za masoko.

(m) Kuboresha mazingira ya kufanya biashara kwa kutekeleza Sheria ya Usajili wa Shughuli za Biashara (BRELA).

54. Utekelezaji kamili wa malengo ya sehemu hizi nne za viwanda, biashara, Kilimo Kwanza na masoko unahitaji upatikanaji wa mitaji kwa wawekezaji na huduma za maji na umeme zisizo katikakatika mara kwa mara. Serikali itatakiwa kukabiliana na changamoto hizo kwa kasi na viwango stahiki.

**MADINI**

55. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita ya 2005-2010, Chama Cha Mapinduzi kiliielekeza Serikali kuchukua hatua zenye lengo la kuharakisha ukuaji wa mchango wa Sekta ya Madini kwenye uchumi wa Taifa.

Baadhi ya mafanikio ambayo yamepatikana kutokana na hatua hizo ni haya yafuatayo:-

(a) Kukamilika kwa Sera ya Madini ya Mwaka 2009 na kupitishwa kwa Sheria ya Madini ya Mwaka 2010.

(b) Kuanzishwa kwa Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania.

(c) Kukamilisha ramani mpya za kisasa za Kijiolojia zinazoonyesha uwepo wa madini Tanga, Nachingwea na Liganga.

(d) Kutengwa kwa maeneo ya wachimbaji wadogo katika maeneo ya Kilindi, Winzo, Mvomero, Melela, Rwamgaza, Nyarugusu, Maganzo na Merelani.

(e) Mapato ya Serikali kutokana na uchimbaji mkubwa yameongezeka kutoka Sh. 457.4 bilioni mwaka 2005 hadi Shilingi 840.0 bilioni mwaka 2008.

(f) Thamani ya madini yanayouzwa nje imeongezeka kutoka dola za Marekani 727.45 milioni mwaka 2005 hadi dola 1,075.9 milioni mwaka 2008.

(g) Ajira katika uchimbaji mkubwa imeongezeka kutoka wafanyakazi 7,000 mpaka 13,000.

56. Katika kipindi cha Ilani hii ya 2010 – 2015, Chama Cha Mapinduzi kitaielekeza Serikali iendelee kukuza mchango wa sekta ya madini kwenye pato la Taifa kwa kuchukua hatua zifuatazo:-

(a) Kuendelea kuliimarisha Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) ili liweze kushiriki katika umiliki wa migodi mikubwa na ya kati na katika utoaji huduma katika sekta ya madini na litumike kuwaendeleza wachimbaji wadogo.

(b) Kuongeza mapato yatokanayo na sekta ya madini kwa kujenga uwezo wa Serikali katika usimamizi, uimarishaji wa miundombinu zikiwemo ofisi, vitendea kazi, kuongeza na kuwaendeleza wataalamu kwenye sekta ikiwa ni pamoja na kuimarisha wakala za Geological Survey of Tanzania (GST) na Wakala wa Ukaguzi wa Madini (TMAA).

(c) Kusimamia na kuhamasisha uwekezaji, utafutaji, uchimbaji na uongezaji thamani katika madini ili kukuza mchango wa sekta hiyo katika pato la Taifa.

(d) Kuwaendeleza wachimbaji wadogo katika utafutaji, uchimbaji, uchenjuaji na biashara ya madini, kuwarasimisha, kuwatafutia maeneo, kuwawezesha kupata mikopo na mitaji kwa kuanzisha mifuko maalumu, kuwapa mafunzo, teknolojia bora na maarifa. Aidha, katika kuhakikisha

wachimbaji wadogo wanachangia katika uchumi wa nchi yatawekwa mazingira mazuri ya kuwawezesha kuendesha shughuli za madini kwa usalama na kutunza mazingira.

(e) Kuendelea kuimarisha ukaguzi wa migodi katika masuala ya usalama, utunzaji wa mazingira na afya migodini.

(f) Kujenga uwezo wa utaalamu wa kushiriki kwa ukamilifu katika mikataba yote ya madini kwa lengo la kulinda maslahi ya nchi.

(g) Kuandaa soko bora la ndani la kuuzia madini lililowazi ili madini yetu yasiuzwe kilanguzi nje ya nchi.

(h) Serikali kuwa na hisa katika uchimbaji mkubwa wa madini.

(i) Kuandaa mkakati wa uchimbaji wa madini ya "uranium" tuliyonayo ili yachangie katika modenaizesheni ya uchumi.

(j) Serikali ihakikishe kwamba migodi yote mikubwa inapata huduma zake kutoka hapa hapa nchini kama vile vyakula, ulinzi n.k.

(k) Kuongeza uwezo wa kitaalamu kwa Watanzania wanaojishughulisha katika Sekta ya Madini.

## SURA YA NNE

## SEKTA YA MIUNDOMBINU NA HUDUMA ZA KIUCHUMI

### ARDHI

57. Chama Cha Mapinduzi na Serikali zake kinatambua kwamba ardhi ndiyo rasilimali namba moja katika modenaizesheni ya uchumi wa nchi yetu. Aidha, ardhi wanayomiliki wananchi katika familia zao au mtu mmoja mmoja ni mtaji wao wa kutegemewa siyo tu kwa kuwapatia ajira ya kudumu kupitia kilimo bali pia kupitia ardhi wanaweza kuitumia kama dhamana kupata mikopo katika vyombo vya fedha. Kwa kuwa ardhi huwa haiongezeki lakini matumizi na watumiaji wanaongezeka kila siku, ili kuondoa migogoro baina ya watumiaji wa ardhi, upo umuhimu wa ardhi yetu yote ipimwe, ipangiwe mipango ya matumizi bora, na imilikishwe kwa wananchi.

58. Katika kipindi cha miaka ya 2005-2010, Chama Cha Mapinduzi kiliielekeza Serikali kupitia Ilani yake kuanza utekelezaji wa Mkakati wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania (MKURABITA), kwa lengo la kutambua rasmi rasilimali za

wanyonge ambazo bado ziko kwenye sekta isiyo rasmi ili zitumike kuwawezesha kuwa washiriki kwenye uchumi rasmi wa Taifa. Vile vile kutambua na kupima mipaka ya vijiji na kuvipatia Hati za Vijiji (Village Land Certificates), kurahisisha upatikanaji wa hatimiliki za ardhi kwa wananchi, kupima na kutayarisha ramani za msingi za nchi yetu kwa ajili ya kupanga mipango ya maendeleo.

59. Katika kipindi cha Ilani hii ya miaka ya 2010-2015, Chama kinazitaka Serikali kulinda na kuendeleza kwa ari na nguvu zaidi mafanikio ambayo yamepatikana kwa kuchukua hatua zifuatazo:-

(a) Kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya na Miji, kukamilisha kazi ya upimaji wa mipaka ya vijiji vipya na kupanga mpango wa matumizi bora ya ardhi. Vile vile kuwahamasisha wananchi kuchangia upimaji wa mashamba yao na kuwapatia hatimiliki za kimila, pamoja na kujenga masjala za ardhi katika ngazi za Wilaya na Vijiji.

(b) Kutekeleza Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi wenye program 12 ambazo ni programu ya kuimarisha TUME, Kilimo, Mifugo, Uvuvi, Misitu, Wanyamapori, Madini, Nishati, Miundombinu, Rasilimali maji, Utalii na Uwanda/Uoto Asili kwa lengo la kukamilisha kazi ya upangaji wa matumizi bora ya ardhi nchini.

(c) Kuandaa utaratibu wa kuwawezesha wananchi wasio na ardhi kupatiwa ardhi katika maeneo mengine ya nchi.

(d) Kusajili Hatimiliki na Nyaraka za Kisheria 300,000 na kuifanyia marekebisho Sheria ya Usajili wa Hati, Sura ya 334 ili kuboresha kazi ya usajili wa Hati na Nyaraka mbali mbali.

(e) Kuimarisha Ofisi ya Ardhi ya Kanda ya Kusini katika Mji wa Mtwara na kuanzisha Kanda mpya ya Magharibi itakayokuwa Mjini Tabora na Kanda ya Dar es Salaam.

(f) Kuziwezesha Halmashauri za Miji na Wilaya zote nchini kuweka na kuutumia mfumo wa kutumia teknolojia ya kompyuta katika kutoa huduma za ardhi kwa kuimarisha na kuboresha utunzaji wa kumbukumbu za upimaji ardhi, na kuzibadilisha kutoka mfumo uliopo sasa kuwa wa kielektroniki.

(g) Kwa kushirikiana na Halmashauri za Miji na Wilaya kutambua ardhi kwa ajili ya kuanzisha Hazina ya Ardhi (Land Bank) kwa ajili ya wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

(h) Kuzijengea uwezo Halmashauri za Miji na Wilaya ziweze kupima viwanja vingi na kuuza kwa wanaohitaji kwa kutumia mfuko wa mzunguko (Plot Development Revolving Fund).

(i) Kutoa elimu kwa umma juu ya Sheria za Ardhi, Sheria ya Mipangomiji, Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi na sheria zingine zinazohusiana na utawala wa ardhi.

(j) Kuzijengea uwezo Halmashauri za Wilaya, Miji na Majiji kuajiri wataalamu wa kutosha wa sekta ya ardhi na kununua zana za kisasa za kupima ardhi na usanifu wa ramani.

(k) Kuboresha utendaji kazi wa Mabaraza ya Wilaya ya Ardhi na Nyumba 39 yaliyopo na kuanzisha Mabaraza mapya 50 (wastani wa mabaraza 10 kwa kila mwaka) kwenye wilaya zenye migogoro mingi ya ardhi na nyumba.

60. Pamoja na Serikali kutekeleza majukumu ya jumla yaliyoelezwa hapo juu kuhusu ardhi, Chama Cha Mapinduzi kitaitaka Serikali kutekeleza mambo yafuatayo katika maeneo maalumu:-

(a) **Nyumba**

(i) Kushirikisha Wakala wa Taifa wa Utafiti wa Nyumba Bora na Vifaa vya Ujenzi (NHBRA) katika kufanya tafiti mbali mbali za vifaa vya ujenzi wa nyumba bora kwa teknolojia rahisi na gharama nafuu na kufikisha matokeo ya utafiti huo kwa wananchi.

(ii) Kuzielekeza Serikali za Mitaa kuratibu na kusimamia upatikanaji wa ardhi na uendelezaji wa miundombinu ili kuwezesha makampuni ya uendelezaji milki na watu binafsi kujenga nyumba na uendelezaji wa miji kwa namna bora na endelevu.

(iii) Kuhakikisha kwamba ujenzi wa nyumba na majengo yanayotumiwa na umma unazingatia mahitaji maalumu hususan ya watu wenye ulemavu.

(iv) Kuhakikisha kuwa jumla ya nyumba 15,000 (kwa wastani nyumba 3,000 kila mwaka) zinajengwa na Shirika la Taifa la Nyumba (NHC) kwa kushirikiana na sekta binafsi.

(v) Kuhimiza uanzishwaji wa vyama vya ushirika wa nyumba, na pia vikosi vya ujenzi wa nyumba bora na za gharama nafuu katika

ngazi za Wilaya na Kata; ili kuwezesha wananchi wa kipato cha chini kufaidika na mikopo ya nyumba.

(vi) Kuboresha mazingira ya upatikanaji wa mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba kwa masharti nafuu, kuwahamasisha wananchi kuzielewa Sheria ili wazitumie kupata mikopo ya muda mrefu kwa ajili ya kujenga au kununua nyumba na kuhamasisha mabenki na vyombo vingine vya fedha kutoa mikopo ya ujenzi wa nyumba ya muda mrefu na yenye riba nafuu.

(vii) Kubadili Mfuko wa Mikopo ya Nyumba kwa watumishi wa Serikali kuwa Mfuko wa Dhamana ya Mikopo ya nyumba kwa madhumuni ya kuwafikia watumishi wote wa umma.

(viii) Kulielekeza Shirika la Nyumba la Taifa kuwa mwendelezaji ardhi mkubwa (Master Estate Developer) na kujenga nyumba nyingi kwa ajili ya kuuza au kupangisha kwa wananchi wote na hasa watu wa kipato cha kati na cha chini.

(ix) Kutunga sheria itakayowataka wote wanaojenga nyumba bora na majengo mbalimbali mijini na vijijini kujenga miundombinu ya kuvuna na kutumia maji ya mvua.

(x) Kukamilisha utungaji wa Sera ya Taifa ya Nyumba (Housing Policy).

(xi) Kuandaa mpango wa kampeni ya kitaifa katika kila wilaya kuhakikisha kuwa wananchi wanajijengea nyumba bora.

(xii) Kuweka mazingira yatakayowezesha ujenzi wa nyumba wa gharama nafuu.

(b) **Mipango Miji**

(i) Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa programu ya Taifa ya Kurasimisha Makaazi nchini. Programu hii itakuwa dira ya kuboresha makaazi na kukabiliana na tatizo la ujenzi holela nchini. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine itaendeleza kasi ya Urasimishaji wa ardhi na nyumba katika Majiji na Hamashauri za Miji na Wilaya na kutoa leseni za makazi.

(ii) Kukasimu kazi za uidhinishaji wa ramani za mipango miji, ramani za upimaji ardhi na taarifa za uthamini wa ardhi katika ngazi za Kanda, Mikoa na Wilaya ili kazi zote hizo zifanyike katika ngazi za chini bila urasimu wowote.

(iii) Kuanzisha miji midogo pembezoni mwa miji mikubwa ili kupunguza msongamano katikati ya miji yote mikubwa tukianzia na Jiji la Dar es Salaam (Satellite Towns).

(iv) Kuanzisha mji wa kisasa wa Kigamboni (Kigamboni New City).

(v) Kushirikiana na Halmashauri za miji na majiji kutekeleza mpango wa kuboresha makazi yaliyojengwa kiholela (Slum Improvement Programmes).

(c) **Upimaji na Ramani**

(i) Kutekeleza mradi kabambe wa kuweka kituo cha kupokea picha za Satellite (Satellite Imagery Receiving Station) kitakachorahisisha upimaji wa ardhi yote nchini na pia kitarahisisha utayarishaji wa ramani kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

(ii) Kukamilisha Sera ya Taifa ya Upimaji na Ramani, kutayarisha Sheria ya Upimaji na Ramani, na kuanzisha Mfuko wa kulipa Fidia ya Ardhi nchini.

(iii) Kukamilisha upimaji na uwekaji wa alama 600 za mtandao wa upimaji nchini, ambazo zitakuwa na wastani wa umbali wa kilomita 30 kati ya alama moja na nyingine kwa maeneo ya vijijini na kilomita 10 kwa maeneo ya Mijini ili kupunguza gharama za upimaji ardhi nchini.

(iv) Kuanza kupima na kutayarisha ramani katika maeneo ya majini (baharini na katika maziwa) kwa kushirikiana na mashirika ya kimataifa ya Haidrografia.

(v) Kwa kushirikiana na nchi tunazopakana, kuimarisha alama za mipaka, na pia kulitafutia ufumbuzi tatizo la mpaka baina yetu na nchi ya Malawi katika Ziwa Nyasa.

**NISHATI**

61. Ujenzi wa msingi wa uchumi wa kisasa wa Taifa linalojitegemea unaotumia kwa wingi sayansi na teknolojia katika shughuli za uzalishaji mali na utoaji huduma,

unahitaji huduma za umeme na maji zinazotolewa kwa uhakika. Hivi sasa asilimia 90 ya nishati tunayotumia nchini inatokana na tungamotaka (biomass) wakati mafuta ya petroli na umeme hutupatia asilimia 10 tu ya mahitaji yetu. Upatikanaji huu wa nishati siyo muafaka kwa Mapinduzi ya viwanda tunayoyahitaji.

62. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Serikali chini ya uongozi wa Chama Cha Mapinduzi imeshughulikia maendeleo ya sekta ya nishati na kupata mafanikio makubwa yakiwemo yafuatayo:-

(a) Kukamilika kwa ujenzi wa mradi wa Songo Songo na kuanza kutumia gesi asilia katika kuzalisha umeme.

(b) Mikoa ya Mtwara na Lindi kupata umeme wa uhakika unaozalishwa kwa gesi asilia ya Mnazi Bay.

(c) Kuongezeka kwa uzalishaji umeme nchini kutoka kwenye miradi ya Kihansi MW 180, Songas MW 180, Ubungo MW 100 na Tegeta MW 45.

(d) Kukamilika kwa miradi ya upelekaji umeme katika Makao Makuu ya Wilaya za Serengeti, Ludewa, Mbinga, Simanjiro, Kilolo, Bahi na Mkinga.

(e) Kukamilika kwa Sheria ya Nishati Vijijini na kuanzishwa kwa Wakala na Mfuko wa Nishati Vijijini.

(f) Kuweka mfumo wa mikopo ya muda mrefu kwa waendelezaji wadogo wa nishati vijijini.

63. Katika miaka mitano ya utekelezaji wa Ilani ya 2010 – 2015, Chama kitaitaka Serikali kuongeza kwa kiwango kikubwa uzalishaji wa nishati ya umeme kutoka MW 1051 hadi MW 1722 (sawa na ongezeko la MW 671) na kupunguza ile ya tungamotaka kwa kuchukua hatua zifuatazo:-

(a) Kuboresha sera, sheria na kanuni zinazoongoza sekta ya nishati nchini.

(b) Kuunganisha gridi ya Tanzania na gridi za nchi jirani ili kuimarisha upatikaji wa umeme nchini.

(c) Kukamilisha upelekaji wa umeme kwenye Mikoa na Wilaya ambako gridi ya Taifa haijafika. Aidha, mkakati kabambe wa kupeleka umeme vijijini utaandaliwa na kutekelezwa kwa kumshirikisha Wakala wa Nishati Vijijini (REA).

(d) Kuimarisha mfuko wa nishati vijijini kwa kubuni vyanzo vya ziada vya kuchangia mfuko huu.

(e) Kuandaa na kutekeleza mpango utakaoipunguzia TANESCO baadhi ya majukumu na kuishirikisha sekta binafsi katika kuongeza na kuimarisha uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa nishati ya umeme nchini. Uzalishaji wa umeme kwa kutumia rasilimaji za maji zilizopo utaendelea kuwa moja ya majukumu ya TANESCO.

(e) Kuendeleza na kupanua uzalishaji, usambazaji na matumizi ya gesi asilia; na

(f) Kuendeleza utafutaji wa mafuta na gesi asilia nchini.

(g) Kujenga mradi wa umeme wa Kinyerezi wenye uwezo wa MW 240.

(h) Kuendeleza mradi wa umeme wa Kiwira (MW 200) na Mchuchuma (MW 240), Ngaka (MW 200) vitakavyozalisha umeme unaotokana na makaa ya mawe.

(i) Kuanza utekelezaji wa mradi wa kuzalisha umeme (358MW) kwa kutumia maji katika bonde la mto Ruhuji.

(j) Kuzalisha umeme (300MW) kutokana na gesi asili ya Mnazi Bay.

(k) Kupanua mitambo ya kusafisha gesi na bomba la kusafirisha gesi kutoka Songo Songo hadi Dar es Salaam.

(l) Kutekeleza mradi wa usambazaji wa gesi asili Dar es Salaam kukidhi mahitaji ya sekta mbalimbali.

(m) Kufanya tathmini na kujenga mfumo wa kusambaza gesi asilia nchini.

(n) Kuanza mchakato utakaowezesha utekelezaji wa mradi wa kufua umeme kwenye vyanzo vya maji katika maporomoko ya Stiegler’s Gorge, Ruhuji, Rumakali, Mpango, Nsovwe na Ruvuma.

(o) Kujenga kiwanda cha kusafisha mafuta na bomba la kusafirisha mafuta kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza (1200 km).

(p) Kuongeza kasi ya uunganishwaji umeme kupitia mifumo nje ya gridi kwa kuhamisha matumizi ya nishati jadidifu kama umeme wa jua, upepo na tungamotaka kupitia mradi wa TEDAP.

(q) Kuandaa programu ya kupunguza matumizi ya umeme hususan viwandani na majumbani.

(r) Kufufua na kupanua mitambo ya TPDC ya kusafishia mafuta na kuhakikisha kwamba mitambo hiyo inafanya kazi wakati wote.

(s) Kuwa na mpango wa kuhimiza matumizi ya nishati mbadala ya jua, upepo na fungamotaka (biogas).

(t) Kuanza utekelezaji wa njia Kuu ya Umeme ya Zambia, Tanzania na Kenya (ZTK) inayounganisha mitandao ya Umeme ya nchi za Mashariki ya Afrika na nchi za Kusini.

(u) Kukamilisha utekelezaji wa mradi wa KV 132 wa Makambako-Songea utakaofikisha umeme wa gridi wilaya za Songea, Namtumbo, Mbinga, Nyasa na Ludewa.

(v) Kuongeza ushiriki wa sekta binafsi ili iwekeze katika uzalishaji wa nishati mbadala kutokana na jua, upepo, biogas na vyanzo vingine kwa kiwango kikubwa na kuongeza uwezo wa usambazaji kwa gharama nafuu zaidi kwa njia ya ubia wa sekta ya Umeme na Sekta binafsi (PPP).

(w) Kuongeza uwezo wa gridi ya Taifa toka MW 240 hadi MW 400.

## MIUNDOMBINU

### Barabara

64. Katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani ya miaka ya 2010 – 2015, Chama kitaielekeza Serikali kuyalinda na kuyaendeleza mafanikio kwa kuchukua hatua zifuatazo:-

(a) **Kuimarisha Mfuko wa Barabara (Tanzania Road Fund)**

Kuendelea kuimarisha Mfuko wa Barabara kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kubuni na kupanua wigo wa vyanzo vya mfuko wa barabara ili kuongeza kiwango cha Mfuko.

(ii) Kuandaa mkakati endelevu wa kukarabati barabara na madaraja nchini ili kuinua uhai wa miundombinu hiyo na kupunguza kwa kiwango

kikubwa gharama za kuzikarabati.

(b) Kutenga fedha za maendeleo ya barabara za miji ikiwemo Dar es Salaam, Arusha na Mwanza na kuangalia uwezekano wa kuunda chombo maalumu cha kusimamia na kuendeleza ujenzi wa barabara za mijini.

(c) **Kukamilisha ukarabati wa barabara zote ambao unaendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami ambao umekwisha anza katika Barabara Kuu na Barabara za Mikoa kama ifuatavyo:**

- Manyoni – Isuna (Km 54);
- Kagoma – Biharamulo – Lusahunga (Km 154);
- Ndundu – Somanga (Km 60);
- Sumbawanga – Matai – Kasanga (Km 112);
- Marangu – Tarakea – Rongai – Kamwanga (Km 98);
- Minjingu – Babati – Singida (Km 222);
- Korogwe – Handeni (Km 65);
- Mziha – Turiani – Magole (Km 84.6)
- Dumila – Kilosa (Km 63)
- Bariadi – Lamadi (Km 71.8);
- Mbeya – Chunya – Makongolosi (Km 115);
- Tanga – Horohoro (Km 65);
- Masasi – Mangaka (Km 54);
- Makofia – Msata (km 64);
- Mwandiga – Manyovu (km 60);
- Handeni – Mkata (km 54);
- Kisarawe – Maneromango (Km 54);
- Njombe – Makete (Km 109).
- Barabara ya Kilwa/DSM (km 12);
- Barabara ya Mandela (km 16);
- Msimba – Ikokoto – Mafinga (Km 219);
- Arusha – Namanga (Km 105);
- Chalinze – Segera – Tanga (Km 245); na
- Isaka – Lusahunga (km 242)
- Kwasadala-Masama (Km 12.2);
- KiboshoShine-Kwa Raphael-International School (Km 43);
- RauMadukani-Mawela-UruNjari (Km 12.5);
- KiruaNduoni-Marangu Mtoni (Km 31.5);
- Kahama Mjini (Km 5).

(d) **Kuanza Ujenzi mpya na ukarabati kwa Kiwango cha Lami Barabara Zifuatazo:**

- Bunda – Kisorya – Nansio  (Km 93);
- Tunduma – Sumbawanga (Km 230);
- Rujewa – Madibira – Mafinga (Km 151);
- Babati – Dodoma – Iringa (Km 523);
- Sumbawanga – Kanyani – Nyakanazi (Km 562);
- Nata – Fort Ikoma (Km 141);
- Nzega – Tabora (Km 116);
- Manyoni – Itigi – Tabora (Km 264);
- Ipole – Koga – Mpanda (Km 255);
- Makurunge – Saadani – Pangani - Tanga (Km 178);
- Matai – Kasesya (Km 65);
- Mangaka – Mtambaswala (Km 65);
- Mto wa Mbu – Loliondo – Mugumu – Nata – Makutano (Km 452);
- Kyaka – Bugene (km 59);
- Mbinga – Mbamba bay (Km 66);
- Tunduru – Namtumbo (Km 194);
- Kamwanga – Sanya Juu (Km 75);
- Tabora – Urambo (Km 90);
- Uvinza – Kidahwe (Km 77);
- Daraja la Malagarasi na barabara zake (Km 48);
- Uyovu – Bwanga – Biharamuro (Km 112);
- Kisesa –Usagara  (Km 17);
- Namtumbo – Songea (Km 70);
- Peramiho – Mbinga (Km 78);
- Kawawa Jct – Mwenge – Tegeta (Km 17);
- Segera – Same – Himo (km 261);
- Makambako – Songea (km 295);
- Mtwara – Masasi (km 200);
- Arusha – Moshi – Himo – Holili (km140);
- Arusha – Minjingu (km 104);
- Nyanguge – Musoma – Sirari (km 262); na
- Sanya Juu – Bomang'omba (Km 25).

(e) **Kuzifanyia Upembuzi na Usanifu Barabara Zifuatazo:-**

- Tabora – Mambali – Bukene – Itobo – Kahama (Km 149);
- Lupilo – Malinyi – Kilosa kwa Mpepo – Londo – Kitanda (km 396);
- Ifakara – Mahenge ( Km 67);
- Kibondo – Mabamba (km 35);
- Kolandoto- Lalago - Mwanhuzi -  Matala - Oldeani Jct (km 328);
- Omugakorongo – Kigarama – Murongo (km 105);
- Mpemba – Isongole (Tanzania/Malawi) (km 49);
- Soni – Bumbuli –Dindira – Korogwe (km 74);

- Makofia – Mlandizi – Vikumburu (Km 148);
- Kibaoni – Majimoto – Inyonga  Km 162);
- Mpanda- Ugala – Kaliua – Ulyankulu – Kahama (km 428);
- Makongolosi- Rungwa – Mkiwa (km 412);
- Mtwara – Newala – Masasi (km 209);
- Handeni – Kiberashi – Kondoa – Singida (Km 460);
- Kibaha – Mapinga (Km 23);
- Geita-Bukoli-Kahama  (Km 107);
- Mbande-Kongwa Jct – Mpwapwa   (Km 50).

.

**Vivuko**

65. Kuandaa utaratibu wa kununua vivuko vipya vyenye uwezo wa kubeba tani 50 kila kimoja kwa ajili ya maeneo yafuatayo:-

    (a) Msanga Mkuu (Mtwara),
    (b) Rusumo (Kagera),
    (c) Itungi Port – Matema (Kyera) na
    (d) Kilambo (Mtwara) kitakachotoa huduma kati ya Tanzania na Msumbiji.

66. **Madaraja**

    (a) Kuanza ujenzi wa daraja la mto Kilombero na daraja la mto Mwatisi katika mkoa wa Morogoro.

    (b) Kuanza ujenzi wa daraja la Malagarasi, Kigoma.

    (c) Kukamilisha maandalizi na kuanza ujenzi wa Daraja la Kigamboni ili kuunganisha Kigamboni na Jiji la Dar es Salaam.

    (d) Kuanza ujenzi wa daraja la Nangoo (Mtwara), Sibiti (Singida), Ruhekei (Mbinga) na Mbutu (Igunga).

    (e) Kuanza usanifu wa daraja la Ruhuhu (Ruvuma).

67. **Usafiri na Uchukuzi**

    (a) Kuendelea kuiimarisha Kampuni ya Reli Tanzania (TRL) kwa lengo la kuipa uwezo wa kutoa huduma bora kwa kusafirisha abiria na mizigo ya ndani na nchi jirani. Pia, reli itaendelezwa kama mhimili wa mpango wa maendeleo wa eneo la Ukanda wa kati.

(b) Kushirikiana na Serikali za Rwanda na Burundi, kuanza ujenzi wa reli mpya kutoka Dar es Salaam kwenda Kigali (Rwanda) na Msongati (Burundi).

(c) Kuimarisha Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) kwa kuboresha miundombinu ya reli na kuendeleza juhudi za kubadilisha mfumo wa uendeshaji wa shirika kwa lengo la kuboresha huduma za abiria na mizigo.

(d) Kujenga na kuimarisha miundombinu ya Reli na Bandari kwa kukamilisha mtandao wa reli na kuunganisha bandari ya Tanga na reli ya Arusha - Musoma:-

(i) Ujenzi wa bandari mpya eneo la Mwambani (Tanga),
(ii) kuboresha reli ya Tanga – Arusha,
(iii) kujenga reli mpya kati ya Arusha na Musoma,
(iv) Kuboresha bandari ya Musoma.

(e) Kuanza ujenzi wa reli ukanda wa Mtwara kwa kuchukua hatua za maandalizi ya mradi wa ujenzi wa reli ya Mtwara – Mchuchuma – Liganga.

(f) Kuendeleza huduma za uchukuzi kwenye maziwa kwa kuimarisha bandari za Kigoma, MbambaBay, Mwanza, Bukoba na Nansio.

(g) Kuboresha huduma za uchukuzi katika Bandari za Mwambao :

(i) Kupanua bandari ya Dar es Salaam na Mtwara
(ii) Kujenga bandari mpya Bagamoyo
(iii) Kujenga magati katika bandari za Mafia na Lindi.

(h) Kutekeleza Programu ya Uwekezaji Katika Sekta ya Uchukuzi kwa kuvutia wawekezaji binafsi katika uendeshaji wa sekta ya uchukuzi kwa kuzingatia Sera ya Sheria ya ushirikishaji wa sekta binafsi (PPP).

(i) Kuimarisha usafiri wa anga iIi uchangie kwenye pato la Taifa kwa kuchukua hatua zifuatazo:

(i) Kuimarisha na kuboresha kiwanja cha JNIA kwa kujenga jengo jipya la abiria na majengo mengine ya huduma za abiria.

(ii) Kukamilisha na kutekeleza Mpango Kabambe wa Usafiri wa Anga.

(iii) Kukamilisha ujenzi wa kiwanja kipya cha Kimataifa cha ndege cha Songwe (Mbeya)

(iv) Kuanza ujenzi wa kiwanja kipya cha Kimataifa cha ndege cha Msalato (Dodoma).

(v) Kufanyia upembuzi na usanifu kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Bagamoyo.

(vi) Kukamilisha uboreshaji wa viwanja vya ndege vya Mwanza na Mtwara.

(vii) Kukamilisha uboreshaji wa viwanja vya ndege vya Mafia, Arusha, Mpanda, Sumbawanga Bukoba, Kigoma, Tabora na Shinyanga.

(viii) Kuunda upya Shirika la Ndege la Taifa kwa kushirikisha sekta binafsi.

(j) Kupunguza Msongamano wa Magari katika Jiji la Dar es Salaam kwa kufanya yafuatayo:

(i) Kujenga barabara za juu (fly overs) kwenye makutano ya barabara maeneo ya Ubungo na TAZARA,

(ii) Kupanua mtandao wa barabara za Jiji za Dar es Salaam kwa kujenga na kukarabati barabara zifuatazo:-

- Mbezi (Morogoro road)-Malambamawili-Kinyerezi-Banana (Km 14.0);
- Tegeta Kibaoni-Wazo-Goba-Mbezi Mwisho (Km 20.0);
- Tangi Bovu-Goba (Km 9.0);
- Kimara Baruti-Msewe-Changanyikeni (Km 2.6);
- Kimara-Kilungule-External Mandela road (Km 9.0);
- Ubungo Bus Termanial-Mabibo-Kigogo Round about (Km 6.4);
- Kigogo Round About-Bonde la Msimbazi-Twiga/Msimbazi Junction (Km 2.7);
- Tabata Dampo-Kigogo- Ubungo Maziwa External (Km 2.25);
- Old Bagamoyo-Garden Road (Km 9.1); na
- Jet Corner-Vituka-Devis Corner (Km 6.0).

(iii) Kuanzisha mradi wa mabasi yaendayo kasi (DART).

**Kuimarisha uwezo wa Utabiri wa Hali ya Hewa**

68. Kuimarisha Uwezo wa Utabiri wa Hali ya Hewa Nchini kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kukamilisha na kutekeleza Sera ya Taifa ya Hali ya Hewa,

(ii) Kuiongezea uwezo Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo,

(iii) Kuendelea kutanua mtandao wa rada hadi kufikia rada saba nchi nzima,

(iv) Kuboresha miundomblnu ya kutoa utabiri na mawasiliano katika kituo kikuu cha Utabiri wa hali ya hewa, na

(v) Kuboresha mfumo wa kutoa taarifa za hali ya hewa mapema na kuhakikisha kuwa taarifa hizo zinafika kwa watumiaji mapema.

**Sayansi na Teknolojia**

69. Mapinduzi ya kilimo, ufugaji, uvuvi na viwanda ambayo Taifa linataka yafanyike ili tuweze kuleta modenaizesheni ya uchumi wetu, yatawezekana na kasi yake itakua kwa njia ya nchi kuwekeza vema katika ujenzi wa msingi imara wa maendeleo ya sayansi na teknolojia (building a solid scientific and technical base). Msingi imara wa sayansi na teknolojia katika uhandisi wa chuma na madawa (kemikali) utaiwezesha nchi kupanua haraka matumizi ya sayansi na teknolojia katika shughuli za uzalishaji mali na utoaji huduma katika sekta mbalimbali za uchumi wetu.

70. Katika kipindi hiki ambacho nchi imeamua kwa dhati kujenga uchumi wa kisasa na kuutokomeza umaskini, ni lazima sasa tulipatie kipaumbele cha kwanza suala la maendeleo na matumizi ya sayansi na teknolojia ili tuweze kuondokana na uchumi ulio nyuma na pia uchumi tegemezi.

71. Hivyo, katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani hii ya 2010-2015, Chama Cha Mapinduzi kitazielekeza Serikali kuweka msisitizo mkubwa katika suala la maendeleo na matumizi ya sayansi na teknolojia kwa kuchukua hatua zifuatazo:-

(a) Kutenga kila mwaka kiasi kisichopungua asilimia 1.0 ya pato ghafi la Taifa (GDP) kwa ajili ya Utafiti, Maendeleo na Maonyesho ya Matokeo ya Utafiti (R,D&D).

(b) Kuchukua hatua za makusudi za kuimarisha Tume ya Sayansi na Teknolojia ili kiwe chombo kinachowaunganisha watafiti na wagunduzi wote nchini ili waweze kukaa kubadilishana uzoefu na kuwa na msukumo wa pamoja katika ujenzi wa msingi wa sayansi na teknolojia tunaouhitaji.

(c) Kuishirikisha sekta binafsi katika kuchangia maendeleo na matumizi ya sayansi na teknolojia kwenye uzalishaji mali na utoaji wa huduma.

(d) Kuandaa programu mahusus ya wataalamu wa kada mbalimbali kama vile za uhandisi, uganga wa binadamu na wanyama, madini, jiolojia na kilimo n.k. watakaojaza nafasi ambazo ni muhimu na za lazima katika kuyafikia malengo hayo ya dira.

(e) Kufufua, kupanua na kuanzisha viwanda ili kukuza uzalishaji viwandani na kuongeza ajira ya wanasayansi.

(f) Kuimarisha shughuli za kuatamia teknolojia (technology incubation) kabla ya kuzipeleka sokoni.

(g) Kuandaa mazingira bora ya kusambaza teknolojia kwa watumiaji.

(h) Kutumia vyombo vya habari kutoa taarifa muhimu za sayansi, teknolojia na ubunifu katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini.

(i) Kuwatambua wagunduzi wetu na kuwapa rasmi hakimiliki za ugunduzi wao.

(j) Kuboresha kwa kiwango kikubwa mishahara, marupurupu na mafao ya watafiti na wagunduzi wetu.

**Sekta ya Fedha**

72. Sekta ya Fedha ndicho kipimo kinachoweza kuonesha viwango vya uchumi wa nchi vilivyofikiwa katika vigezo mbalimbali kama vile pato la Taifa, ukuaji wa uchumi, mfumko wa bei n.k. Maendeleo ya haraka katika nyanja hizo yanategemea uimara na uwezeshaji wa Sekta ya Fedha.

73. Katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani hii ya 2010 - 2015, Chama kitaielekeza Serikali kuimarisha Sekta ya Fedha kwa kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kuendelea kuwaelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa kuweka akiba na kutumia huduma za benki katika shughuli zao za kila siku za kifedha.

(b) Kuendelea kupanua huduma za benki ili kuwafikia wananchi wengi zaidi.

(c) Kuendelea kuwahamasisha wananchi ili waone umuhimu wa kujiunga na huduma za bima mbalimbali ili zitumike pamoja na mifuko ya hifadhi ya jamii katika kukuza uwekezaji katika uchumi.

(d) Kulipatia ufumbuzi wa kudumu suala la riba za mabenki ili kuondoa tofauti iliyopo baina ya riba za mikopo na riba za amana na kuhakikisha kwamba mikopo ya muda mrefu ina riba ndogo.

## SURA YA TANO

## SERA YA UWEZESHAJI WA WANANCHI KIUCHUMI

74. Sera yetu ya Msingi ni kwamba wananchi wenyewe wamiliki na kuendesha uchumi wa nchi yao. Lakini ili wananchi wa Tanzania waweze kumiliki uchumi lazima wawe na maarifa ya kisasa. Watanzania walio wengi wanapungukiwa na maarifa ya uchumi wa kisasa, hawana mitaji na mazingira ya jamii yenye vikwazo

vingi vinavyowafanya washindwe kushiriki katika uchumi wao. Ndio maana ukabuniwa mkakati wa kuwawezesha wananchi kiuchumi ili nao waweze kushiriki katika uendeshaji wa uchumi wa kisasa.

75. Kwa kutambua kwamba kila raia wa Tanzania anayo fursa ya kumiliki ardhi na kuendesha shughuli za maendeleo pale anapoishi, Chama Cha Mapinduzi kinaendelea kutoa wito kwa wananchi kwamba sera ya uwezeshaji itafanikiwa tu katika maisha yao kama kila mwenye uwezo wa kufanya kazi atatekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Kutambua kwa dhati kwamba uwezo wa kufanya kazi alio nao mwananchi ni nguvu na mtaji wake namba moja katika kujiletea maendeleo yake pale alipo. Mtaji huu utumike kama sharti la kujikwamua na umaskini.

(b) Kutambua kwamba ardhi, cherehani, mgahawa, duka, mashine ya kufyatulia matofali anayomiliki n.k. ni msingi imara wa maendeleo yake na kwamba uwezeshaji ni njia ya kumuunga mkono. Kila mwananchi mwenye shughuli halali ya kufanya azame katika kujiletea maendeleo kwa kuendeleza shughuli hiyo.

(c) Kukubali kwamba kufanya kazi kwa bidii na kwa maarifa, pamoja na kutumia kwa busara mapato yatokanayo na kazi, ni msingi bora wa kuishi kwa kujitegemea. Kazi ni uhai na pia ni chimbuko la mali au utajiri ambao mwananchi anauhitaji.

(d) Wananchi ambao wanajishughulisha na kilimo na ufugaji wanatakiwa kulima kila zao kwa kuzingatia kanuni bora za kilimo ili wapate mavuno mengi kwa kila eneo wanalolima. Aidha, anayefuga ng'ombe, mbuzi, kondoo na kuku anatakiwa kufanya hivyo kwa kuzingatia kanuni bora za ufugaji ili aweze kupata faida kubwa hata kabla ya kupanua shughuli zake.

76. Katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani hii ya 2010-2015, Chama kitaielekeza Serikali kuendelea kutekeleza sera ya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi kwa kuchukua hatua zifuatazo:-

(a) Kufufua kwa nguvu zote elimu yenye manufaa ya watu wazima nchini kote ili masomo ya ujasiriamali, uwezeshaji, urasimishaji wa biashara, kilimo, ufugaji na uvuvi yaweze kutolewa kwa wananchi wengi. Maandalizi kamili yafanyike ili elimu itakayotolewa iweze kuziingiza kwenye mfumo rasmi rasilimali na biashara za wanyonge ambazo bado ziko nje ya mfumo huo. Mafunzo hayo yalenge katika kuutokomeza umaskini wa wananchi walio wengi.

(b) Kuhamasisha uanzishwaji wa ushirika wa kuweka na kukopa (SACCOS na VICOBA), wa mazao, ujenzi, uvuvi, biashara na aina nyingine za ushirika ili wananchi wengi zaidi wajiunge na ushirika na wawezeshwe kimtaji kupanua shughuli zao za uzalishaji mali. Serikali izingatie kwa ukamilifu uzoefu ambao umepatikana katika eneo hili la ushirika na iandae wataalam wengi wa ushirika ambao wataajiriwa kuimarisha na kuboresha sekta ya ushirika nchini kote.

(c) Kuandaa mpango maalumu utakaowezesha utekelezaji makini wa Mkakati wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania (MKURABITA) kwa kuhakikisha kwamba upatikanaji wa hatimiliki za ardhi, leseni za biashara na mikopo ya kupanulia shughuli za wanyonge, unakuwa mwepesi ili shughuli za kuinua mapato ya wananchi na kupambana na umaskini zisicheleweshwe wala kukwamishwa na taratibu za mikopo.

(d) Kukuza mifuko ya uwezeshaji, kuboresha usimamizi wake na taratibu za kutoa mikopo ya riba nafuu ili walengwa wengi zaidi waweze kunufaika nayo. Serikali iunde chombo cha wataalam makini na waaminifu watakaokabidhiwa jukumu la kusimamia na kuratibu shughuli hizo nchini kote ili ionekane wazi kwamba lengo la uwezeshaji kimitaji linazaa matunda yanayoboresha maisha ya wanyonge.

(e) Kuimarisha Benki ya Rasimali Tanzania (TIB) kwa kuongeza mtaji wake kwa kiwango kikubwa ili kuongeza nguvu ya uwekezaji katika kilimo.

(f) Kuhamasisha wananchi kutumia fursa zinazotokana na kupitishwa kwa sheria zifuatazo:-

(i) Sheria ya Mikopo na Karadha inayowawezesha wananchi kupata zana bora za kufanyia kazi.

(ii) Sheria ya Dhamana ya Mikopo ya Nyumba inayowawezesha wananchi kujenga nyumba bora, na

(iii) Sheria ya Umilikaji wa Sehemu ya Nyumba inayowawezesha wananchi kumiliki sehemu ya jengo kwa ajili ya makazi au shughuli mbalimbali.

## AJIRA NA UWEZESHAJI WA WANANCHI

77. Chama Cha Mapinduzi kinatambua kwamba katika kipindi hiki suala la ajira, na hasa ajira ya vijana, limekuwa nyeti. Hii ni kwa sababu idadi ya vijana wanaofuzu elimu ya msingi, sekondari, vyuo na vyuo vikuu kila mwaka ni kubwa

sana. Idadi hiyo inakuzwa pia na vijana wanaomaliza mafunzo ya JKT. Vijana hawa wote ni nguvu kazi ya Taifa ambayo inaweza kutumika katika kazi na shughuli halali za ujenzi wa nchi.

78. Ili kujenga fursa za ajira hasa kwa vijana, katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani ya 2010 – 2015, Chama kitaitaka Serikali ishughulikie mambo yafuatayo:-

(a) Kuimarisha na kupanua mafunzo ya vyuo vya maendeleo ya wananchi ili vipokee vijana wengi zaidi na kuwapatia mafunzo ya maarifa ya kisasa katika fani za kilimo, biashara, ufundi stadi na ujasiriamali.

(b) Kufanya utafiti wa kina wenye lengo la kuandaa mpango wa muda mrefu utakaowashirikisha vijana katika shughuli mbalimbali za kiuchumi ili kuwajengea uwezo wa kujitegemea.

(c) Kuimarisha Shirika la Tija la Taifa (NIP) ili kuongeza ufanisi na tija katika utekelezaji wa shughuli za uendeshaji wa uchumi nchini.

(d) Serikali kuibua Mpango Kabambe wa kuwawezesha kiuchumi vijana wasomi waliotayari kujituma kwa kujiajiri ili watumie nguvu na maarifa waliyonayo katika kilimo, ufugaji, uvuvi n.k. wa kisasa. Mpango huo utawawezesha vijana hao kwa:-

    (i) Kuwaandalia na kuwapa mafunzo ya ujasiriamali na yanayohusu shughuli wanazokusudia kuzifanya;

    (ii) Kuweka utaratibu mwepesi wa kupata mikopo nafuu;
    (iii) Serikali kutenga maeneo makubwa ya ardhi kwa ajili ya mpango wa aina hii kwenye maeneo yanayozunguka miji, majiji na kwingineko.

**Wafanyakazi**

79. Katika kipindi cha 2010-2015, CCM itaendelea kuwa karibu na wafanyakazi na kuhakikisha kuwa Serikali zinayatambua na kuyashughulikia kwa ukamilifu na kwa wakati muafaka matatizo yao. Miongoni mwa hatua zitakazochukuliwa na Serikali zitakuwa pamoja na hizi zifuatazo:-

(a) Kuendelea kuboresha mishahara ya wafanyakazi kwa kadri hali ya uchumi wa nchi utakavyoruhusu.

(b) Kuimarisha na kufanya kaguzi za kazi, ikiwa ni pamoja na masuala ya afya na usalama mahali pa kazi.

(c) Kusuluhisha na kuamua kwa wakati migogoro yote ya kikazi na kuimarisha ushiriki na ushirikishwaji wa wafanyakazi mahali pa kazi.

(d) Kuhakikisha kwamba mishahara ya wataalamu wa ndani na nje wenye sifa na kazi zinazofanana wanalipwa mishahara inayolingana.

(e) Serikali kuanzisha mchakato utakaohakikisha kwamba pamoja na kuthamini mchango wa kila mfanyakazi na kufanya kazi katika taaluma zao na kuziheshimu ni muhimu ione tofauti kubwa iliyopo kati ya malipo ya wafanyakazi wa ngazi za juu na wale wa ngazi za chini.

**Vijana**

80. Chama Cha Mapinduzi kinatambua umuhimu wa vijana ambao ni kundi kubwa la nguvukazi. Changamoto zinazowakabili ni pamoja na ukosefu wa ajira, elimu na maarifa ya kisasa katika uzalishaji mali, biashara na ujasiriamali. Katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani hii Chama kitazihimiza Serikali zake kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kupanua mafunzo ya VETA yaweze kuchukua vijana wengi zaidi wanaofuzu elimu ya msingi ili waandaliwe kujiajiri wenyewe.

(b) Kuwahamasisha vijana kuanzisha miradi ya kiuchumi na kujiunga katika vikundi vya ushirika wa kuweka na kukopa (SACCOS) na VICOBA na kuziwezesha kimitaji.

(c) Kuwahamasisha vijana kujiunga na vituo vya ufundi stadi ili wapate stadi za kuwawezesha kujiajiri wenyewe.

(d) Kuimarisha usimamizi na matumizi ya fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake na Vijana katika Halmashauri zote ili uweze kuwanufaisha vijana wengi zaidi kupitia SACCOS zao.

(e) Kushirikiana na wadau wengine katika kuimarisha vyama vya vijana vya ushirika wa akiba na Mikopo (SACCOS) ili viweze kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa vijana. Umuhimu wa kulipa mikopo kwa wakati utasisitizwa.

(f) Kushirikiana na wadau wengine katika kufanya utafiti juu ya maeneo mengi ya ajira na kupanua wigo wa harakati za kiuchumi zinazozalisha ajira nyingi kama vile kilimo, ufugaji, uvuvi, biashara na viwanda vidogo vidogo ili kuongeza fursa za ajira kwa vijana.

(g) Kuandaa na kuboresha mikakati na mipango mbalimbali ya malezi na makuzi bora kwa vijana yakiwemo mafunzo ya uraia mwema, maadili mema na uzalendo kwa nchi yetu.

(h) Kutekeleza mipango endelevu ya kuwaandaa vijana wataalamu katika fani mbalimbali za maendeleo. Mkazo mkubwa wa maandalizi utawekwa kwenye ajira binafsi.

(i) Serikali kuandaa mafunzo maalum kwa vijana ya kupenda kufanya kazi na kuwa waadilifu ili waweze kuajirika.

(j) Serikali isimamie kikamilifu sheria ya ajira kwa wageni.

(ki) Kuhamasisha ushiriki wa vijana katika ngazi mbalimbali za maamuzi ikiwa ni pamoja na kukamilisha uanzishaji wa Baraza la Vijana.

**Hifadhi ya Jamii**

81. Ili kuimarisha na kuendeleza hifadhi ya jamii Chama Cha Mapinduzi katika kipindi cha utekelezaji wa ilani hii kitazielekeza Serikali zake kuchukua hatua zifuatazo:-

(a) Kufanya tathmini ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na kurekebisha viwango vya mafao vinayotoa ili visipishane mno.

(b) Kuanzisha na kuimarisha Mamlaka ya Udhibiti na Usimamizi wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii.

(c) Kuchukua hatua za makusudi za kupanua wigo wa kinga ya Hifadhi ya Jamii, ili Watanzania walio wengi waweze kufaidika na huduma za mifuko ya jamii.

(d) Kuelimisha jamii ya wafanyakazi na waajiri juu ya umuhimu wa Hifadhi ya Jamii kwa maendeleo ya wafanyakazi na ya nchi kwa ujumla.

(e) Kuendelea kutumia uwezo wa kifedha uliopo katika kila Shirika la Hifadhi ya Jamii, kwa kuwekeza katika miradi mbalimbali ya maendeleo ya nchi.

## SURA YA SITA

## SEKTA YA HUDUMA ZA JAMII

82. Sekta ya huduma za jamii inayojumuisha huduma za elimu, afya na maji ni muhimu sana katika maendeleo ya nchi maana ubora wake ni kielelezo cha maisha yenye neema yaliyofikiwa. Aidha, katika kila Taifa la kisasa, ustawi wa jamii una sura mbili zinazotegemeana za maendeleo ya vitu kwa upande mmoja na maendeleo ya watu kwa upande mwingine. Huduma za jamii ndiyo maendeleo ya watu wenyewe.

83. Katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani hii ya 2010 – 2015, Chama Cha Mapinduzi kitaitaka Serikali iyalinde mafanikio yaliyopatikana katika kila sekta na kuyaendeleza ili wananchi waendelee kufurahia matunda ya uhuru wa nchi yao.

**ELIMU:**

84. Serikali itachukua hatua za kuboresha, kuimarisha na hata kupanua elimu ya Awali hadi ya Chuo Kikuu na kuhakikisha kwamba elimu ya ngazi zote itakayotolewa nchini tangu sasa iwe ya ubora utakaowawezesha vijana wetu kuchukua nafasi zao stahiki katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na dunia kwa ujumla. Hivyo, lengo hilo litafikiwa kwa kuishirikisha sekta binafsi kwa ukamilifu katika kutekeleza yafuatayo:-

(a) **Elimu ya Awali**

(i) Kuhakikisha kwamba kila shule ya msingi ina darasa la Elimu ya Awali lenye madawati yanayolingana na hali ya watoto wa elimu hiyo.

(ii) Kujenga vyoo kwa ajili ya watoto wa Elimu ya Awali ili wasiingiliane na wale wa shule za msingi.

(iii) Kuandaa walimu wengi wa Elimu ya Awali na kuwapanga katika shule zinazohusika.

(b) **Elimu ya Msingi**

Kusimamia kwa ukamilifu utekekezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi awamu ya pili (MMEM II – 2007 – 2011) na kuandaa na kutekeleza awamu ya tatu (MMEM III):-

(i) Kununua na kusambaza vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika shule zote.

(ii) Kuimarisha Vituo vya Walimu (Teacher Resource Centres) katika Kanda na Halmashauri zote ili viweze kutoa mafunzo ya walimu kazini.

(iii) Kuimarisha utoaji wa mafunzo kwa walimu wa masomo ya Hisabati, Kiingereza na Sayansi.

(iv) Kuendelea kuweka msukumo katika uandikishaji wa watoto wote wa rika lengwa katika ngazi ya Elimu ya Msingi kufikia asilimia 100 mwaka 2015.

(v) Kuinua kiwango cha uandikishaji wa watoto wenye ulemavu na wenye mahitaji maalumu.

(vi) Kuendelea kuratibu na kusimamia upatikanaji wa maslahi ya walimu wa shule za msingi, sekondari, vyuo vya ualimu na kuyaboresha ili kuhakikisha kwamba mishahara itolewayo inazingatia hali halisi ya maisha na ya soko.

(vii) Kuendelea kuimarisha ukaguzi wa shule na kuhakikisha kuwa kila shule inakaguliwa angalau mara moja kwa mwaka na taarifa za ukaguzi kufanyiwa kazi.

(viii) Kuhakikisha kwamba kila shule ya msingi ina walimu, madawati, vitabu vya kiada kwa kila somo vya kutosha. Uwiano wa mwalimu mmoja kwa kila wanafunzi 60 ufanyiwe kazi.

(xv Serikali Kuu ihakikishe kwamba kila Manispaa au Halmashauri ya Wilaya inajenga vyoo vya kisasa na vya kutosha katika shule zote za msingi ambazo ziko chini yake. Sekta binafsi ishirikishwe katika utekelezaji wa mradi huu.

(x) Kuanzisha mradi kabambe wa ujenzi wa nyumba nyingi za walimu wa shule za msingi za vijijini kwa kuwashirikisha wadau wote. Utekelezaji uanzie katika Wilaya ambazo zina uhaba mkubwa wa nyumba za walimu.

(xi) Kuongeza idadi ya wanafunzi watakaochaguliwa kuendelea na elimu ya sekondari kufikia asilimia 100 ifikapo mwaka 2015.

(xii) Kuimarisha uwezo wa watendaji katika usimamizi na menejimenti ya programu za elimu katika ngazi zote.

(c) **Elimu ya Sekondari**

Kusimamia kwa ukamilifu utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari awamu ya pili (MMES II – 2010 - 2014), kuandaa na kutekeleza awamu ya tatu (MMES III):-

(i) Kuendelea kutekeleza azma ya kuwa na angalau shule moja ya kidato cha tano na sita kwa kila tarafa.

(ii) Kuongeza idadi ya wanafunzi wa kidato cha 4 kwenda kidato cha 5 kufikia asilimia 50 ya watoto wanaofaulu ifikapo mwaka 2015.

(iii) Kuendeleza na Kuimarisha mafanikio tuliyofikia katika ujenzi wa shule za sekondari kwa kuongeza idadi ya walimu, kununua vifaa vya maabara, vitabu, kuimarisha Maktaba na kukabiliana na jambo lolote litakalopunguza ufanisi wa kiwango cha elimu katika shule hizo.

(iv) Kuendelea kutekeleza mpango wa kujenga maabara ya Sayansi na ya Lugha katika kila Shule ya Sekondari ili kuboresha ufundishaji.

(v) Kuendelea kutekeleza Programu ya kufundishia na kujifunzia kwa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika Shule za Sekondari.

(vi) Kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa masomo ya Sayansi, Hisabati na Lugha na kuinua ufaulu wa masomo hayo.

(vii) Kuendelea na mpango wa ujenzi wa nyumba za walimu hasa sehemu za vijijini na maeneo magumu kufikika.

(viii) Kuendelea kusimamia na kuimarisha michezo shuleni.

(ix) Kupitia na kuimarisha mitaala ya elimu ya sekondari kulingana na mahitaji.

(x) Kusimamia ubora wa miundombinu ya shule za sekondari ili kuleta ufanisi katika utoaji wa elimu.

(xi) Kuimarisha uwezo wa watendaji katika usimamizi na menejimenti ya programu za elimu katika ngazi zote.

(xii) Kurudisha utaratibu wa kuzipelekea shule vitabu na vifaa ili kuhakikisha kwamba shule hazitofautiani katika upatikanaji na utumiaji wa vifaa hivyo.

(xiii) Kuimarisha na kuboresha kwa kiwango kikubwa shule za vijana wenye vipaji maalumu ili lengo la kuzianzisha liweze kufikiwa kama lilivyokusudiwa tangu mwanzo.

(xiv) Katika shule za sekondari, uwiano wa mwalimu mmoja kwa wanafunzi 45 uzingatiwe kama hatua ya kuinua ubora wa elimu hiyo.

(d) **Elimu ya Ualimu**

Kusimamia kwa ukamilifu utekelezaji wa Mkakati wa Maendeleo na Menejimenti ya Ualimu (Teacher Development Management Strategy - TDMS) katika utoaji wa mafunzo ya ualimu:-

(i) Kuanzisha mafunzo ya walimu wa shule za msingi watakaoandaliwa kufundisha masomo mawili tu ambayo kila mmoja anayamudu ili kuinua ubora wa elimu ya msingi.

(ii) Kuandaa na kuendeleza walimu wanaofundisha masomo ya Sayansi, Hisabati na Lugha katika Shule za Msingi na Sekondari.

(iii) Kuongeza udahili wa wanachuo katika mafunzo ya Ualimu tarajali ngazi ya Cheti na Stashahada.

(iv) Kutoa mafunzo kwa walimu kazini ili kuimarisha na kuendeleza mbinu za ufundishaji kwa walimu.

(v) Kutoa mafunzo ya TEKNOHAMA katika kufundishia na kujifunzia katika Vyuo vya Ualimu.

(vi) Kuendelea kusimamia na kuimarisha michezo katika vyuo vya ualimu.

(vii) Kuimarisha miundombinu ya vyuo vya ualimu ili kuleta ufanisi katika utoaji wa elimu.

(viii) Kuboresha maabara ya vyuo vya ualimu vyenye mchepuo wa sayansi na kuvipatia vifaa na kemikali zinazotakiwa kwa ajili ya mafunzo ya vitendo katika vyuo hivyo.

(ix) Kuandaa mitaala wa mafunzo yatakayojumuisha masomo ya mapinduzi ya kilimo, ufugaji, uvuvi na viwanda ili kupata wataalamu wa kufundisha masomo hayo. Uandishi wa vitabu vya masomo hayo yaende sambamba na maandalizi ya mtaala huo.

(x) Kuimarisha uwezo wa watendaji katika usimamizi na menejimenti ya programu za elimu katika ngazi zote.

(e) **Elimu ya Juu**

Kusimamia kwa ukamilifu utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Juu:-

(i) Kuboresha utaratibu wa utoaji na urejeshwaji wa mikopo kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu.

(ii) Kupanua wigo wa utoaji wa mikopo ili kila mwanafunzi aliye na sifa ya kuingia chuo kikuu apate mkopo.

(iii) Kukarabati, kupanua na kuimarisha miundombinu ya vyuo vikuu na vyuo vikuu vishiriki ili iweze kuhimili ongezeko kubwa la wanafunzi watakaomaliza elimu ya sekondari.

(iv) Kuongeza udahili wa wanafunzi kwenye vyuo vya elimu ya juu.

(v) Kuongeza idadi ya wanafunzi wa kike vyuo vikuu ili ifikie angalau asilimia 40 ya wanavyuo wanaodahiliwa kila mwaka.

(vi) Kuandaa wahadhiri wa kutosha na wenye sifa za kufundisha kwenye vyuo vya elimu ya juu.

(vii) Kuunganisha vyuo vikuu na taasisi za utafiti kwenye mtandao ili kuimarisha utafiti wa pamoja, kupanua elimu kiwango cha uzamili na uzamivu.

(viii) Kuratibu na kusimamia utoaji wa Elimu ya Juu iliyo bora na kufanyika kwa utafiti ili ziweze kutatua matatizo ya kijamii na kiuchumi.

(ix) Kuimarisha mazingira ya utoaji wa Elimu ya Juu na maslahi yanayoendana nayo ili wahadhiri wavutiwe kujiunga na kubaki katika vyuo vya Elimu ya Juu na Vyuo Vikuu.

(x) Kuimarisha utoaji wa Elimu ya Juu kwa njia ya Masafa na Elimu Mtandao.

(xi) Kuimarisha uwezo wa watendaji katika usimamizi na menejimenti ya programu za elimu katika ngazi zote.

(f) **Mafunzo ya Ufundi**

Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi:-

(i) Kuongeza kasi ya upanuzi wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi kwa kushirikisha sekta binafsi.

(ii) Kuanzisha vyuo vya Ufundi Stadi angalau kimoja kwa kila wilaya ifikapo mwaka 2015.

(iii) Kuendeleza mafunzo ya ufundi na kada za kati za fani mbalimbali.

(iv) Kuongeza idadi ya wahitimu wa vyuo vya ufundi stadi wenye sifa za kuendeleza progamu za elimu ya ufundi kuanzia ngazi ya ufundi sanifu hadi ngazi za juu.

(v) Kuendelea kuhamasisha wanafunzi wa kike kujiunga na Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi.

(vi) Kuimarisha miundombinu ya Vyuo vya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi.

(vii) Kuimarisha uwezo wa watendaji katika usimamizi na menejimenti ya programu za elimu katika ngazi zote.

(g) **Elimu ya Watu Wazima Yenye Manufaa**

(i) Kuandaa na kutekeleza mpango kabambe wa Elimu ya Watu Wazima Yenye Manufaa nchini kote.

(ii) Kuimarisha Mipango ya Elimu ya kujiendeleza ikiwa ni pamoja na Elimu Masafa na Ana kwa Ana.

(iii) Kuimarisha utoaji wa Elimu Nje ya Mfumo Rasmi kupitia Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Watoto Walioikosa (MEMKWA) kwa kushirikiana na wadau wengine.

(iv) Kuinua ubora wa utoaji elimu ya watu wazima kupitia Mpango wa Uwiano Kati ya Elimu ya Watu Wazima na Jamii (MUKEJA).

(v) Kuimarisha uwezo wa watendaji katika usimamizi na menejimenti ya programu za elimu katika ngazi zote.

**SEKTA YA AFYA**

85. Maendeleo ya Taifa letu yataletwa na wananchi wenye afya bora inayowawezesha kuzalisha mali na kutoa huduma mbalimbali. Katika miaka mitano ijayo, Serikali itatekeleza na Chama kutoa kipaumbele katika maeneo yaliyoainishwa katika MKUKUTA na Malengo ya Milenia kwa kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM), ambao unazingatia na kutoa kipaumbele katika maeneo yafuatayo:-

(i) Upatikanaji wa rasilimaliwatu wenye ujuzi na wa kutosha katika Sekta ya Afya,

(ii) Uwepo wa miundombinu ya huduma za afya na ustawi wa jamii kwa kukarabati na kujenga vituo vya kutolea huduma katika Afya na Ustawi wa Jamii hasa ngazi ya kijiji na kata,

(iii) Kuongeza upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitenganishi katika vituo vya kutolea huduma; na

(iv) Kuimarisha mfumo wa rufaa toka ngazi ya kijiji hadi Taifa.

(b) Kuimarisha usafiri wa wagonjwa, vifaa vya huduma za afya na ustawi wa jamii, njia za mawasiliano ya simu, "redio call na Internet", katika ngazi zote za utoaji wa huduma za afya na ustawi wa jamii, ili kuwezesha upatikanaji wa huduma za kawaida za dharura za rufaa, zilizo bora, pamoja na upatikanaji wa vifaa vya kuwawezesha watu wenye ulemavu kumudu maisha ya kila siku.

(c) Kuhakikisha vituo vyote vinapata dawa muhimu na vifaa vya teknolojia ya kisasa, ya kuchunguza na kutibu magonjwa ili kuboresha utoaji wa huduma za kinga, tiba na utengemao.

(d) Kuimarisha nyenzo, vifaa na Mfumo wa ufuatiliaji na ukaguzi wa Huduma za Afya na Ustawi wa Jamii, pamoja na upatikanaji wa Taarifa na takwimu za Uendeshaji ikiwemo ufanyaji tathmini na utafiti, wa huduma za Afya na Ustawi wa Jamii.

(e) Kuhakikisha kuwa, huduma za Bima ya Afya zinaboreshwa na kuungana na Mfumo wa Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) na Tiba kwa Kadi (TIKA), ili ziwafikie Wananchi na kuongeza asilimia za wanachama kutoka 7.7 hadi 30 ifikapo mwaka 2015.

(f) Kuendeleza jitihada za kujenga uwezo wa ndani wa kutoa huduma ya matibabu ili kupunguza idadi ya wagonjwa wanaopelekwa nje ya nchi kwa matibabu hususan kwa maradhi ya moyo, figo, mishipa ya fahamu na saratani.

(g) Kuboresha huduma za Ustawi wa Jamii, Serikali inatarajia kufanya yafuatayo:-

(i) Kutafsiri sheria 3 zifuatazo, Sheria ya Mtoto Na. 21 ya 2009, Sheria ya usafirishaji Haramu wa Binadamu ya 2009 na Sheria ya Wenye Ulemavu ya 2010.

(ii) Kutengeneza kanuni za utekelezaji wa sheria hizo.

(iii) Kuhuisha miongozo iliyopitwa na wakati ili kuendana na mabadiliko ya kiuchumi na kijamii.

(iv) Kufanya utambuzi wa watoto walio katika mazingira hatarishi katika wilaya 48 ambazo hazijafanya utambuzi.

(v) Kupeleka huduma za ustawi wa jamii kwenye Halmashauri.

(vi) Kutoa mafunzo kwa Maafisa Ustawi wa Jamii kwa ngazi za Shahada 30, Stashahada 20 na Udaktari 5.

(vii) Kununua magari kwa makazi ya wazee 10 na vyuo 4 vya ufundi kwa watu wenye ulemavu.

(viii) Kufufua vyuo 4 vya watu wenye ulemavu na kuvipatia rasilimali watu na fedha.

(ix) Kuboresha Chuo cha Walezi wa Kulelea Watoto mchana Kisangara na Ilonga ili kutoa Wataalamu ngazi ya Cheti na Diploma.

(x) Kujenga vyuo 2 vya Ustawi wa Jamii na Jengo la Ofisi ya Ustawi wa Jamii.

(xi) Kuanza ujenzi wa Chuo Kikuu kipya cha Udaktari pamoja na hospitali ya kufundishia katika eneo la Mloganzila, Dar es Salaam ambacho kitakuwa na kitivo cha matibabu ya moyo, saratani na mishipa ya fahamu. Aidha, katika Chuo Kikuu cha Dodoma kinajengwa Chuo kishiriki cha Udaktari.

(h) Kuimarisha huduma ya matibabu ya wazee nchini kwa kuwapatia vitambulisho na kuyatungia sheria matibabu yao ya bure ili waweze kutibiwa hivyo katika vituo vyote vya matibabu bila ya usumbufu wowote.

(i) Kuimarisha huduma za mama Wajawazito, Watoto Wachanga na Watoto walio chini ya umri wa miaka mitano, ili kuendelea kupunguza idadi ya vifo vyao kwa kutoa mafunzo ya huduma ya uzazi wa dharura na kuimarisha huduma za "EMOs" katika vituo vyote vya afya nchini.

(j) Kuwajengea uwezo na kuimarisha ujuzi wa watumishi wa Sekta ya Afya na Ustawi wa Jamii, katika ngazi zote za kutolea huduma.

(k) Kuvijengea uwezo vituo vinavyotoa huduma za afya na Ustawi wa Jamii nchini.

(l) Kuimarisha udhibiti wa magonjwa yanayoambukiza, yasiyoambukiza na yale yaliyosahaulika.

**Sekta ya Maji**

86. Kutokana na umuhimu wa Sekta ya Maji kwa maendeleo ya kiuchumi, kijamii na hifadhi ya mazingira Chama kitaielekeza Serikali kuendeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji na kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kufikia asilimia 65 vijijini na mijini asilimia 75 ifikapo mwaka 2015.

(b) Kuandaa na kutekeleza mipango shirikishi ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji katika mabonde yote tisa kwa kuimarisha uwezo wa Ofisi za Mabonde hayo na Maabara za Maji. Mabonde hayo ni ya Mto Pangani, Rufiji, Wami/Ruvu, Ruvuma na Bubu; Maziwa ya Victoria, Nyasa na Tanganyika na Bonde la Kati (Ziwa Eyasi na Manyara).

(c) Kuendelea kushirikisha kwa ukamilifu nguvu za wananchi katika hatua zote za kutoa huduma ya maji ikiwa ni pamoja na kupanga, kujenga, kuendesha na kumiliki miradi yenyewe kwa njia ya kueneza Kamati za Maji za Vijiji sambamba na kuimarisha mifuko ya maji.

(d) Kuimarisha ushiriki wa Tanzania katika matumizi na usimamizi wa maji shirikishi.

(e) Kuimarisha utunzaji wa vyanzo vya maji na kudhibiti uchafuzi wa mazingira.

(f) Kuendeleza utekelezaji wa ujenzi wa malambo na mabwawa mapya, kukarabati na kufufua malambo ya zamani ili maji mengi zaidi yaweze kupatikana kwa ajili ya matumizi ya wananchi na mifugo.

(g) Kutunga sheria itakayoiwezesha Serikali kuhakikisha kwamba upatikanaji wa maji unaongezeka nchini kwa njia ya kila shule, chuo, taasisi, wizara, hoteli, kiwanda, kata, vijiji na mtu binafsi atakayejenga nyumba ya kisasa mjini au kijijini anajenga miundombinu ya kuvuna na kutumia maji ya mvua.

(h) Kutekeleza mradi mkubwa wa kufikisha maji katika miji ya Igunga, Nzega hadi Tabora kutoka mkoa wa Shinyanga.

(i) Kuboresha huduma ya maji katika miji mikuu ya mikoa na wilaya kwa kukarabati na kujenga miundombinu ya maji safi na majitaka.

(j) Kuimarisha na au kuikarabati miradi ya kitaifa ya Wanging’ombe, Maswa, Mugango – Kiabakari, Handeni Trunk Main (HTM), Chalinze, Makonde na Kahama – Shinyanga ili iwe endelevu.

(k) Kuhakikisha kwamba kila mamlaka ya maji mjini inadhibiti upotevu wa maji katika eneo lake lote kwa kukagua na kukarabati mara kwa mara miundombinu ya maji ili huduma itolewe kwa gharama nafuu.

(l) Kujenga uwezo wa kuhudumia miradi ya maji vijijini kwa kutoa mafunzo ya wataalamu na mafundi wa maji.

## SURA YA SABA

## MAZINGATIO MAALUMU YA ILANI
## KUHUSU ZANZIBAR

### Utangulizi

87. Sura hii ya Ilani ya Uchaguzi wa CCM ya mwaka 2010-2015, inatafsiri na kuainisha maeneo muhimu ya sera za CCM kwa kuzingatia mazingira maalumu ya Zanzibar. Ushindi wa CCM katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 1995, 2000 na 2005 kwa upande wa Zanzibar, kimsingi ulitokana na ridhaa ya wananchi baada ya kuridhishwa na sera zake zenye kutekelezeka na kuweka mbele maslahi ya wananchi, Uhuru wa taifa letu, umoja na mshikamano wa kitaifa na kuongozwa na misingi ya usawa, uadilifu, uwazi, na uwajibikaji.

88. Katika kipindi cha mwaka 2005–2010, ambacho ni cha pili na cha mwisho kwa Awamu ya Sita ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, yapo mafanikio makubwa yaliyopatikana chini ya uongozi mahiri wa Mhe. Dk. Amani Abeid Karume, Rais wa Zanzibar na Makamu Mwenyekiti wa CCM Zanzibar.

89. Katika kutekeleza azma yake ya kuwaunganisha wananchi wa Zanzibar pamoja na sera zake za umoja, amani na mshikamano CCM imeendelea kuimarisha umoja na mshikamano miongoni mwa wananchi wote wa Zanzibar na Tanzania kwa jumla.

### MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA ILANI YA CCM YA UCHAGUZI MKUU WA MWAKA 2005-2010

90. Chini ya uongozi wa CCM na Rais Karume, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imetekeleza kwa mafanikio makubwa Mwelekeo wa Sera za CCM katika miaka ya 2000-2010, Dira ya Maendeleo ya Zanzibar (2020), Malengo ya Milenia na Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005-2010.

91. Katika kipindi hiki, Zanzibar imepiga hatua kubwa katika kuendeleza na kuimarisha huduma za kiuchumi na kijamii ikiwemo miundombinu ya barabara, bandari, viwanja vya ndege pamoja na huduma za jamii hususan elimu na afya. Baadhi ya mafanikio hayo yanajidhihirisha katika sekta zifuatazo:-

### Uchumi

92. Mafanikio yaliyofikiwa katika kukuza Uchumi ni kama yafuatayo:-

(a) Ukuaji wa pato la Taifa umeongezeka kutoka asilimia 4.9 mwaka 2004 na kufikia wastani wa asilimia 6.7 mwaka 2009.

(b) Kasi ya mfumko wa bei imeendelea kushuka kutoka asilimia 18.5 mwaka 2004 na kufikia asilimia 8.9 mwaka 2009.

(c) Pato kwa kila mwananchi limeongezeka kutoka kiwango cha Tshs. 325,000 mwaka 2004 na kufikia Tshs. 726,000 mwishoni mwa mwaka 2009.

(d) Nakisi katika mizania ya biashara nayo inaonesha kupungua kutoka kiwango cha 115,233.0 milioni mwaka 2004 na kufikia kiwango cha Tshs. 92,137.5 milioni mwaka 2009.

(e) Ukusanyaji wa mapato ya ndani kwenye Pato la Taifa nao umeongezeka kutoka asilimia 13.5 ya mwaka 2004/2005 na kufikia asilimia 18.5 mwaka 2009/2010.

**Sekta za Uzalishaji Mali**

**Mapinduzi ya Kilimo**

93. Mafanikio yaliyofikiwa katika Sekta ya Kilimo ni kama yafuatayo:-

(a) Kutekeleza miradi ya jamii inayohusu kilimo, mifugo na utunzaji rasilimali za baharini (ASSP/ASDP-L, PADEP na MACEMP).

(b) Kuanzisha Skuli za wakulima (mashamba darasa) ili kutoa mafunzo ya kilimo bora na ufugaji wa kisasa kwa wakulima. Jumla ya Skuli 186, zimeanzishwa kupitia mpango wa ASDP-L Unguja na Pemba.

(c) Kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji maji na kutoa mafunzo kwa wakulima. Jumla ya hekta 300, visima 6 na pampu 6 zimeimarishwa na kuwekwa katika mabonde ya Kibokwa, Bumbwisudi, Mchangani na Cheju.

(d) Kununua zana za kisasa za kilimo yakiwemo matrekta 27 na matrekta madogo "power tillers" 20.

(e) Kufufua kituo cha kuzalisha mbegu bora za nafaka – Bambi.

(f) Kufanya utafiti wa mbegu bora za mazao ya chakula na kufanikiwa kupata mbegu 3 za mpunga (NERICA) na 4 za muhogo (Machui, Kizimbani, Mahonda na Kama) zenye sifa na ubora unaohitajika.

(g) Kuimarisha vituo vya utafiti na mafunzo na kufanya ukarabati wa miundombinu ya utafiti zikiwemo maabara 2, visima 3 vya maji na ujenzi wa barabara za ndani katika Kituo cha Kizimbani.

(h) Kuanzisha ujenzi wa Kituo cha Mafunzo ya Usarifu wa Mazao ya wakulima huko Kizimbani.

(i) Kuendeleza udhibiti wa wadudu waharibifu wa mazao na kuandaa mpango madhubuti wa matumizi ya mbinu za uwiano (Intergrated Pest Management).

**Mapinduzi ya Ufugaji**

94. Mafanikio yaliyofikiwa katika Sekta ya Mifugo ni kama yafuatayo:-

(a) Kununua mtambo mpya wa **"Liquid Nitrogen"** ili kuendeleza kazi ya upandishaji ng'ombe kwa sindano na kupata mbegu bora ya ng'ombe wa maziwa.

(b) Kuwaendeleza wafugaji wadogo kwa kuwapatia ng'ombe wa maziwa kwa njia ya mkopo (kopa ng'ombe ulipe ng'ombe). Zaidi ya wafugaji 400 walifaidika na mpango huu kupitia Mfuko wa OPEC. Aidha, wafugaji 2,373 walipatiwa ng'ombe bora na wafugaji 3,666 walipatiwa mbuzi wa maziwa kwa kupitia mradi wa PADEP.

(c) Kuanzisha vituo vya Huduma za Ufugaji (Farm Service Centres) na kuendeleza huduma za kinga na tiba ya mifugo.

**Mapinduzi ya Uvuvi na Mazao ya Baharini**

95. Mafanikio yaliyofikiwa katika Sekta ya Uvuvi na Mazao ya Baharini ni kama yafuatayo:-

(a) Kuwaendeleza wavuvi wadogo wadogo kwa kuwapatia mafunzo ya kudhibiti uharibifu wa mazingira ya baharini na kuwapatia vifaa vya kisasa vya uvuvi zikiwemo boti na mashine, nyavu, mishipi, madema pamoja na majokofu ya kuhifadhia samaki.

(b) Kuanzisha na kutekeleza mradi wa MACEMP pamoja na kuendeleza maeneo ya hifadhi ya ukanda wa pwani ya Mnemba-Chwaka, Mkondo wa Pemba na kuongeza maeneo mapya ya Tumbatu, Bawe na Menai.

(c) Kuwaendeleza wakulima wa mwani kwa kuwapatia vifaa vya kulima mwani.

(d) Kukamilika kwa utafiti wa viumbe hai adimu vya baharini ulioainisha kuwepo kwa pomboo 136, aina ya Bottleneck na pomboo 63 aina ya Humback.

**Maliasili**

96. Mafanikio yaliyofikiwa katika Sekta ya Maliasili ni kama yafuatayo:-

(a) Kuwahamasisha wananchi ili kudhibiti matumizi mabaya ya rasilimali ikiwemo misitu na bahari pamoja na kusimamia ulinzi na utunzaji wa misitu katika maeneo yao.

(b) Kuwaelimisha wananchi juu ya sheria mbalimbali za maliasili na kuhamasisha upandaji miti na uhifadhi wa misitu.

(c) Kuendeleza utunzaji wa wanyama pori walio katika hatari ya kutoweka kama vile kima punju, popo wa Pemba na paa nunga na kuwatumia kama vivutio vya utalii. Idadi ya kima punju wa Jozani imeongezeka kutoka 2,500 hadi 5,000, kima punju wa msitu wa Masingini nao wameongezeka kutoka 500 hadi 21,700.

**Mazingira**

97. Mafanikio yaliyofikiwa katika Sekta ya Mazingira ni kama yafuatayo:-

(a) Kuendeleza kazi ya udhibiti wa uchafuzi wa mazingira katika maeneo ya kazi, viwanda na mahoteli.

(b) Kufanya mapitio ya miradi ya vitega uchumi na kutoa mapendekezo kwa wahusika. Jumla ya taarifa za miradi 107 zilifanyiwa mapitio na maeneo 485 ya miradi ya vitega yalifanyiwa ukaguzi.

**Utalii**

98. Mafanikio yaliyofikiwa katika Sekta ya Utalii ni kama yafuatayo:-

(a) Kutengeneza tovuti kwa lugha ya Kichina ili kuitangaza Zanzibar kwa wawekezaji kutoka Jamhuri ya Watu wa China.

(b) Kuziingiza hoteli ndogo hasa zinazomilikiwa na wananchi katika mtandao maalumu wa **"World Hotel Link"** ili kuziwezesha kuingia katika mashindano ya soko la kimataifa.

(c) Ushiriki wa Zanzibar katika maonyesho 40 ya Kimataifa katika kuitangaza kiutalii na kutoa matangazo katika jarida maalumu la **TANZANIA na UNESCO.**

(d) Kuchapisha jarida la **"The Ultimate Indian Ocean Experience"** kwa lugha za Kiingereza, Kihispania, Kifaransa na Kujerumani pamoja na Jarida la vivutio vya Utalii vya Zanzibar kwa lugha ya Kirusi na Kichina. Harakati hizo za utangazaji zimeiwezesha Zanzibar kutembelewa na watalii 670,231 katika kipindi cha mwaka 2005-2009.

(e) Kuingiza taswira ya Zanzibar katika tiketi za kampuni za boti ziendazo kasi za Azam Marine Ltd. na Farst Ferries Ltd.

(f) Kupitishwa kwa Sheria Namba 7 ya Mwaka 2008 ya Chuo cha Maendeleo ya Utalii na Sheria Namba 6 ya Mwaka 2009 ya Kamisheni ya Utalii.

(g) Kukamilisha tafiti 4 kubwa juu ya Sekta ya Utalii (Tanzania Tourism Sector Survey) zilizopelekea uwekaji wa viwango vya kutoza kodi kwa huduma za mahoteli.

(h) Kukamilisha Mpango wa Uendelezaji Utalii wa baharini na Sera ya Utalii wa Utamaduni pamoja na kufanyika kwa utafiti wa kuzitambua rasilimali za Utalii ambazo hazijatumika ipasavyo kwa lengo la kuongeza idadi ya siku kwa watalii na kuondokana na utalii wa msimu.

(i) Kujengwa kwa hoteli 11 za daraja la 5, 11 za daraja la 4 na 12 za daraja la 3 ambazo zimeanza kutoa huduma.

(j) Kuimarishwa kwa Mitaala ya Chuo cha Maendeleo ya Utalii hadi kufikia kiwango cha Diploma katika somo la "Tourism and Hospitality

Management" pamoja na kuhitimu kwa jumla ya wanafunzi 891 katika ngazi ya cheti na diploma.

(k) Kukamilisha ujenzi wa vituo viwili vya Polisi (Nungwi na Kiwengwa) kwa mashirikiano na wawekezaji katika Sekta ya Utalii na ununuzi wa vifaa vya mawasiliano (redio calls 10) ili kuimarisha ulinzi na usalama wa watalii na mali zao.

**Viwanda na Biashara**

99. Mafanikio yaliyofikiwa katika Sekta ya Viwanda na Biashara ni haya yafuatayo:-

(a) Kuandaa na kupitisha Sera ya Biashara na Sera ya uendelezaji wa biashara/viwanda vidogo vidogo na vya kati (SMEs) na kutafsiriwa katika lugha nyepesi.

(b) Kukamilisha Mpango Mkakati wa Usafirishaji wa Bidhaa na kuanza utekelezaji wake.

(c) Baraza la Biashara la Zanzibar lenye wajumbe kutoka sekta ya umma na sekta binafsi limeundwa na linafanyakazi zake.

(d) Kuwapatia mafunzo wajasiriamali 250 katika fani zifuatazo:-

(i) Uzalishaji na kuongeza thamani hasa kwa mazao ya Kilimo.

(ii) Elimu ya ujasiriamali

(iii) Usindikaji wa mazao ya Kilimo

(iv) Huduma za maendeleo ya biashara (BDS).

(v) Uzalishaji wa mafuta ya majani ya mikarafuu na utumiaji wa vinu vya uzalishaji.

(e) Kujenga vituo viwili vya majaribio vya kukaushia mazao ya kilimo/bahari Unguja na Pemba.

(f) Kununua vinu vinane vya kuzalisha mafuta ya majani ya mkarafuu na kuvigawa kwa wajasiriamali ambavyo vimetoa ajira kwa watu 2,052.

(g) Kuwapatia mafunzo wajasiriamali 60 katika fani zifuatazo:-

(i) Utengenezaji nguo
(ii) Ufugaji bora
(iii) Maandalizi ya Mpango wa Biashara
(iv) Utafutaji masoko
(v) Ubora wa bidhaa
(vi) Tathmini ya ujasiriamali ( SWAOC analysis).

(h) Kiwanda cha mafuta ya karafuu na makonyo kimefanikiwa kupeleka bidhaa zake katika soko la Marekani chini ya utaratibu wa AGOA.

(i) Kituo cha taarifa za biashara kimeendelezwa kwa kupatiwa vifaa na kuanzishwa kwa mtandao wa taarifa za biashara (database).

(j) Usafirishaji wa bidhaa umeongezeka kutoka T.Sh. 15.0 bilioni mwaka 2006 hadi kufikia T.Sh. 30.0 bilioni mwaka 2010 sawa na ongezeko la asillimia 100.

(k) Jumla ya tani 32,910 za karafuu zenye thamani ya US$ 99.16 milioni zimesafirishwa kwenda nje ya nchi.

(l) Jumla ya vikundi 159 vya wajasiriamali vilishiriki katika maonyesho tofauti yakiwemo ya Sabasaba, Juakali na Kilimo.

(m) Jumla ya viwanda vidogo vidogo na vya kati 10 (SMEs) vimeanzishwa au kufufuliwa vikiwemo vya maji, vyakula, nguo, mbao, ukamuaji wa mafuta na sukari na kutoa ajira kwa wafanyakazi wapatao 2,334.

(n) Jumla ya miradi ya Uwekezaji 192 yenye thamani ya dola 2.2 bilioni imeidhinishwa. Katika miradi hiyo ni Utalii (115), Biashara (17), Viwanda (15), Kilimo (6), Mawasiliano (11) na mingineyo 28.

(o) Miundombinu ya maji, umeme, na barabara imefikishwa katika maeneo huru ya uchumi ya Fumba na Uwanja wa Ndege ambapo Wawekezaji 1,010 wameweza kutumia huduma hizo.

(p) Muundo wa Mamlaka ya Uwekezaji umekamilishwa ili kukidhi masharti ya Sera na Sheria ya Uwekezaji.

**Vyama vya Ushirika**

100. Kusajili SACCOS 313 na vyama vya Ushirika wa uzalishaji 544 pamoja na kutoa mafunzo ya uendeshaji kwa wanachama 13,790.

**MIUNDOMBINU YA KIUCHUMI**

**Barabara**

101. Mafanikio yaliyofikiwa katika Sekta ya Miundombinu ya barabara ni haya yafuatayo:-

(a) Mtandao wenye urefu wa kilomita 136.10 za barabara kwa Unguja na Pemba umekamilika ambazo ni:-

- Mazizini - Fumba Km 18.0
- Tunguu - Kinyasini Km 26.8
- Paje - Makunduchi Km 17.3
- Paje - Pingwe Km 16.6
- Mkwajuni - Nungwi Km 18.4
- Pongwe - Matemwe Km 20.2
- Donge - Mkokotoni Km 12.8
- Mkoani - Makombeni Km 6.0

(b) Mtandao wenye urefu wa kilomita 102.9 za barabara umeanza kujengwa kwa upande wa Pemba, barabara hizo ni:-

- Kengeja - Mtambile – Mwambe Km 9
- Kenya - Chambani Km 3.2
- Mizingani - Wambaa Km 10
- Chanjamjawili- Tundaua Km 10
- Chanjaaani - Pujini Km 5
- Mtambile - Kangani Km 6.2
- Chake - Wete Km 30
- Wete - Konde Km 15
- Wete - Gando Km 13
- Mgagadu - Kiwani Km 5

(c) Jumla ya kilomita 375.2 za barabara za mjini na vijijini zimefanyiwa matengenezo kwa Unguja na Pemba.

(d) Barabara za Mfenesini – Bumbweni Km. 13.2 na Welezo – Dunga Km. 12.7 kwa upande wa Unguja ujenzi wake umeaanza.

**Bandari**

102. Mafanikio yaliyofikiwa katika Sekta ya Miundombinu ya Bandari ni haya yafuatayo:-

(a) Kukamilisha Mradi wa ujenzi wa gati ya Malindi Unguja, ujenzi wa gati ya abiria pamoja na ununuzi wa vifaa vipya vya kubebea makontena (Reach Stacker 2 na Terminal Tractor 2).

(b) Kukamilisha ujenzi wa chelezo cha Malindi na kuongeza urefu wake kutoka mita 100 hadi mita 140 kuelekea baharini.

(c) Bandari ya Mkoani Pemba imeimarishwa na kutangazwa kuwa ni Mlango Mkuu (Entry Point) wa kuingilia meli za kigeni.

(d) Kuifanyia matengenezo gati ya Wete Pemba, na kuongeza urefu wake hadi kufikia mita 125 kutoka mita 114; na upana wa mita 6 pamoja na kukamilisha ujenzi wa jengo la abiria.

(e) Kukamilisha ujenzi wa ukuta wa kuzuia mmong'onoko wa ardhi ili kuimarisha gati ya Wesha-Chake Chake Pemba.

**Usafiri wa Baharini**

103. Mafanikio yaliyofikiwa katika Sekta ya Usafiri wa Baharini ni haya yafuatayo:-

(a) Shirika la Meli pamoja na Makampuni Binafsi 8, yameendelea kutoa huduma ya usafiri wa baharini.Makampuni 7 kati ya hayo yanamilikiwa na Wazanzibari.

(b) Jumla ya vyombo vya baharini 49, hutoa huduma ya kusafirisha abiria na mizigo. Kati ya hivyo 21 ni vya abiria, 25 vya mizigo na 3 vya mafuta.

**Usafiri wa Anga**

104. Mafanikio yaliyofikiwa katika Sekta ya Usafiri wa Anga ni haya yafuatayo:-

(a) Kukamilisha maandalizi na kuanza kutekeleza Mpango Mkuu wa Uendelezaji wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Zanzibar.

(b) Matengenezo ya barabara ya kurukia na kutulia ndege (runway) ya Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Zanzibar kilicho na urefu wa mita 3,022 na upana wa mita 45 na ujenzi wa uzio yamekamilika.

(c) Ununuzi wa mtambo mpya wa kuongozea ndege, magari 2 ya kisasa ya zimamoto na gari la kufanyia doria za kiwanja umefanyika.

(d) Kukifanyia matengenezo kiwanja cha ndege cha Karume-Pemba, na kupatiwa gari la zimamoto.

(e) Kukamilika kwa matayarisho yote ikiwa pamoja na mikataba ya ujenzi wa jengo jipya la abiria la Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Zanzibar.

**Umeme**

105. Mafanikio yaliyofikiwa katika Sekta ya Umeme ni haya yafuatayo:-

(a) Kukamilisha kwa rasimu ya Sera ya Nishati.

(b) Kukamilika kwa Sheria na Kanuni za Uanzishwaji wa Shirika la Umeme.

(c) Kufikisha huduma ya umeme katika vijiji 141, kikiwemo kisiwa kidogo cha Kojani Pemba na Uzi Unguja.

(d) Kufikisha huduma ya umeme wa jua katika Kisiwa cha Tumbatu na Uzi pamoja na vijiji vya Cheju, Charawe na Matemwe Unguja.

(e) Taaluma ya matumizi ya nishati mbadala imetolewa kwa wananchi wa vijiji vya Kiembesambaki, Donge na Bububu.

(f) Kisiwa cha Pemba ambacho kwa muda mrefu kilitumia umeme wa "generator" kimeweza kuunganishwa na Gridi ya Taifa na kupata umeme wa uhakika kutoka Tanga. Hatua hii imewezesha visiwa vya Unguja na Pemba kuwa na umeme wa uhakika wa gridi.

(g) Kazi ya uwekaji wa njia ya pili ya umeme kupitia baharini kutoka Ubungo hadi Mtoni chini ya Mradi wa "Millenium Challenge" umewekwa saini.

(h) Kununua magenereta 32 yenye uwezo wa kuzalisha 25 MW kwa ajili ya umeme wa akiba.

**Ardhi**

106. Mafanikio yaliyofikiwa katika Sekta ya Ardhi ni haya yafuatayo:-

(a) Kukamilisha maandalizi ya Mpango Mkuu wa Kitaifa wa Matumizi bora ya Ardhi.

(b) Kufanya mapitio ya Sheria za Ardhi, ikiwemo Sheria ya Mahkama ya Ardhi (Land Tribunal Act) na Sheria ya Uhaulishaji wa Ardhi (Land Transfer Act) ya Mwaka 1994.

(c) Kufanya usajili wa ardhi katika eneo la Mji Mkongwe ambapo Viwanja 795 vimesajiliwa na kupatiwa hati rasmi.

(d) Kuanzisha Mahkama ya Ardhi, ili kutatua migogoro ya ardhi na kupunguza msongomano wa kesi za ardhi katika mahkama za kawaida.

(e) Kupima viwanja katika maeneo ya Tunguu, Kiwengwa na Nungwi Unguja, Tumbe na Ole-kianga kwa Pemba, kwa ajili ya makaazi bora na kilimo. Jumla ya viwanja 4,181 vimepima na kugawiwa kwa wananchi kwa ajili ya makazi, vikiwemo viwanja 308 kwa ajili ya shughuli za uwekezaji hususan ujenzi wa hoteli za kitalii, viwanda, kilimo na shughuli za kijamii.

## SEKTA YA HUDUMA ZA JAMII

### Elimu

107. Mafanikio yaliyofikiwa katika Sekta ya Elimu ni haya yafuatayo:-

(a) Sera ya Elimu imepitishwa. Elimu ya lazima sasa ni miaka 12 ambapo elimu ya maandalizi ni miaka 2, msingi miaka 6 na sekondari miaka 4.

(b) Uandikishaji wa watoto waliofikia umri wa kuanza darasa la kwanza umeongezeka kutoka asilimia 100 mwaka 2005, hadi asilimia 106.8 mwaka 2010. Mafanikio haya yameiwezesha Zanzibar kuvuka kiwango cha lengo la Milenia kabla ya mwaka 2015.

(c) Wananchi wamehamasishwa kuchangia ujenzi wa skuli mpya na kuongeza madarasa katika maeneo yao. Jumla ya madarasa 910 yamejengwa katika maeneo mbalimbali Unguja na Pemba.

(d) Ujenzi wa kituo cha Elimu Mbadala kiliyopo Rahaleo Unguja, umekamilika. Kituo kimefunguliwa tarehe 6 Juni 2006, na kuanza kutoa mafunzo ya kompyuta, uchongaji, upishi na ushoni.

(e) Ujenzi wa kituo cha Mafunzo ya Amali cha Mkokotoni Unguja na Vitongoji Pemba, umekamilika. Vituo hivi vinatoa mafunzo ya fani za ufundi, ufugaji, ushoni, useremala na kilimo.

(f) Ujenzi wa Maktaba Kuu ambao ulisimama kwa kipindi kirefu umekamilika. Maktaba hiyo imeanza kutoa huduma.

(g) Mafunzo ya Diploma ya Msingi yamenzishwa katika Vyuo vya Ualimu (badala ya cheti). Hatua hii imeimarisha ufundishaji katika ngazi ya Elimu ya Msingi na kutayarisha walimu bora.

(h) Vituo vya ualimu vimeimarishwa na kupatiwa vifaa vya kufundishia vikiwemo vitabu pamoja na kompyuta, ili viweze kutoa huduma kwa walimu kwa ufanisi.

(i) Chuo cha Ufundi cha Karume-Mbweni, kimepandishwa hadhi na kuwa "**Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia".**

(j) Ujenzi wa majengo mapya ya Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA) umeanzishwa huko katika eneo la Tunguu mkoa wa Kusini Unguja.

**Afya**

108. Mafanikio yaliyofikiwa katika Sekta ya Afya ni haya yafuatayo:-

(a) Kuifanyia mapitio Sera ya Dawa (National Drug Policy) na kuanzisha Sheria ya Dawa (Pharmaceutical Act) pamoja na Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala.

(b) Kuimarisha Hospitali kuu ya Mnazi Mmoja kwa kuzifanyia ukarabati sehemu muhimu na kuanzisha huduma ya Matibabu ya Haraka (Fast Track) pamoja na kuipatia vifaa vya kisasa (Mashine za X-Ray, CT Scan, Fluoroscopy, Ultra Sound, na Echo- Cardiography).

(c) Kuimarisha sehemu ya matibabu ya macho kwa kuifanyia ukarabati na kuipatia vifaa vya kisasa (AB Scan, automatic Torometer, Slit Lamp Machine, Electronic Operation Microscope na Phaco Emulsification Machine).

(d) Kujenga maabara mpya ya damu salama katika eneo la Sebleni Unguja.

(e) Kujenga jengo jipya la huduma kwa waathirika wa UKIMWI VCT (Gold Standard) na kuanza kutoa tiba ya ARV kwa waathirika wa UKIMWI katika vituo vya Kivunge, Bububu, Mwembeladu na Alrahma kwa Unguja na Chake Chake, Wete na Micheweni kwa Pemba**.**

(f) Kuimarisha huduma za hospitali ya Chake Chake na kuipatia mashine za kuchunguza VVU, ECG pamoja na vifaa vya upasuaji. Aidha, hospitali ya Wete imepatiwa "Solar Power" pamoja na sehemu ya kuhifadhia damu.

(g) Kuanzisha Mpango Maalumu wa huduma za afya na tiba ya macho, koo, pua na masikio vijijini kwa kutumia basi maalumu (mobile theatre).

(h) Kuanzisha chanjo ya kipindupindu katika Shehia ya Mtopepo, Chumbuni na Karakana kwa Unguja na Mwambe, Kengeja na Kojani kwa Pemba. Jumla ya wananchi 33,898 sawa na asilimia 65.2 ya wakaazi wa Shehia hizo wamepatiwa chanjo hiyo.

(i) Kuendeleza mapambano dhidi ya malaria kwa kufukiza dawa ya mbu majumbani na kugawa vyandarua vyenye dawa kwa watoto walio chini ya umri wa miaka mitano. Hatua hii imeiwezesha Zanzibar kuudhibiti ugonjwa huo kwa kiwango cha asilimia 98.

(j) Kuanzisha Mpango Maalum (Road Map) kwa ajili ya kupunguza idadi ya vifo vya akina mama wakati wa kujifungua na vituo vya Afya ya msingi vya daraja la pili (PHCU+) kuanza kutoa huduma za uzazi salama. Vituo hivyo ni Fuoni, Jambiani, Muyuni, Uzini, Nungwi, Bumbwini Misufini, Tumbatu kwa Unguja na Bogoa, Pujini Wesha na Makangale kwa Pemba.

(k) Kuendeleza Kampeni ya chanjo ya surua kwa watoto wenye umri wa miezi 6 hadi miaka 10 na utoaji wa matone ya Vitamin A kwa watoto wenye umri wa kati ya miezi 6-59 kwa kiwango cha asilimia 95%.

(l) Kujenga vituo vipya vya afya 43 vya daraja la kwanza, kuvifanyia matengenezo makubwa vituo 10 vya daraja la pili na kuvijenga upya vituo 11 vya daraja la pili, Unguja na Pemba.

(m) Kukamilisha ujenzi wa Hospitali ya daraja la pili ya Jimbo la Mpendae.

(n) Kupitisha Sheria ya Mdawa ya Kulevya ili kudhibiti uingizwaji na utumiaji wa madawa hayo nchini, na kulinda afya za wananchi hususan vijana.

(o) Kukiimarisha Chuo cha Taaluma za Sayansi za Afya Mbweni. Aidha, kwa kushirikiana na **Chuo Kikuu cha Matansas** cha Cuba, madarasa mawili ya madaktari wanafunzi yameanzishwa (darasa la wanafunzi 38 Unguja na wanafunzi 13 Pemba).

**Maji**

109. Mafanikio yaliyofikiwa katika Sekta ya Maji ni haya yafuatayo:-

(a) Kukamilisha maandalizi ya Sera ya Maji inayozingatia dhana ya ushirikishwaji wa wananchi katika kuchangia huduma za maji pamoja na Sheria ya Maji ya Mwaka 2007.

(b) Kuanzisha Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA).

(c) Kukamilisha Awamu ya Kwanza ya Mradi wa Usambazaji Maji katika mkoa wa Mjini Magharibi kwa kuchimba visima 11, kujenga matangi 4 ya kuhifadhia maji na miundombinu mipya ya usambazaji maji.

(d) Kukamilisha Mradi wa Usambazaji Maji Vijijini na kufikisha huduma ya maji safi na salama katika kijiji cha Kigongoni, Kilimani Tazari, Kilindi, Dunga, Kikungwi, Mfumbwi, Kidimni, Ubago, Mfenesini, Bumbwini, Kitope, Melinne, Welezo, Koani na Dungabweni kwa Unguja.

(e) Kukamilisha Mradi wa Usambazaji Maji Vijijini na kufikisha huduma ya maji safi na salama kijiji cha Pondeani, Gombani, Maziwang'ombe, Kiuyumbuyuni, Kwa Pweza, Kwa Bi Mtumwa, Kwale, Michungwani, Kiguuni, Shamiani, Kengeja, Mwambe, Mlindo, Mgelema, Mkungu, Kijichame Ngwachani, Kiuyu Momongawa, Nyali Shumbamjini,Wete Mjini, Bagamoyo, Kiuyu Penjewani, Mtambwe Kaskazini, Mtambwe Kivumoni, Ole kianga, Junguni na Gando kwa Pemba.

(f) Kufikisha huduma maji safi na salama kwa wananchi waishio mijini kwa kiwango cha asilimia 75 na wananchi wa vijijini kwa kiwango cha asilimia 60 Unguja na Pemba.

**Makazi**

110. Mafanikio yaliyofikiwa katika Sekta ya Makazi ni haya yafuatayo:-

(a) Kuandaa Sera ya Taifa ya Nyumba, ambayo inazingatia tasnia ya ujenzi na kuanzisha Bodi ya Kusajili Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji wa Majengo na Bodi ya Kusajili Wakandarasi.

(b) Kukamilisha ujenzi wa Nyumba Namba 9 na 10 Michenzani zenye jumla ya fleti 166 (24+142) na kuzigawa kwa wananchi wanaostahiki.

(c) Kuanza ujenzi wa nyumba moja ya Maendeleo huko Bambi, baada ya kukwama kwa muda mrefu.

## MAENEO MENGINE YA KIPAUMBELE

### Utamaduni na Michezo

111. Mafanikio yaliyofikiwa katika Sekta ya Utamaduni na Michezo ni haya yafuatayo:-

(a) Kuifanyia mapitio Sheria ya Baraza la Taifa la Michezo.

(b) Kuajiri walimu wa kigeni ili kufundisha na kukuza vipaji vya wanamichezo hasa wa mipira wa miguu, mpira wa kikapu, riadha na judo.

(c) Kuufanyia matengenezo makubwa uwanja wa Amani na kuimarisha miundombinu ya umeme katika uwanja wa Gombani Pemba.

(d) Kuanzisha ujenzi wa kituo cha michezo huko Dole.

(e) Kuandaa na kuendesha Matamasha ya Utamaduni kama vile ZIFF, SAUTI YA BUSARA, MKONGWE HAGEWA, MWAKA-KOGWA na "ZANZIBAR MUSIC AWARDS".

(f) Kuvipatia fursa vikundi vya utamaduni hasa ngoma na taarabu asilia, kutumbwiza kwenye hoteli mbalimbali za kitalii, ili kukuza na kuendeleza utalii wa kiutamaduni.

### Vyombo vya Habari

112. Mafanikio yaliyofikiwa katika Sekta ya Vyombo vya Habari ni haya yafuatayo:-

(a) Kuaandaa Sera ya Habari na Utangazaji, Shirika la Magazeti ya Serikali na Tume ya Utangazaji.

(b) Kuimarisha Studio za TVZ na Sauti ya Tanzania Zanzibar (STZ) kwa kuzipatia mitambo mipya na vifaa vya kisasa.

(c) Kupitisha Sheria ya kuanzisha Chuo cha Uandishi wa Habari na kuanza kutoa mafunzo ya Diploma ya Uandishi wa Habari.

(d) Kuanzisha vituo 4 vya Televisheni na 8 vya Radio vya binafsi.

**Majanga na Huduma za Uokozi**

113. Mafanikio yaliyofikiwa katika kuimarisha udhibiti wa Majanga na Huduma za Uokozi ni haya yafuatayo:-

(a) Kukiimarisha Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kwa mafunzo ya kazi na uongozi nje ya nchi (Uingereza, China na India) na vifaa vya kisasa zikiwemo gari 12. Kati yake 10 za zimamoto na 2 za kubebea wagonjwa.

(b) Kuanzisha Kitengo cha Taifa cha Maafa na Kamati za Maafa za Mikoa na Wilaya.

**Demokrasia na Utawala Bora**

114. Mafanikio yaliyofikiwa katika kukuza Demokrasi na Utawala Bora ni haya yafuatayo:-

(a) Kuridhia Sheria ya Bunge ya Uanzishwaji wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na kuiwezesha Tume hiyo kufanya kazi zake Zanzibar.

(b) Kuanzisha ujenzi wa ukumbi mpya wa Baraza la Wawakilishi.

(c) Kukamilisha ujenzi wa ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Zanzibar.

(d) Kuanzisha Kitengo Maalumu cha kupokea malalamiko ya wananchi.

(e) Kuanzisha Kamati ya pamoja ya viongozi wa dini tofauti ili kujenga mshikamano miongoni mwa viongozi na waumini wa dini ya Kiislamu na wa dini nyingine.

(f) Kuanzisha kanuni ya adhabu ya kutumikia jamii kwa wahalifu wa makosa madogo madogo, ili kupunguza msongamano katika Vyuo vya Mafunzo.

## Serikali za Mitaa

115. Mafanikio yaliyofikiwa katika kuimarisha Serikali za Mitaa ni haya yafuatayo:-

(a) Kukamilisha ujenzi wa majengo mapya ya ofisi za Mabaraza ya Miji ya Chake Chake, Wete, Mkoani pamoja na Halmashauri za Wilaya.

(b) Kukamilisha ujenzi wa soko la Wafanyabiashara wadogo wadogo la Saateni-Unguja.

(c) Kukamilisha ujenzi wa mitaro ya maji ya mvua katika Manispaa ya Zanzibar.

(d) Serikali Kuu kuendelea kutoa ruzuku kila mwezi kwa Baraza la Manispaa ya Zanzibar (Tshs. 100.6 milioni), Baraza la Mji wa Chake, Wete, Mkoani (Tshs. 59.25 milioni) na Halmashauri za Wilaya (Tshs. 15.66).

(e) Wananchi wamehamasishwa kushiriki katika ulinzi wa maeneo yao kwa njia ya ulinzi wa umma na Polisi Jamii. Aidha, Kamati za Ulinzi na Usalama za kila Shehia zimeundwa.

## Vikosi Maalumu vya SMZ

116. Mafanikio yaliyofikiwa katika kuimarisha Vikosi Maalumu vya SMZ ni haya yafuatayo:-

(a) Vikosi vyote vya SMZ vimeimarishwa kwa kupatiwa mafunzo ndani na nje ya nchi katika fani ya utawala na uongozi, sheria, fedha, mawasiliano ya kompyuta, ufundi na afya.

(b) Aidha, vikosi vimeimarishwa kwa kupatiwa zana na vifaa vya kisasa.

## KUYAENDELEZA MAKUNDI MBALIMBALI

## Watoto

117. Kwa upande wa maendeleo ya watoto mafanikio yafuatayo yamefikiwa:-

(a) Kuandaa Sera ya Uhai, Hifadhi na Maendeleo ya Watoto.

(b) Kuifanyia marekebisho Sheria ya Ajira ili kuwalinda watoto dhidi ya ajira mbaya.

(c) Kuandaa Mkakati wa Kitaifa wa Kupambana na Ajira Mbaya kwa Watoto na kuanzisha Kamati za Kupambana na Ajira Mbaya katika maeneo yaliyoathiriwa na tatizo hilo. Hatua hii imewezesha zaidi ya watoto 1,000 kuondolewa katika ajira mbaya.

(d) Kuanzisha Sera ya Elimu ambayo inayoanzisha Elimu ya Awali (Elimu ya Msingi) ya miaka 6 na umri wa watoto kuanza darasa la kwanza ni miaka 6 badala ya miaka 7.

(e) Huduma za chanjo ya surua kwa watoto wanaoanzia umri wa mia 6 hadi miaka 10 na kiwango cha utoaji wa matone ya Vitamin A kwa watoto wenye umri wa kati ya miezi 6–59 nacho kimefikia asilimia 95.

(f) Kuanzisha mradi wa ujenzi wa Nyumba ya Watoto yatima Mazizini Unguja.

**Vijana**

118. Kwa upande wa maendeleo ya Vijana mafanikio yafuatayo yamefikiwa:-

(a) Kuandaa Sera ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2005, Sera ya Ajira pamoja na Sheria ya Kazi, ambayo inatoa mwongozo kwa vijana kuunganisha nguvu zao na kuanzisha vikundi vya uzalishaji mali ili kuweza kujiajiri wenyewe.

(b) Kutoa mafunzo ya ujasiriamali ndani na nje ya nchi pamoja na kupatiwa vijana fursa ya kushiriki katika maonyesho ya Kimataifa yanayohusu biashara na kilimo.

(c) Kutenga maeneo maluumu kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya mafunzo ya ujasiriamali kama vile ushonaji, kilimo, uvuvi, useremala na utalii.

**Wanawake**

119. Kwa upande wa maendeleo ya Wanawake mafanikio yafuatayo yamefikiwa:-

(a) Serikali imeendelea kupiga vita mila na desturi zinazowabagua wanawake pamoja na kusimamia Sheria na Mikataba ya Kimataifa inayohusu ustawi wa wanawake kwa kuifanyia marekebisho Sheria Namba 4 ya Mwaka 1995 ya kuwalinda wari, wajane na vizuka. Lengo la Sheria hiyo ni kulinda haki zao.

(b) Kuwapatia mafunzo Waratibu wa Maendeleo ya Wanawake na Watoto wa Wilaya yanayohusu sheria, haki za binadamu, mkataba wa kimataifa wa kuondoa aina zote za ubaguzi dhidi ya wanawake na UKIMWI.

(c) Vikundi mbalimbali vya wanawake vimepatiwa mikopo kupitia Mifuko ya Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi pamoja na mafunzo ya ujasiriamali.

## CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA

120. Mbali na mafanikio makubwa ya kiuchumi na kijamii, uchumi wa Zanzibar ulipata pigo kutokana na kuchakaa kwa njia ya umeme chini ya bahari inayounganisha Zanzibar na gridi ya Taifa kutoka Tanzania Bara na kusababisha kukatika kwa umeme mwezi Machi, mwaka 2008 na mwezi Novemba 2009. Aidha, ukame na hali ya kudorora kwa uchumi wa dunia mwanzoni mwa mwaka 2009 ni miongoni mwa changamoto kubwa zilizojitokeza katika kipindi hiki na kudhoofisha uwezo wa Serikali katika kuendeleza huduma muhimu za kiuchumi na kijamii kwa wananchi.

## MALENGO YA ILANI YA CCM KWA AJILI YA UCHAGUZI MKUU WA MWAKA 2010-2015

121. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2010-2015) CCM ikipata ridhaa ya wananchi itaiongoza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na kuhakikisha kwamba, inatekeleza kikamilifu malengo ya Ilani hii na kuaandaa mipango mbalimbali ya maendeleo kwa kuzingatia Mwelekeo wa Sera za CCM katika miaka ya 2010 hadi 2020, Malengo ya Maendeleo ya Milenia, Dira ya Maendeleo ya Zanzibar (2020) na Awamu ya Tatu ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar (MKUZA).

## SEKTA YA KIUCHUMI

### Kukuza Uchumi

122. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2010-2015), CCM itahakikisha kwamba Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, inaendeleza mafanikio yote ya kiuchumi yaliyofikiwa hadi sasa zikiwemo Sera na Sheria za Uwekezaji, ili kuchochea kasi ya uwekezaji na ujenzi wa msingi wa uchumi endelevu unaokua na kuendeshwa kwa nguvu ya soko na kutekeleza hatua zifuatazo:-

(a) Kujenga mazingira yatakayowezesha uchumi wa Zanzibar kufikia kiwango cha ukuaji wa asilimia 10, mfumko wa bei kufikia kiwango cha chini cha asilimia 7 na pato la kila mwananchi kuongezeka kutoka Tsh. 726,000/= za sasa hadi Tsh. 884,000/= ifikapo mwaka 2015.

(b) Kuimarisha udhibiti wa mapato na matumizi ya Serikali, kuziba mianya ya uvujaji wa mapato ya Serikali na kuongeza kiwango cha ukusanyaji wa

mapato ya ndani kwa uwiano wa asilimia 22 ya pato la taifa na kushusha kiwango cha nakisi ya Bajeti ya Serikali kutoka uwiano wa asilimia 9.2 ya pato la taifa (mwaka 2007/2008) na kufikia asilimia 8.0 ifikapo mwaka 2014/2015.

(c) Kusimamia utekelezaji wa sheria za fedha ikiwemo Sheria ya Kodi na Makampuni na kuimarisha miundombinu ya kiuchumi.

(d) Kuendeleza juhudi za kuimarisha maeneo huru ya kiuchumi ya Fumba na Micheweni pamoja na Bandari huru.

123. Kuendeleza jitihada za kuimarisha sekta binafsi ili kuongeza mchango wake katika uwekezaji kutoka asilimia 45 mwaka 2009 hadi asilimia 75 mwaka 2015. Hatua zifuatazo zitatekelezwa:-

(a) Kufanya mapitio ya sheria na kanuni za biashara ili kuimarisha uwazi, kupunguza urasimu na vikwazo katika biashara ukiwemo mlolongo wa Leseni na Mamlaka za kodi.

(b) Kuwa na uwakilishi wa sekta binafsi kwenye vikao vya baadhi ya Bodi za Mashirika na Taasisi za Serikali zenye kutoa huduma za kiuchumi na kupanga kodi mbalimbali za biashara, ili kujenga mahusiano mema, kuleta ufanisi na tija katika makusanyo ya kodi na kukuza uchumi wa nchi kwa ujumla.

(c) Kuandaa mazingira bora ya kiuchumi yatakayoweza kuvishawishi vyombo vya fedha kutoa mikopo yenye masharti na riba nafuu kwa wawekezaji wa ndani.

(d) Kuendeleza utekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi (Zanzibar Growth Strategy), Awamu ya Tatu ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar (MKUZA) pamoja na kutekeleza mageuzi ya kiuchumi hususan sera ya Fedha, Kilimo, Viwanda vidogo na Biashara.

**Kupambana na Umasikini**

124. Mwelekeo wa Sera za CCM katika miaka ya 2010-2020 unabainisha kuwa, mkakatia wa kuwawezesha wananchi kiuchumi umelenga katika kuhakikisha kwamba wananchi wenyewe wanamiliki na kuendesha uchumi wa nchi yetu ama mmoja mmoja kwa kupitia vyama vyao huru vya ushirika wa aina mbalimbali au kwa kupitia makampuni ya wananchi ya ubia ambamo maelfu ya wananchi watanunua hisa na kwa kupitia umilikaji wa dola kwa mashirika yote yatakayoendelea kuwa mikononi mwake.

125. Kwa kutambua kwamba, wananchi walio wengi bado ni masikini na wanakabiliwa na tatizo la ukosefu wa maarifa, ujuzi na mitaji katika kilimo, biashara na ujasiriamali hali ambayo ni kizuizi cha maisha bora na mapambano dhidi ya umasikini, CCM itaielekeza Serikali (SMZ) kuendeleza jitihada za kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kuendeleza mafunzo na elimu ya ujasiriamali kwa wananchi na kuhamasisha matumizi ya kanuni za kilimo bora na Sayansi na Teknolojia rahisi katika uzalishaji mali.

(b) Kuendeleza utekelezaji wa Awamu ya Tatu ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar (MKUZA).

(c) Kuimarisha Mifuko ya Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi ili kukuza uwezo wake wa kutoa mikopo kwa wananchi na kuwawezesha kutumia fursa zilizopo katika maeneo wanayoishi ili kujiendeleza kiuchumi.

(d) Kuendelea kuunga mkono juhudi za uanzishwaji wa vikundi vya ushirika na SACCOS hasa kwa vijana na akina mama.

(e) Kuyaendeleza maeneo maalumu ya kufanyia shughuli za biashara ndogo ndogo hasa mijini na kuimarisha mfumo na taratibu za utoaji wa leseni za biashara wenye kuzingatia usafi wa miji na hifadhi ya mazingira.

(f) Kutilia mkazo dhana ya kujitegemea kwa kuzitambua rasilimali na biashara za wanyonge ambazo ziko kwenye sekta isiyo rasmi ili waweze kuziendeleza kuboresha maisha yao.

## KUHUSU SEKTA ZA UZALISHAJI MALI

### Mapinduzi ya Kilimo

126. Sekta ya kilimo ina mchango mkubwa katika kukuza uchumi na maendeleo ya Zanzibar. Kilimo ndio chanzo kikuu cha ajira kwa wananchi walio wengi hasa vijijini, na huchangia asilimia 27.3 ya Pato la Taifa (GDP) katika uchumi wa Zanzibar na kutoa ajira kwa asilimia 44 ya wananchi wa vijijini.

127. Kwa kutambua umuhimu na mchango wa sekta ya kilimo katika kujenga msingi wa uchumi wa kisasa, katika kipindi cha miaka mitano ijayo(2010-2015) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa CCM, itaendelea kuimarisha Mapinduzi ya kilimo kwa kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kusimamia utekelezaji wa Sera na Programu mbalimbali za Kilimo na kuzifanyia mapitio kwa lengo la kuziimarisha. Aidha, Sera ya Chakula na Lishe na Sera ya Mifugo zitaanzishwa.

(b) Kuendelea kuhimiza na kutilia mkazo mafunzo na matumizi ya kanuni za kilimo bora kwa mazao ya chakula, biashara na matunda, huduma za ugani na zana za kisasa wakiwemo wanyamakazi, matrekta makubwa na madogo.

(c) Kuendeleza miundombinu ya umwagiliaji maji na kuhamasisha uvunaji wa maji ya mvua, ili yatumike katika kuzalisha mazao mengi ya chakula na mboga mboga kwa njia ya umwagiliaji maji.

(d) Kuihamasisha sekta binafsi kutoa huduma ya pembejeo katika maeneo ya kilimo.

(e) Kuendelea kukiimarisha Chuo cha Kilimo Kizimbani na kuendeleza utafiti wa mbegu bora za mazao ya chakula, biashara na mboga mboga. Njia ya utafiti shirikishi itatumika kwa lengo la kuwawezesha wakulima kushiriki kikamilifu katika kutoa mawazo yao kuhusiana na matatizo yanayowakabili.

(f) Kuanzisha mradi maalumu wa kuwawezesha wananchi na sekta binafsi kuingia katika kilimo cha kisasa na cha kibiashara cha mazao ya viungo na matunda.

(g) Kuendeleza vituo vya huduma na udhibiti wa maradhi ya mazao, wadudu waharibifu na elimu kwa wakulima kuhusu hifadhi ya mazao na utafutaji wa masoko ya ndani na nje kwa kutumia Nembo ya Zanzibar.

(h) Kuendeleza uzalishaji wa mazao ya biashara hasa karafuu, matunda na viungo na kutilia mkazo kilimo hai na kilimo mseto, ili kuhifadhi mazingira na kupunguza matumizi ya kemikali zenye sumu kali kwa lengo la kuongeza kasi ya ukuaji wa sekta ya kilimo hadi kufikia asilimia nne (4%) ifikapo 2015.

(i) Kuendeleza kazi ya ukaguzi na karantini dhidi ya maradhi na wadudu waharibifu wa mimea na mfugo ili kudhibiti uingiaji nchini wa maradhi hayo.

**Mapinduzi ya Ufugaji**

128. Kuleta mapinduzi ya ufugaji Zanzibar si tu kunazingatia tija na ubora wa mazao ya mifugo, bali vile vile tatizo la uhaba wa ardhi, ongezeko la idadi ya watu na kupanuka kwa shughuli mbalimbali za maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika ardhi ambayo ukubwa wake hauongezeki.

129. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2010-2015) Serikali ya Mapinduzi Zanzibar chini ya uongozi wa CCM itaendelea kuimarisha ufugaji wa kisasa wa ng'ombe wa maziwa, mbuzi na kuku wa nyama na mayai ili kuongeza tija na kipato cha wafugaji, kwa kutekeleza hatua zifuatazo:-

(a) Kusimamia utekelezaji wa Sera na Sheria ya Mifugo pamoja na programu za miradi mbalimbali itakayowawezesha wafugaji wadogo kuendeleza ufugaji wa kisasa (Zero-grazing) na kuongeza uzalishaji wa nyama, maziwa, ngozi na mayai kwa ajili ya mahitaji ya soko la ndani na nje ya Zanzibar.

(b) Kuendeleza kazi za utafiti na upandishaji wa ng'ombe kwa njia ya sindano, ili kupata mbegu bora ya ng'ombe wa maziwa na nyama na kuwagawia wafugaji wadogo kwa njia ya mkopo.

(c) Kuendeleza Vituo vya Huduma za Ufugaji na huduma za kinga na tiba ya mifugo na kuihamasisha sekta binafsi kutoa huduma za afya na pembejeo za mifugo.

**Mapinduzi ya Uvuvi na Mazao ya Baharini**

130. Kwa kuzingatia maumbile na jiografia ya Zanzibar, uvuvi ni shughuli muhimu ya kiuchumi miongoni mwa wananchi wengi wanaoishi pembezoni mwa mwambao wa bahari. Kutokana na ukosefu wa zana bora za uvuvi, wavuvi wadogo wadogo wamekuwa wakitumia zana duni ambazo husababisha uharibifu mkubwa wa mazingira.

131. Ili kuimarisha uvuvi wa kisasa ambao ni endelevu na unaozingatia uhifadhi wa mazingira ya bahari na kukuza kipato cha wavuvi, CCM kupitia Ilani hii itaielekeza Serikali kuchukua hatua zifuatazo:-

(a) Kuandaa Sera ya Uvuvi na kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Uvuvi kwa lengo la kuimarisha uvuvi na uhifadhi wa mazingira ya bahari.

(b) Kuendelea kuwahamasisha wavuvi juu ya uanzishaji wa vikundi vya ushirika na matumizi ya maarifa ya kisasa na zana bora za uvuvi na kuwapatia misaada na mikopo ya zana hizo, ili uvuvi uwe wa kisasa zaidi utakaokidhi mahitaji ya soko la ndani.

(c) Kusimamia mpango shirikishi wa kuyaendeleza maeneo ya hifadhi ya bahari yakiwemo maeneo mapya ya Tumbatu, Chumbe-Bawe, Menai, MIMCA na PECCA.

(d) Kujenga mazingira ya kuvutia sekta binafsi kuwekeza katika uvuvi wa bahari kuu, ujenzi wa kiwanda cha samaki na zana za kisasa za uvuvi.

(e) Kufanya utafiti juu ya uwezekano wa kulima mwani aina ya **"cottonii"** kwenye kina kirefu cha maji na kuwahamasisha wananchi kuanzisha vikundi vya ushirika ili kurahisisha upatikanaji wa nyenzo za uzalishaji na soko la uhakika. Aidha, wananchi watahamasishwa kuanzisha vikundi vya ufugaji wa chaza ili kupata lulu na kuongeza kipato cha kuwawezesha kupambana na umasikini.

(f) Kuendeleza uhifadhi wa viumbe hai na adimu vya baharini (pomboo, kasa n.k) na kuvitumia kama vivutio vya utalii.

**Maliasili**

132. Maumbile ya Visiwa vya Unguja na Pemba yamesheheni utajiri mkubwa wa maliasili ambao ni kivutio cha watalii. Ili kuiendeleza zaidi sekta ya misitu, katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2010-2015) CCM itaielekeza Serikali kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kusimamia ulinzi na udhibiti wa maeneo ya hifadhi ya misitu ya Taifa ya Jozani, Unguja na Ngezi, Pemba pamoja na misitu ya asili kwa mashirikiano na wananchi na wadau mbalimbali.

(b) Kuendeleza utunzaji na hifadhi ya wanyama pori walio katika hatari ya kutoweka hasa kimapunju, popo wa Pemba na paa nunga na kuwatumia kama vivutio vya utalii.

(c) Kuendelea kuwahamasisha wananchi na kuwahimiza wajiunge pamoja kuanzisha vikundi vya jamii vitakavyopatiwa mafunzo ya utunzaji na upandaji miti katika maeneo wanayoishi na pembezoni mwa barabara, ufugaji wa nyuki na uvunaji wa asali.

**Mazingira**

133. Mazingira ni suala mtambuka ambalo linagusa sekta zote za kiuchumi na kijamii. Hivyo, uharibifu wa mazingira ni tishio la taifa zima na mazingira endelevu ni muhimu kwa maslahi ya kizazi cha sasa na kijacho.

134. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2010-2015) CCM kupitia Ilani hii itahakikisha kuwa, Serikali inatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuandaa Sera ya Mazingira na kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Hifadhi ya Mazingira katika maeneo ya ardhi, bahari na ukanda wa pwani.

(b) Kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa utunzaji wa hifadhi ya mazingira na kuimarisha ukaguzi katika maeneo ya makazi na sehemu za kazi, viwanda na mahoteli.

(c) Kufanya mapitio ya miradi ya vitega uchumi ili kuangalia masuala ya mazingira na kupendekeza hatua za utekelezaji.

**Utalii**

135. Zanzibar ni miongoni mwa Visiwa vyenye historia na vivutio vingi vya utalii. Fukwe mwanana, misitu ya asili, wanyama, magofu na urithi wa Kimatifa wa Mji Mkongwe wa Zanzibar ni miongoni mwa vivutio hivyo.

136. Ili kuendeleza sekta ya utalii na kuifanya itoe mchango mkubwa zaidi katika uchumi wa Zanzibar na maendeleo ya wananchi kwa jumla, katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2010-2015), Serikali ya Mapinduzi Zanzibar chini ya uongozi wa CCM, itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria na Mpango Mkuu wa Utalii na kufanya mapitio ili kuziimarisha kwa kuandaa kanuni za utekelezaji wake.

(b) Kuendeleza jitihada za kuitangaza Zanzibar katika masoko mapya hasa ya Asia, ili kuongeza mapato ya utalii na kuchukua hatua za kudhibiti mianya ya uvujaji wa mapato, yakiwemo mapato ya utalii wa vikundi (package tourism).

(c) Kuendeleza na kuimarisha utalii wa kumbukumbu za kihistoria, utalii wa kiutamaduni na utalii wa ndani wenye kutunza mazingira.

(d) Kuibua maeneo mapya ya vivutio vya utalii yakiwemo mapango, michezo ya asili, matamasha, maeneo ya hifadhi ya wanyama (Zoo), "Aquarium" na kijiji kilichozama Mkumbuu kisiwani Pemba na kuongeza idadi ya watalii na muda wa kukaa nchini.

(e) Kufanya uhakiki wa hoteli ili kubaini hali halisi ya kila hoteli, kupanga madaraja yake, kuzisajili na kuanzisha mfumo wa mawasiliano ya komputa kwa lengo la kuimarisha huduma, gharama na mapato ya Serikali.

(f) Kuimarisha huduma za utalii kwa kuziendeleza Jumuiya za watoa huduma kama vile watembezaji na wasafirishaji watalii wakiwemo "Tour Operators", wenye gari za Taxi na boti ziendazo kasi.

(g) Kuhamasisha wananchi kuendeleza miradi ya uzalishaji mali, hususan kilimo cha kisasa cha mboga mboga na matunda ili kuhudumia sekta ya utalii na kujiendeleza kiuchumi.

(h) Kupunguza idadi ya vituo vya ukaguzi katika maeneo wanayopita watalii ili kuwaondolea usumbufu na kuandaa vijarida vya taarifa za watalii na maelekezo katika maeneo ya kuingilia "Entry Points".

(i) Kukiimarisha Chuo cha Maendeleo ya Utalii kwa kuboresha miundombinu yake, kuandaa Dira ya Chuo, kuboresha viwango vya elimu ya wakufunzi na huduma kwa wanafunzi.

**Mapinduzi ya Viwanda na Biashara**

137. Sekta ya Viwanda na Biashara ni yenye umuhimu mkubwa kwa maendeleo ya uchumi na ustawi wa wananchi. Ili kuendeleza shughuli za viwanda na biashara na kuinua uchumi wa Zanzibar, CCM katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2010-2015) itaielekeza Serikali kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Uendelezaji wa Viwanda Vidogo na vya Kati na kufanyia mapitio Sheria ya Biashara ya Mwaka 2006 ili kubaini mapungufu na kuchukua hatua zinazopasa pamoja na kuweka mfumo bora zaidi wa utoaji wa leseni za biashara .

(b) Kuwaendeleza wawekezaji, wazalishaji wa ndani na wajasiriamali wadogo na wa kati (SMEs) kwa kuwapatia fursa za mafunzo, mikopo ya fedha na vifaa vya kisasa vya uzalishaji mali ili kuzalisha bidhaa bora kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi.

(c) Kufanya mapitio ya vivutio vya uwekezaji ili kuviendeleza na kuimarisha mtandao wa usambazaji wa habari za biashara kwa wafanyabiashara. Wawekezaji wenye mitaji mikubwa hasa kutoka nje watahamasishwa kuwekeza katika miundombinu na viwanda vinavyozalisha ajira nyingi vikiwemo vya nguo na usindikaji wa mazao.

(d) Kufanya mapitio ya Sheria Namba 2 ya Kusimamia Mwenendo wa Biashara na Kumlinda mlaji ya Mwaka 1995, Sheria Namba 4 ya Mizani na Vipimo ya Mwaka 1983 na Sheria ya Biashara Namba 4 ya Mwaka 1989.

(e) Kuanzisha Taasisi ya Viwango ya Zanzibar.

(f) Kufanya utafiti ili kubaini maeneo ambayo wawekezaji wageni watavutiwa kuingia ubia na wafanyabiashara wa ndani na kuwawezesha

wafanyabiashara wazalendo kupata mitaji kutoka katika vyombo vya fedha kwa riba nafuu.

(g) Kufanya utafiti utakaowezesha usarifu wa zao la karafuu kutengeneza dawa na aina nyingine za matumizi ya zao hilo kwa kukitumia Kiwanda Cha Makonyo kilichoko Pemba.

(h) SMZ kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano na sekta binafsi, itaanzisha mchakato wa kujenga viwanda vinavyotumia malighafi inayopatikana hapa nchini hususan viwanda vya nguo, samaki, sukari, viwanda vya kuunganisha mitambo ya aina mbalimbali na vya kusindika mazao ya kilimo na matunda ili kuyaongezea thamani katika soko na kukuza uchumi.

(i) Kuanzisha na kuendeleza eneo la Uwanja wa Maonesho ya Biashara ya Kimataifa na kuwahamasisha wafanyabiashara, wajasiriamali na wazalishaji wa bidhaa mbalimbali kutumia fursa za masoko ya EAC, SADC, AGOA na EU.

(j) Kuimarisha shughuli za bandari huru katika maeneo ya Maruhubi na Uwanja wa Ndege – Zanzibar na kuanzisha maeneo mapya.

**Vyama vya Ushirika**

138. Vyama vya Ushirika ni chombo cha kuwaunganisha na kuwawezesha wananchi kubadili hali ya maisha yao na kujiendeleza kiuchumi. Aidha, vyama vya ushirika wa kuweka na kukopa (SACOSS) ni nyezo ya kuwapatia wananchi mitaji kutokana na michango yao na mikopo kutoka katika vyombo vya fedha.

139. Ili kuendeleza ushirika, katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2010-2015) CCM itaielekeza Serikali kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Vyama vya Ushirika na programu mbalimbali za kuendeleza sekta ya ushirika.

(b) Kuendelea kusajili vyama vipya vya ushirika na kuendeleza ukaguzi wa vyama vya ushirika.

(c) Kuendeleza mafunzo kuhusu uendeshaji na uongozi wa vyama vya ushirika, uzalishaji mali, utunzaji wa rasilimali na hesabu za ushirika.

**Sekta za Miundombinu ya Kiuchumi**

140. Maendeleo endelevu ya uchumi yanategemea sana ubora wa miundombinu ya kiuchumi ambayo hujumisha barabara, bandari,viwanja vya ndege na umeme. Katika kipindi kilichopita Serikali ya Mapinduzi Zanzibar chini ya uongozi wa CCM, imepata mafanikio makubwa katika ujenzi wa miundombinu ya kiuchumi, kuimarisha ustawi wa jamii na kuvutia uwekezaji na biashara.

141. Ili kuendeleza kazi ya kuimarisha miundombinu ya kiuchumi, katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2010-2015) CCM itahakikisha kuwa SMZ, inatekeleza kazi zifuatazo:-

**Barabara**

(a) Kuendeleza kazi ya utunzaji na matengenezo ya barabara zilizokwisha jengwa, ili ziendelee kuwa imara kwa kiwango kinachokubalika.

(b) Kukamilisha ujenzi wa barabara ya Mfenesini hadi Bumbwini (Km.13) na Welezo hadi Dunga (Km.12.75) kwa Unguja na Km. 108.9 za barabara za Pemba.

(c) Kujenga jumla ya Km. 119.9 za barabara Unguja, na kilomita 76.6, Pemba kama ufuatavyo:-

**Unguja**

(d) **Kujenga kilomita 152.9 za barabara za**:-

- Matemwe - Muyuni - Km. 6.5
- Kichwele - Pangeni - Km. 4.0
- Kizimbani - Kiboje - Km. 6.0
- Njianne - Umbuji/Uroa - Km. 11.0
- Fuoni - Kombeni - Km. 6.7
- Koani - Jumbi - Km. 6.0
- Jendele - Cheju-Kae bona - Km. 6.0
- Jozani - Ukongoroni Charawe- Bwejuu - Km. 15
- Mkwajuni - Kijini - Km. 5.5
- Pale - Kiongele - Km. 11
- Fumba ring road - Km. 8
- Bububu - Mtoni - Kinazini - Malindi - Km. 9
- Creek road - Mkunazini - M'moja - Km. 1.2
- Funi - Magomeni-Kariako-Mkunazini - Km. 8.3

- Welezo - Amani-Ng'ambo - Kariakoo - Km. 3.5
- Amani - Mtoni - Km. 4
- U'ndege - K'samaki- Kilimani - M'moja - Km. 7
- Nyumba mbili - Maili Nne - Km. 1.2
- Mahonda - Donge - Km. 14
- Fukuchani - Kigongoni - Km. 8
- Utambi - Tazari - Km. 3
- Oshora - Kilimani - Km. 4
- Donge-Mtambile - Mwanda - Km. 3
- Amani-Freshi - Mboriborini - Km. 1

**Pemba**

(e) **Kukamilisha ujenzi wa kilomita 108.9 za barabara za**:-

- Mtambile – Kengeja - Mwambe - Km. 9
- Kenya - Chambani - Km. 3.2
- Mizingani - Wambaa - Km. 10
- Chanjamjawiri- Tundaua - Km. 10
- Chanjaani - Pujini - Km. 5
- Mtambile - Kangani - Km. 6.2
- Chake - Wete - Km. 30
- Wete - Konde - Km. 15
- Wete - Gando - Km. 13
- Mgagadu - Kiwani - Km. 7.5

**Pemba**

(f) **Kujenga kilomita 94.5 za barabara za:-**

- Ole - Kengeja - Km. 35
- Bahanasa-Daya - Mtambwe - Km. 13.6
- Mzambarau takao - Pandani Finya - Km. 8
- Mzambarau Karim-Mapofu - Km. 8.6
- Chwale - Kojani - Km. 2
- Kipangani - Kangagani - Km. 3
- Mkanyageni - Kangani - Km. 6.5
- Finya - Kicha - Km. 8.8
- Shumbaviamboni - Tumbe - Km. 5
- Kuyuni - Ngombeni - Km. 4

(g) Aidha, Serikali itaendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria zinazohusiana na usafiri na kukamilisha maandalizi ya kanuni za Sheria ya Usalama Barabarani pamoja na kuimarisha Karakana Kuu ya Serikali.

**Bandari**

142. Huduma za bandari zinao mchango mkubwa katika kukuza uchumi na ustawi wa jamii. Ili kuendeleza miundombinu ya bandari na kuimarisha uchumi wa Zanzibar, katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2010-2015) CCM itaielekeza Serikali kutekeleza hatua zifuatazo:-

(a) Kujenga majengo mapya ya kuhudumia abiria katika bandari ya Malindi pamoja na matengenezo ya maeneo ya kuhifadhia makontena bandarini na kuimarisha vifaa katika bandari hiyo.

(b) Kuifanyia matengenezo bandari ya Mkoani kwa kurekebisha sehemu ya gati iliyodidimia pamoja na kuipatia vifaa vya kuhudumia mizigo.

(c) Kuiendeleza zaidi gati ya Wete kwa kuongeza urefu na upana wake, kuipatia vifaa vya kuhudumia mizigo na kujenga ramp ya kuhudumia vyombo vya aina ya **"Land Craft".**

(d) Kuimarisha gati ya Mkokotoni kwa kujenga jeti kwa ajili ya majahazi na usafiri wa wananchi hasa wa Tumbatu.

(e) Kusimamia utekelezaji wa Mpango Mkuu (Master Plan) wa bandari ya Malindi, ikijumuisha huduma za bandari huru na kuendelea kutafuta uwezo wa kujenga Bandari Mpya ya Kibiashara ya Mpiga Duri.

**Usafiri wa Baharini.**

143. Ili kuimarisha huduma za usafiri wa baharini, katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2010-2015) CCM itahakikisha kwamba Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, inatekeleza hatua zifuatazo:-

(a) Kuliimarisha Shirika la Meli la Zanzibar, ili liweze kujiendesha kibiashara.

(b) Kubadili mfumo wa uendeshaji wa Afisi ya Mrajis wa Meli na kuwa Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Usafiri wa Baharini 'Maritime Authority.

(c) Kuendeleza mazingira ya kuvutia wawekezaji wa nje na ndani ili kuwekeza zaidi katika sekta ya usafiri wa baharini na kuboresha huduma ya usafiri kwa wananchi na wageni hususan watalii wanaotembelea Zanzibar.

**Usafiri wa Anga:**

144. Usafiri wa anga ni moja ya nyenzo muhimu katika kukuza uchumi na kichocheo cha kuendeleza Sekta ya utalii. Ili kuiendeleza zaidi Sekta ya Usafiri wa Anga, katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2010-2015) CCM itahakikisha kuwa SMZ, inatekeleza kazi zifuatazo:-

(a) Kusimamia utekelezaji wa Mpango Mkuu wa Uendelezaji wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Zanzibar na kukamilisha ujenzi wa jengo jipya la abiria.

(b) Kukamilisha kazi ya ujenzi wa uzio, uwekaji wa taa katika barabara ya kurukia na kutulia ndege na uimarishaji huduma za umeme kwa kukipatia "generator" la akiba Kiwanja cha Ndege cha Karume Pemba.

(c) Kuwapatia mafunzo na vifaa vya kisasa wafanya kazi wa Kiwanja cha Ndege cha Zanzibar na Karume Pemba pamoja na kuimarisha huduma za zima moto na usalama wa viwanja vya ndege.

**Umeme:**

145. Nishati ya umeme ni muhimu katika kujenga Msingi wa Uchumi wa Kisasa wa Taifa linalojitegemea. Ili kuendeleza kazi ya usambazaji wa nishati ya umeme na kukuza maendeleo ya kiuchumi na kijamii, CCM katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2010-2015) itahakikisha kuwa, kazi zifuatazo zinatekelezwa na Serikali:-

(a) Kusimamia utekelezaji wa Sera na Sheria ya Nishati na kuendeleza juhudi za utafiti wa vyanzo mbadala vya nishati ya umeme, ukiwemo umeme wa jua, upepo, mawimbi ya bahari, mafuta na gesi asilia.

(b) Kukamilisha utekelezaji wa mradi wa kujenga njia ya pili ya umeme inayopita chini ya bahari kutoka Ras Kiromoni Tanzania Bara hadi Fumba Unguja (Mradi wa MCC).

(c) Kuendeleza kazi ya usambazaji umeme mijini na vijijini, vikiwemo visiwa vidogo vidogo vinavyoishi watu katika maeneo mbalimbali Unguja na Pemba.

(d) Kuwahamasisha wananchi juu ya matumizi ya majiko sanifu, gesi asilia na umeme unaotokana na vyanzo mbadala kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, hotelini na sehemu zote za majeshi na daghalia.

(e) Kuimarisha mazingira ya kuwavutia wawekezaji wa nje na ndani ili kuwekeza katika sekta ya nishati ya umeme.

(f) Kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Sekta ya Nishati kwa kuwapatia mafunzo ya fani mbali mbali za Nishati na Madini.

(g) Kuliimarisha Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO), kwa kulijengea mazingira bora zaidi ili liweze kujiendesha kibiashara.

(h) Kusimamia utekelezaji wa Sheria na Kanuni za Uendeshaji wa Bohari, **'Depot'** na usambazaji wa nishati ya mafuta kwa wananchi na kuhakikisha kuwa zinachangia katika mapato ya nchi.

**Ardhi:**

146. Ardhi ni rasilimali namba moja katika Ujenzi wa Msingi wa Uchumi wa kisasa na kichocheo cha maendeleo ya wananchi. Umiliki wa ardhi pia ni moja ya malengo ya Mapinduzi ya Zanzibar ya tarehe 12, Januari1964.

147. Ili kuendeleza na kusimamia matumizi bora ya ardhi, katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2010-2015), CCM itahakikisha kuwa SMZ inatekeleza yafuatayo:-

(a) Kukamilisha maandalizi ya Sera ya Ardhi ya Zanzibar na kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Kitaifa wa Matumizi bora ya Ardhi.

(b) Kuendeleza kazi ya kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa matumizi bora ya ardhi na kuongeza kasi ya upimaji wa viwanja katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya makazi na shughuli nyingine za maendeleo.

(c) Kuendeleza kazi ya usajili wa ardhi katika maeneo mbalimbali hasa yale yasiyopimwa na kuwapatia wahusika hati za umiliki wa ardhi hiyo kwa mujibu wa sheria.

(d) Kuziimarisha Mahakama za Ardhi na kuanzisha Mahkama za Ardhi katika kila mkoa ili kusogeza huduma hiyo karibu na wananchi na kupunguza migogoro ya ardhi.

(e) Kupanua shughuli za usajili wa ardhi kwenye maeneo ya fukwe na maeneo ya miji yaliyopangwa na yasiyopangwa.

(f) Kufanya mapitio ya ramani zote na kuzifanyia marekebisho kwa mujibu wa mabadiliko yanayojitokeza, kuhuwisha ramani za miji ya Zanzibar (Unguja mjini, Chake chake, Wete, na Mkoani) vikiwemo visiwa vidogo vidogo na kuchapisha ramani mpya za visiwa vya Unguja na Pemba.

## Sekta za Huduma za Jamii

### Elimu

148. Elimu ya kisasa na hasa Sayansi na Teknolojia ina nafasi ya pekee katika kufanikisha ujenzi wa msingi wa uchumi wa kisasa wa taifa linalojitegema. Kwa kutambua ukweli huu Serikali ya Mapinduzi Zanzibar chini ya uongozi wa CCM imetoa kipaumbele cha kwanza kwa sekta ya elimu.

149. Ili kuiendeleza sekta ya Elimu, katika kipindi cha mwaka cha miaka mitano ijayo (2010-2015), CCM itahakikisha kuwa SMZ inatekeleza yafuatayao:-

(a) **Elimu ya Maandalizi**

(i) Kuendeleza juhudi za kuongeza ushiriki wa wanafunzi katika ngazi ya Elimu ya Maandalizi kutoka 18% hadi 50% ifikapo mwaka 2015.

(ii) Kutoa mafunzo kwa walimu wa Skuli za Maandalizi na kutayarisha vifaa vya kufundishia na kujifunzia (vikiwemo vitabu) vya Elimu ya maandalizi kulingana na mihutasari mipya.

(iii) Kukamilisha maandalizi ya Sera ya Makuzi na Malezi ya Mtoto **(Integrated Early Childhood Care and Development Policy**), na

(iv) Kuongeza idadi ya madarasa ya Elimu ya Maandalizi na kuwahasisha wananchi na sekta binafsi kujenga Skuli za Maandalizi.

(b) **Elimu ya Msingi**

(i) Kuhamasisha wananchi kushiriki katika ujenzi wa skuli mpya na kuongeza idadi ya madarasa katika skuli zilizopo kwenye maeneo yao. Lengo ni kwenda sambamba na ongezeko la watoto wanaohitaji kuandikishwa katika Elimu ya Msingi.

(ii) Kuimarisha ufundishaji katika madarasa ya awali ya Msingi (Std 1 – 4) na kusambaza vitabu na vifaa vyengine vya kufundishia na kujifunzia kwa Elimu ya Msingi kulingana na mihutasati mipya ya masomo, na

(iii) Kuimarisha mazingira ya skuli za Msingi ili ziwe zenye kumjali mtoto (child friendly schools) pamoja na kukamilisha maandalizi ya Sera ya Elimu Mjumuisho.

(c) **Elimu ya Sekondari**

(i) Kuendeleza juhudi za kukarabati Skuli za Sekondari zilizopo, kuongeza idadi ya madarasa na kujenga skuli mpya za Sekondari ili kuongeza ushiriki wa wanafunzi katika ngazi ya Sekondari.

(ii) Kununua vitabu vya masomo ya Hisabati, Jiografia, Elimu ya uraia, Historia, Sayansi, Biashara, Ufundi, Dini, Kiingereza na Kiswahili kwa Elimu ya Sekondari pamoja na vifaa vya maabara na kuvisambaza katika skuli za sekondari.

(iii) Kuimarisha Elimu ya Sayansi na Hisabati kwa kuendesha kambi za Sayansi kwa walimu na wanafunzi katika Vituo vya Walimu na maskulini.

(iv) Kuendelea kuwashajiisha wanafunzi wa kike kupenda masomo ya Sayansi na Hisabati kwa kuwashirikisha kwa wingi katika kambi za Sayansi na kufungua madarasa zaidi ya watoto wa kike.

(v) Kuimarisha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano na ufundishaji wa somo la kompyuta katika skuli kwa kuzipatia kompyuta. Aidha, tovuti ya Wizara itaanzishwa ili kuhifadhi taarifa muhimu na kuzisambaza kwa wadau mbali mbali wa elimu.

(vi) Kuimarisha uendeshaji wa masuala ya elimu katika ngazi mbali mbali kwa kutoa mafunzo kwa walimu wakuu, maafisa wa elimu wa wilaya, mikoa, idara pamoja na kuendelea kufanya ukaguzi na

kutoa ushauri kwa walimu juu ya mbinu bora za ufundishaji madarasani.

(vii) Kujenga skuli mpya 21 za sekondari Unguja na Pemba. Skuli hizo zitajengwa katika vijiji vya Muanda, Matemwe, Chaani, Dole, Uzini, Paje (Mtule), Tunguu, Dimani, Kiembesamaki, Kibuteni, Mpendae kwa Unguja na Pandani, Chwaka Tumbe, Konde, Wawi, Kiwani, Mauani, Ngwachani, Shamiani, Utaani na Mkanyageni.

(viii) Kujenga nyumba 41 za waalimu Unguja na Pemba. Nyumba hizo zitajengwa kwa mpango ufuatao:-

- Kibuteni - 7
- Muanda - 3
- Uzini - 3
- Paje (Mtule) - 3
- Mkanyageni - 7
- Pandani - 3
- Chwaka Tumbe - 3
- Kiwani - 3
- Wawi - 3
- Utaani - 3
- Matemwe - 3

(ix) Kujenga Chuo cha Ualimu, Mchangamdogo Pemba pamoja na nyumba 3 za Walimu.

(x) Kuzifanyia ukarabati mkubwa skuli sita za sekondari skuli hizo ni Uweleni, Utaani na Fidel Castro kwa Pemba na Forodhani, Tumekuja na Hamamni Unguja.

(d) **Elimu Mbadala na Elimu ya Watu Wazima**

(i) Kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Elimu Mbadala cha Wingwi Micheweni na kuanzisha vituo vya Elimu Mbadala katika Mikoa mengine ya Unguja na Pemba.

(ii) Kufanya mapitio ya mihutasari na vitabu vya Elimu Mbadala na kutayarisha mihutasari na vitabu vipya kulingana na Sera Mpya ya Elimu.

(iii) Kuendeleza mafunzo kwa walimu wa Elimu Mbadala na Elimu ya Watu Wazima, kuwahamasisha vijana kujiunga na madarasa ya

Elimu Mbadala na kuanzisha elimu endelevu (Continuing Education) kwa watu wazima.

(e) **Kuimarisha Huduma za Maktaba:**

(i) Kuandaa Sera ya Maktaba Zanzibar.

(ii) Kujenga Maktaba Kuu mpya Pemba na kuimarisha Maktaba za Wilaya, vituo vya Walimu na za skuli.

(iii) Kuendeleza mafunzo ya Ukutubi, kuongeza idadi ya vitabu kwa rika mbali mbali katika maktaba zote.

(iv) Kuhamasisha wananchi kupenda kutumia maktaba na kuendeleza matumizi ya **"Mobile Libraries"** kwa Skuli za Vijijini zisizokuwa na maktaba.

(f) **Kuendeleza na kuimarisha fursa za Elimu ya Juu:**

(i) Kukamilisha ujenzi wa majengo mapya ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) huko Tunguu.

(ii) Kuimarisha Elimu ya Sayansi na Teknolojia ya kisasa katika vyuo vikuu, sambamba na upatikanaji wa Wakufunzi katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA).

(iii) Kuwaendeleza wakufunzi waliopo.

(iv) Kuanzisha Diploma ya Sayansi kwa Walimu na Diploma ya Uongozi.

(v) Kuendeleza mazingiza ya kuwahamasisha wawekezaji na sekta binafsi kuendelea kuwekeza katika elimu ya juu.

(g) **Kuimarisha Mafunzo ya Ualimu**

(i) Kuandaa Sera ya Mafunzo ya Ualimu Kazini na kuendelea kutoa mafunzo kazini kwa walimu kuhusiana na masomo wanayofundisha na mbinu bora za kufundishia masomo hayo.

(ii) Kupitia mitaala ya Diploma ya Ualimu Msingi, Sekondari, Lugha na Dini na Kiarabu na kuifanyia marekebisho na kuanza kutoa mafunzo ya ualimu kwa Walimu wa Skuli za Maandalizi.

(iii) Kuendelea kutoa mafunzo ya ualimu katika Vyuo vya Ualimu na kuendeleza mafunzo ya ualimu kwa walimu wasiosomea kwa njia ya Elimu Masafa.

(iv) Kuendelea kutoa mafunzo kwa Walimu wa Sayansi na Hisabati kupitia Mradi wa Teacher Advancement Programme (TAP) katika vituo vyote vya Walimu na kuendeleza mafunzo ya kompyuta kwa Walimu 170.

(h) **Kuimarisha Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Amali:**

(i) Kujenga Ofisi ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali na kuimarisha matumizi ya teknolojia ya kisasa katika elimu.

(ii) Kuimarisha Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia kwa kuifanyia matengenezo makubwa na kuongeza madarasa pamoja na kuanza kutekeleza mpango wa utekelezaji wa Taasisi wa miaka mitano.

(iii) Kununua vifaa vya kisasa vya kufundishia na kujifunzia kwa masomo ya Ufundi katika Taasisi ya Sayansi na Teknolojia na Skuli za Ufundi za Mikunguni na Kengeja.

(iv) Kupanua na kuimarisha Skuli ya Ufundi Kengeja kwa kuyafanyia matengenezo majengo yaliyopo, na

(v) Kujenga vituo vipya vya Mafunzo ya Amali katika Mikoa ya Kusini Unguja, Kaskazini Pemba na Mjini Magharibi.

(i) **Kuhifadhi Kumbukumbu za Kihistoria na Mambo ya kale:**

(i) Kuandaa mpango wa miaka mitano (Master Plan) wa Uhifadhi wa Mambo ya Kale, uanzishaji wa Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu za Kale na vituo vya kuhifadhi kumbukumbu (Records Centres) katika kila Mkoa.

(ii) Kuendeleza matengenezo ya Makumbusho ya Mnazi Mmoja, Beit – Ajab, jengo la Kale la Mtoni na Makumbusho ya Kasri Forodhani.

(iii) Kuendelea kukusanya kumbukumbu na nyaraka kutoka ofisi za Serikali na kuzihifadhi kumbukumbu hizo kwa kutumia kompyuta.

(iv) Kuendelea kufanya tafiti za kiakiolojia na hifadhi za Urithi katika Mapango ya kale na Baharini na kuanzisha Kituo cha Uhifadhi wa vitu vya baharini

(v) Kukamilisha upimaji wa maeneo ya Kihistoria na kuyapatia hati miliki.

**Afya**

150. Huduma bora za afya kwa wananchi wote bila ya ubaguzi ni miongoni mwa malengo makuu ya Mapinduzi ya Zanzibar ya tarehe 12, Januari1964.

151. Ili kuendeleza uimarishaji wa sekta ya afya kwa maendeleo na ustawi wa wananchi, katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2010-2015), Serikali ya Mapinduzi Zanzibar chini ya uongozi wa CCM itatekeleza hatua zifuatazo:-

(a) Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Afya na ushirikishwaji wa wananchi na sekta binafsi katika kuchangia maendeleo ya afya, kwa kuzingatia malengo ya Milenia, Dira ya 2020 na MKUZA.

(b) Kuendelea kuimarisha huduma za Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja, ili ifikie hadhi na kiwango cha Hospitali ya Rufaa, Hospitali ya Abdalla Mzee na Wete Pemba zifikie hadhi na kiwango cha Hospitali za Mkoa na **"Cottage Hospital"** ya Michweni na Vitongoji Pemba na Makunduchi na Kivunge Unguja, zifikie hadhi na kiwango cha Hospitali za Wilaya.

(c) Kuendelea kuimarisha huduma za kinga na tiba katika hospitali na vituo vya afya na kuendeleza elimu ya afya kwa wananchi ili kudhibiti maradhi hasa yale ya kuambukiza.

(d) Kuendeleza mapambano dhidi ya malaria, **UKIMWI** pamoja na maradhi mengine ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza.

(e) Kuendeleza huduma za tiba asili katika sehemu zote za Unguja na Pemba.

(f) Kuendelea kukiimarisha Chuo cha Taaluma za Sayansi ya Afya pamoja na watumishi wa sekta ya afya kwa kuwapatia mafunzo ya ndani na nje ya nchi.

**Maji**

152. Maji ni uhai, hasa maji safi na salama**.** Serikali ya Mapinduzi Zanzibar chini ya uongozi wa CCM imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya usambazaji maji mijini na vijijini.

153. Ili kuendeleza kazi ya usambazaji wa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi, CCM katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2010-2015) itahakikisha kuwa, SMZ inatekeleza yafuatayo:-

(a) Kufanya mapitio ya Sera na Sheria ya Maji ili kuzihuwisha kwa kuzingatia haja na umuhimu wa usimamizi na udhibiti wa maji machafu, ambayo ni matokeo ya matumizi ya maji safi pamoja na hifadhi ya mazingira.

(b) Kukamilisha Awamu ya Pili ya Mradi wa usambazaji maji safi na salama katika mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

(c) Kuendelea kusambaza huduma ya maji safi na salama kutoka asilimia 75 mwaka 2010 hadi asilimia 95 mwaka 2015 mjini na kusimamia huduma hiyo kutoka asilimia 60 mwaka 2010 hadi kufikia asilimia 80 mwaka 2015 vijijini kupitia mradi mkubwa wa maji unaofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB) ambao utajenga miundombinu ya maji kwa miji mitatu ya Pemna (Chake-Chake, Wete na Mkoani) pamoja na maeneo ya vijiji ambavyo kwa upande wa Unguja ni Nungwi, Matemwe, Machui na Dunga/Tunguu. Maeneo ya Vijiji vya Pemba ni Mizingani, Wambaa, Vitongoji, Ndagoni na Kambini-Mchangamdogo. Aidha, Serikali itaendelea kupeleka maji katika maeneo ambayo hayajafikiwa na miradi mikubwa iliyojengwa.

(d) Kuendelea kuhamasisha wananchi ili kukuza kiwango cha uelewa na mwamko wao katika kuchangia huduma za maji ili ziwe endelevu na kutoa kipaumbele katika kulinda, kuhifadhi na kutunza rasilimali maji hasa katika vyanzo na makinga-maji (Catchment areas) dhidi ya uvamizi kwa shughuli za ujenzi na kilimo.

(e) Kupunguza kiwango cha upotevu wa maji(Non revenue water) kwa kufunga mita za maji na kuwaelemisha wateja wa maji jinsi ya kutumia maji vizuri ili kuyahifadhi.

(f) Kuandaa Sera ya Usafi wa Mazingira (Sanitation Policy) ili kuweza kudhibiti kwa kiwango kikubwa usafi wa mazingira ikiwemo kusimamia vyema shughuli za maji machafu.

## Makazi

154. Kuwapatia wananchi maakazi na nyumba bora ni miongoni mwa malengo ya Mapinduzi matukufu ya tarehe 12 Januari, 1964. SMZ chini ya uongozi wa ASP na sasa CCM imefanya juhudi kubwa kuendeleza ujenzi wa nyumba bora kwa ajili ya makaazi ya wananchi Unguja na Pemba.

155. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2010-2015) CCM itaendeleza juhudi za kuimarisha makaazi ya wananchi na kuhakikisha kwamba, SMZ inatekeleza yafuatayo:-

(a) Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Nyumba na kuandaa Sheria ya **"Condominium"** ili kuwawezesha wananchi waliopangishwa katika nyumba za maendeleo mijini na vijijini kuuziwa sehemu ya majengo hayo (**fleti**).

(b) Kuandaa taratibu za kuwashirikisha wananchi wanaoishi katika Nyumba za Maendeleo mijini na Vijijini, kuchangia gharama za matengenezo na utunzaji wa nyumba hizo.

(c) Kuanzisha maeneo maalumu ya ujenzi wa nyumba za ghorofa hususan mijini, ambako idadi ya wakaazi na tatizo la uhaba wa ardhi ni kubwa zaidi.

(d) Kukamilisha ujenzi wa Nyumba moja ya Maendeleo huko Bambi.

## Uendelezaji wa Mamlaka ya Mji Mkongwe

156. Mji Mkongwe wa Zanzibar ni hazina kubwa na kivutio cha historia ya Zanzibar. Mji Mkongwe pia ni **Urithi wa Kimataifa,** ambao unapaswa kulindwa, kuhifadhiwa na kutumika kama kivutio cha utalii. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2010-2015), CCM itaielekeza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kusimamia utekelezaji wa sheria ya Mamlaka ya Mji Mkongwe na kuimarisha kitengo cha sheria, ili kutoa ushauri kwa wananachi na wakaazi wa Mji Mkongwe.

(b) Kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Mamlaka ya Mji Mkongwe kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi na mafunzo ndani ya kazi.

(c) Kuandaa Mpango wa Matumizi Endelevu ya Eneo la Mji Mkongwe na kuimarisha mashirikiano na Mamlaka nyingine za Miji iliyoko katika orodha ya **UNESCO** na Urithi wa Kimatifa.

(d) Kuhamasisha ukarabati wa majengo yanayomikiwa na watu binafsi na Taasisi za Serikali na kupunguza wingi wa majengo yaliyo katika hali mbaya.

(e) Kujenga ukingo wa ukuta wa barabara ya Mizingani, ili kuzuia athari za mmong'onyoko wa ardhi unaosababishwa na bahari.

(d) Kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Matumizi ya Magari na Vyombo vya Moto **(Traffic Plan)** ndani ya eneo la Mji Mkongwe.

## Maeneo Mengine ya Kipaumbele

## Utamaduni na Michezo

157. Utamaduni ni nyenzo muhimu katika kulinda na kudumisha mila na silka njema za jamii. Michezo huimarisha afya na kujenga udugu na mashirikiano miongoni mwa wananchi na mataifa mbalimbali.

158. Ili kuiendeleza zaidi sekta ya Utamaduni na Michezo, katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2010-2015), CCM itaielekeza SMZ kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kusimamia utekelezaji wa Sera na Sheria za Michezo na Utamaduni na kuhimiza matumizi ya sanaa katika kuhamasisha na kuelimisha jamii kuhusu masuala mbalimbali ya maendeleo na kampeni za kitaifa.

(b) Kuandaa Sera ya Utamaduni na Michezo na kuendeleza utalii wa kiutamaduni na wa kimaumbile.

(c) Kujenga kiwanja cha kisasa cha michezo ya ndani katika eneo la kiwanja cha Amaani na kukamilisha Ujenzi wa Kituo cha Michezo Dole (Akademia).

(d) Kuanza maandalizi ya ujenzi wa uwanja mpya wa kisasa wa michezo ambao pia utatumika kwa maadhimisho ya sherehe mbalimbali za kitaifa.

(e) Kuanza matengenezo ya kuboresha uwanja wa Gombani Pemba.

(f) Kuendeleza na kuimarisha vipaji vya wanamichezo kwa kuwapatia fursa za kushiriki katika mashindano ya kitaifa na kimataifa kwa njia ya ziara za kimichezo nje ya nchi na mafunzo.

(g) Kuendeleza juhudi za kulinda, kuhifadhi na kudumisha mila, silka na maadili mema ya Wazanzibari.

**Vyombo vya Habari**

159. Vyombo vya Habari vinalo jukumu kubwa la kuburudisha, kuelimisha na kuhamasisha jamii juu ya masuala mbalimbali ya maendeleo, demokrasia na Utawala Bora. Kwa kutambua wajibu huo wa vyombo vya habari, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar chini ya uongozi wa CCM, inao wajibu wa kusimamia na kuendeleza uhuru wa Vyombo vya Habari.

160. Ili kukuza na kuendeleza Uhuru wa Vyombo vya Habari, katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2010-2015), CCM itahakikisha kuwa, hatua zifuatazo zinatekelezwa na Serikali:-

(a) Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Habari na kuendeleza Uhuru wa Vyombo vya Habari.

(b) Kusimamia utekelezaji wa Miongozo, Kanuni na Sheria ya Vyombo vya Habari ili kuongeza ufasini na kasi ya mageuzi ya Utangazaji.

(c) Kuendeleza mafunzo kwa watendaji wa Vyombo vya Habari na Utangazaji, ili kujenga weledi na vipaji vyao.

(d) Kuviimarisha Vyombo vya Habari ikiwemo TVZ na STZ, kwa kuvipatia vifaa na mitambo ya kisasa ili viweze kurusha matangazo yake kwa ufanisi, kuonekana na kusikika katika sehemu mbalimbali ndani na nje ya Zanzibar na Tanzania kwa jumla.

(e) Kuendelea kukiimarisha Chuo cha Uandishi wa Habari ili kiwe chombo cha kujenga na kutoa mwelekeo wa matumizi sahihi ya lugha ya Kiswahili kwa Vyombo vya Habari.

(f) Kusimamia na kudhibiti uingizaji wa vifaa vya utangazaji na kuhakikisha kwamba, Zanzibar haigeuzwi kuwa jaa la kutupia vifaa visivyotumika vya televisheni, redio na utangazaji kwa ujumla.

(g) Kukiimarisha kiwanda cha uchapaji kwa kukifanyia matengenezo makubwa na kukipatia mitambo mipya ya uchapaji na vifaa vya kisasa.

## Majanga na Huduma za Uokoaji

161. Huduma za uokoaji ni muhimu kwa jamii hasa pale yanapozuka majanga ya kimaumbile na yale yanayosababishwa na binadamu. Ili kuimarisha huduma za Uokoaji, katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2010-2015), CCM itahakikisha kuwa Serikali inatekeleza yafuatayo:-

    (a) Kuimarisha uwezo wa Kikosi Cha Zimamoto na Uokozi (KZU) kwa mafunzo na vifaa vya kisasa na kuanzisha vituo vipya katika kila wilaya.

    (b) Kukiimarisha Kitengo cha Taifa cha Maafa na Kamati za Maafa za Mikoa na Wilaya kwa kuzipatia mafunzo na miongozo kuhusu kazi na wajibu wao.

    (c) Kuanzisha kikosi maalum cha uokoaji wakati wa majanga ya baharini, ili kutoa huduma za uokoaji wa maisha na mali za wananchi wanaopatwa na ajali wakiwa baharini.

## MADAWA YA KULEVYA

162. Madawa ya kulevya pamoja na maambukizi ya VVU ni miongoni mwa changamoto kubwa zinazowakabili vijana wa Zanzibar. Madawa ya kulevya huathiri afya za watumiaji ambao wengi wao ni vijana na kudhoofisha nguvu kazi na uchumi wa Taifa letu. Aidha, upo uhusiano mkubwa kati ya matumizi ya madawa hayo na maambukizi ya VVU.

163. Ili kuendeleza mapambano dhidi ya madawa ya kulevya na kudhibiti maambukizi ya VVU, CCM katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2010-2015) itahakikisha kwamba, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inatekeleza hatua zifuatazo:-

    (a) Kuendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Kudhibiti Madawa ya Kulevya.

    (b) Kuendelea kushirikiana na Asasi za kijamii katika kuhamasisha na kuelimisha vijana athari za madawa ya kulevya na kuwashawishi waachane na matumizi ya madawa hayo.

    (c) Kuendelea kuchukua hatua thabiti za kuimarisha ulinzi na udhibiti wa vituo vya kuingilia nchini zikiwemo bandari na viwanja vya ndege.

(d) Kuhamasisha wananchi kushiriki katika ulinzi shirikishi na polisi jamii ili kudhibiti uingizaji, usambazaji na matumizi ya madawa ya kulevya katika maeneo yao.

(e) Kuanzisha Kituo Maalumu cha Kurekebisha Vijana walioathirika na madawa ya kulevya.

**Demokrasi na Utawala Bora**

164. Demokrasi na Utawala Bora ni hatua muhimu katika ujenzi wa jamii yenye umoja, mshikamano, uadilifu na uwajibikaji. Ili kuendeleza ujenzi wa demokrasia na utawala bora katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2010-2015) CCM itaendeleza azma yake ya kuimarisha na kukuza demokrasia na utawala bora na kuhakikisha kwamba SMZ inatekeleza yafuatayo:-

(a) Kusimamia utekelezaji wa kazi na majukumu ya Serikali kwa kuzingatia misingi ya demokrasia na utawala bora kama ilivyoainishwa katika Katiba ya nchi, kuimarisha uwazi na uwajibikaji na kulifanya suala la maadili kuwa agenda ya kitaifa.

(b) Kuendeleza kazi ya utekelezaji wa mkakati wa elimu ya uraia, ikiwemo elimu ya demokrasia, haki za binadamu na utawala bora kwa viongozi, watendaji na wananchi kwa jumla.

(c) Kukamilisha kazi ya kuandaa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa na kusimamia utekelezaji wake, ili kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa.

(d) Kuimarisha ofisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka Zanzibar na kukamilisha hatua za wanasheria wa ofisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka kuendesha mashtaka katika ngazi zote za mahakama.

(e) Kukiimarisha kitengo cha kupokea malalamiko kwa kuyapokea, kuyafanyia kazi na kuyapatia ufumbuzi wa haraka.

(f) Kuimarisha ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa kuwapatia watendaji wake elimu ya kada mpya za ukaguzi, ukiwemo Ukaguzi wa Thamani (Value for Money Auditing), Ukaguzi wa Komputa (Computerize Auditing) na Ukaguzi wa Mazingira (Enviromental Auditing).

(g) Kuimarisha Mahakama kwa kujenga majengo mapya, nyumba za Mahakimu katika vituo vya kazi Unguja na Pemba, kuzipatia vifaa vya kisasa na kufanya marekebisho ya sheria na kanuni za utendaji kazi wa Mahakama.

(h) Kuanzisha Mahakama ya Biashara Zanzibar.

(i) Kufanyiwa mapitio ya Sheria ya Asasi za Wananchi (NGO's) na kuweka mfumo wa kisasa utakaorahisisha usajili wa Jumuiya hizo.

(j) Kukamilisha ujenzi wa ukumbi mpya wa Baraza la Wawakilishi.

**Serikali za Mitaa**

165. Serikali za Mitaa ni chombo muhimu cha kuwawezesha wananchi kushiriki katika Utawala wa nchi yao. Serikali za Mitaa ni kichocheo cha maendeleo na ustawi wa wananchi, ujenzi wa domokrasi na utawala bora. Ili kuziendeleza Serikali za Mitaa katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2010-2015) CCM itahakikisha kwamba, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inatekeleza hatua zifuatazo:-

(a) Kuifanyia mapitio Sheria ya Serikali za Mitaa na Mamlaka ya Tawala za Mikoa na Miji na kuandaa Mpango wa Mageuzi ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ili kuimarisha uwajibikaji na ufanisi.

(b) Kuendelea kuziimarisha Serikali za Mitaa kwa kuzipatia ruzuku, wataalamu wa fani mbalimbali, vifaa vya kisasa na vitendea kazi, ili kuendeleza utendaji wake wa kazi na huduma bora kwa wananchi.

(c) Kuimarisha mahusiano kati ya wananchi na Madiwani na watendaji wa Halmashauri za Wilaya, Mabaraza ya Miji na Baraza la Manispaa kwa kuwapatia mafunzo na miongozo mbalimbali Madiwani ili kuimarisha uwajibikaji wao kwa wananchi.

(d) Kuwahamasisha wananchi kuunda Kamati za Maendeleo katika maeneo yao, ili kusukuma kasi ya maendeleo yao kiuchumi na kijamii na kudhibiti aina zote za uhalifu ukiwemo wizi wa mazao na mifugo na kupiga vita vitendo vya ukahaba na madawa ya kulevya kupitia mfumo wa Ulinzi Shirikishi na Polisi Jamii.

(e) Kuzihimiza Serikali za Mitaa kusimamia suala la usafi wa miji, hifadhi ya mazingira na kuhakikisha kuwa kila mwenye uwezo wa kufanya kazi anafanya kazi.

**Vikosi Maalumu vya SMZ**

166. Vikosi Maalumu vya SMZ kama vilivyoainishwa katika Katiba ya Zanzibar, kwa ujumla wake ni vyombo muhimu vya utekelezaji wa Sera za CCM kuhusu Ulinzi

na Usalama na hususan dhana ya Ulinzi wa Umma, ambao unawashikisha wananchi wote.

167. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo(2010-2015), Serikali ya Mapinduzi Zanzibar chini ya uongozi wa CCM itaendelea kuviimarisha Vikosi Maalumu vya SMZ, na kutekeleza hatua zifuatazo:-

(a) Kuvijengea uwezo na mazingira mazuri ya kazi kwa kuvipatia mafunzo na vifaa vya kisasa ili viweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

(b) Kuendeleza juhudi za kukiimarisha Kikosi Maalumu cha Kuzuia Magendo (KMKM) kwa kukipatia mafunzo na zana za kisasa, ili kuongeza uwezo na mbinu za kuweza kukabiliana na kudhibiti aina mpya za uhalifu unaoanza kujitokeza katika maeneo ya ukanda wa pwani, ukiwemo uharamia na utekaji nyara wa vyombo wa baharini.

(c) Kuendeleza juhudi za kuliimarisha Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) na kuimarisha miundombinu ya kambi zake, ili kuwavutia vijana wengi zaidi na kuwa vituo vya kuwajenga vijana katika uzalendo, ukakamavu, usawa na umoja wa kitaifa na kuwaandaa katika stadi mbalimbali za maisha.

(d) Kukiimarisha zaidi Kikosi cha Valantia (KVZ) kwa kukamilisha ujenzi wa majengo yake ya Makao Makuu huko Mtoni na maeneo mengine ya mikoa na wilaya, na kukiwezesha kutekeleza jukumu lake la msingi la kuendeleza mafunzo ya **Ulinzi wa Umma** miongoni mwa wananchi hasa vijana (ambao ni nguvu kubwa), ili kushiriki katika ulinzi wa maeneo yao wanayoishi chini ya mfumo wa Ulinzi Shirikishi na Polisi Jamii.

(e) Kuendeleza na kudumisha mashirikiano mema yaliyopo baina ya Vikosi vya SMZ na vyombo vya Ulinzi na Usalama nchini.

**Kuwaunganisha Wananchi wa Zanzibar**

168. Hoja ya kuwaunganisha wananchi wa Zanzibar, kimsingi inatokana na sera za CCM za kujenga Umoja wa taifa, Amani na Utulivu. Mazingira ya amani na utulivu ndio zana ya kwanza inayohitajika ili kufanikisha utekelezaji wa Ilani hii ya CCM ya mwaka 2010-2015 na kufikia azma ya Chama ya kujenga msingi wa uchumi wa kisasa wa taifa linalojitegemea. Nchi yenye fujo na vurugu haiwezi kujenga uchumi imara na kuwaletea maendeleo ya maana wananchi wake. Hakuna mwekezaji atakayekubali kuja kuwekeza na wananchi hawatapata fursa ya kujiendeleza kiuchumi na kupambana na umasikini.

169. Hii ndio sababu siku zote CCM imekuwa ya kwanza kutetea na kusimamia amani, umoja na utulivu miongoni mwa wananchi. Kufikiwa kwa Muafaka wa

kisiasa wa mwaka 1999, 2001 na Maridhiano ya kisiasa juu ya mustakabali wa Zanzibar ya Novemba 2009, ni uthibitisho thabiti wa ukweli huu.

170. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2010-2015), CCM itaendelea kuimarisha jitihada za kusimamia amani, utulivu na kuwaunganisha Wananchi wa Zanzibar na Tanzania kwa jumla na kuhakikisha kuwa SMZ inatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuendeleza na kuimarisha amani, utulivu na mshikamano wa kitaifa miongoni mwa Wazanzibari na Watanzania kwa jumla.

(b) Kuendelea kupiga vita, kudhibiti na kutoruhusu vitendo vya ubaguzi wa aina yoyote ile kujitokeza katika sehemu za utoaji wa huduma au fursa mbalimbali za kiuchumi na kijamii miongoni mwa wananchi.

(c) Kuendeleza umoja na mshikamano miongoni mwa wananchi kwa kuwapatia elimu ya uraia na kuwajengea mazingira ya kuaminiana, kuvumiliana na kushirikiana kama dhana na silaha muhimu ya kuharakisha maendeleo yao, kuboresha huduma za kijamii na kupambana na umasikini.

## Kuyaendeleza Makundi Mbalimbali

### Watoto

171. Watoto ndio chanzo cha rasilimali watu na mrithi wa taifa la kesho. CCM inaamini kuwa, watoto wanayo haki ya kuishi, kulindwa, kuendelezwa kwa kupewa elimu na afya bora na kutobaguliwa kwa mujibu wa Katiba na Sheria za nchi.

172. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2010-2015) CCM itaendelea kuimarisha haki na maendeleo ya watoto na kuhakikisha kwamba, SMZ inatekeleza hatua zifuatazo:-

(a) Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Uhai, Hifadhi na Maendeleo ya Watoto, kupiga vita ajira kwa watoto na kusimamia utekelezaji wa sheria na mikataba ya Kimataifa inayohusu haki, usawa na hifadhi ya watoto.

(b) Kupitisha Sheria ya Mtoto na kusimamia utekelezaji wake.

(c) Kufuatilia na kusukuma kasi ya upatikanaji wa huduma za tiba, kinga na afya ya mama na mtoto katika Hospitali na vituo vyote vya afya mijini na vijijini kwa kiwango na ubora unaokubalika.

(d) Kusimamia na kuratibu ubora wa huduma zinazotolewa na Mashirika ya hiari na yasiyokuwa ya Serikali yanayojishughulisha na huduma zinazomgusa mtoto, vikiwemo vituo vya malezi na Skuli za awali.

(e) Kukamilisha ujenzi wa Nyumba ya Watoto yatima – Mazizini Unguja

(f) Kujenga Nyumba ya Watoto yatima Pemba.

**Vijana**

173. Vijana walioandaliwa vyema na kujipanga vizuri wanao mchango mkubwa katika kukuza uchumi na maendeleo ya jamii. Ukosefu wa ajira, kukosa ujuzi na maarifa ya kisasa pamoja na mitaji ni miongoni mwa changamoto kubwa zinazowakabili vijana wengi mijini na vijijini na kuwafanya washindwe kujiendeleza na kutekeleza wajibu wao wa kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa uchumi wa kisasa.

174. Katika kipindi cha mwaka 2010-2015, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa CCM itaendeleza juhudi za kuzipatia ufumbuzi changamoto za vijana na kahakikisha kuwa, SMZ inachukuwa hatua zifuatazo:-

(a) Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Vijana, Sera ya Ajira na Sheria ya Kazi na kuendelea kuwahamasisha vijana ili kuunda vikundi vya uzalishaji mali.

(b) Kuimarisha mashirikiano na Asasi zisizokuwa za Serikali (NGOs) zenye kushughukia maendeleo ya Vijana ili kuanzisha vituo vya ujasirimali kwa vijana, kuwaendeleza na kuwapatia elimu ya stadi mbalimbali zitakazowawezesha kujiajiri wenyewe.

(c) Kuanzisha Mfuko Maalumu wa vijana utakaotoa mikopo nafuu ili kuwasaidia kujiendeleza kwenye shughuli mbalimbali za kiuchumi.

(d) Kukamilisha uanzishaji wa Baraza la Taifa la Vijana ili kuimarisha ushiriki wa vijana katika ngazi mbalimbali za maamuzi na kupiga vita UKIMWI na kuendeleza mapambano dhidi ya madawa ya kulevya.

**Wanawake**

175. CCM inatambua uwezo na nguvu kubwa ya wanawake katika kusukuma kasi ya maendeleo na kuleta mageuzi ya kiuchumi, kijamii na kisiasa na kwamba: **"Wakiwezeshwa, Wanaweza".**

176. Ili kuendeleza juhudi za kuwawezesha wanawake kiuchumi, kijamii na kisiasa, CCM katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2010-2015) itahakikisha kwamba Serikali inatekeleza yafuatayo:-

(a) Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Hifadhi na Maendeleo ya Wanawake na kuhakikisha kwamba, haki za wanawake zinaimarishwa na kulindwa kwa mujibu wa Katiba na Sheria za nchi.

(b) Kuendelea kupiga vita mila na desturi zinazowabagua na kuwadhalilisha wanawake na kusimamia utekelezaji wa sheria na mikataba mbalimbali ya Kimatifa inayohusu haki na ustawi wa jamii.

(c) Kuendeleza juhudi za kuwahamasisha wanawake kujiendeleza kielimu na kutoa kipaumbele cha elimu kwa watoto wa kike.

(d) Kuendeleza juhudi za kuwapatia mafunzo na elimu ya uraia ili kujenga uelewa wao na nguvu za kutetea haki zao na kushiriki kikamilifu katika shughuli za kijamii.

(e) Kuimarisha uwezo wa Mifuko mbalimbali ya Kuwawezesha Kiuchumi Wanawake na kujenga mazingira yatakayowawezesha kuanzisha Benki ya Wanawake.

**Wazee**

177. Wazee ni hazina na chemchem ya busara katika jamii. Wazee ndio chimbuko la familia na wametoa mchango mkubwa katika ujenzi na maendeleo ya taifa letu. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2010-2015) CCM itahakikisha kwamba, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inaendelea kuchukua hatua thabiti za kuwatunza na kuendeleza ustawi wa maisha yao na kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kuendeleza juhudi za kuwapatia hifadhi ya makazi, huduma za afya na misaada ya kijamii kwa wazee wasiojiweza pamoja na kuzifanyia matengenezo ya mara kwa mara nyumba za wazee zilizopo Sebleni Unguja na Limbani Pemba.

(b) Kuihamasisha jamii kuendeleza utamaduni wa kuwaheshimu, kuwaenzi na kuwatunza wazee wetu pamoja na kuwapa nafasi wanayostahiki katika jamii.

**Walemavu**

178. CCM inaamini katika usawa wa binadamu na kwamba, watu wenye ulemavu wanayo haki kwa mujibu wa Katiba ya kutambuliwa utu wao, kuendelezwa, kuheshimiwa na kutokubaguliwa. Aidha, Chama kinatambua uwezo mkubwa walionao watu wenye ulemavu katika kujiendeleza na kuchangia katika uchumi na maendeleo ya taifa letu.

179. Ili kuwaendeleza watu wenye ulemavu, katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2010-2015) CCM itahakikisha kuwa, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inaendeleza jitihada za kuimarisha hali ya ustawi wa watu wenye ulemavu na kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Watu wenye Ulemavu na kuendelea kuwapatia huduma zote za msingi hasa elimu, afya pamoja na vifaa muhimu vinavyoendana na mahitaji yao maalumu.

(b) Kuunga mkono na kushirikiana kwa karibu na Jumuiya ya Watu wenye Ulemavu katika kuhamasisha na kuelimisha jamii iondokane na mtizamo hasi dhidi ya watu wenye ulemavu.

(c) Kuendelea kuwapatia watu wenye ulemavu fursa za mafunzo ya stadi mbalimbli za ufundi, misaada, mikopo ya fedha na vifaa vya kisasa.

**Wafanya Kazi**

180. Wafanyakazi ni rasilimali watu na ndio msingi wa mageuzi yote ya kiuchumi na kijamii. Wafanyakazi huchangia katika kukuza uchumi na maendeleo ya nchi yetu. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2010-2015) CCM itahakikisha kuwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inaimarisha jitihada zake katika kuwaendeleza wafanyakazi na kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kuandaa Sera ya Hifadhi ya Jamii na kufanya mapitio ya Sheria za Kazi.

(b) Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Ajira, Mpango wa Kuzalisha Ajira, Sheria za Kazi na Kanuni za Utumishi, ili kulinda na kuendeleza haki na wajibu wa wafanya kazi.

(c) Kuimarisha mashirikiano kati ya Serikali na wafanyakazi kupitia chombo chao "Shirikisho la Vyama Huru vya Wafanyakazi" kwa lengo kukuza mahusiano mema na kujenga "Utatu".

(d) Kuendelea kuimarisha mazingira bora ya kazi na maslahi ya wafanyakazi kwa kadri hali ya uchumi wa Zanzibar utakavyoimarika.

## SURA YA NANE

## MAENEO MENGINE MUHIMU

### Kuimarisha Muungano

181. Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ambao ni wa kipekee katika Bara la Afrika, sasa umefikisha umri wa miaka 46, tangu kuasisiwa kwake hapo tarehe 26, Aprili 1964. Katika kipindi hiki Muungano wetu umezidi kuimarika na kupiga hatua kubwa katika nyanja za kisiasa, kiuchumi na kijamii. Sambamba na mafanikio hayo, zipo changamoto nyingi ambazo bado zinahitajika kufanyiwa kazi.

182. Hii ni pamoja na kujenga mazingira endelevu na kuimarisha fursa za kiuchumi miongoni mwa wananchi wa kila upande, ili waone na kuamini kwamba, Muungano wa Tanganyika na Zanzibar sio tu ni ngao madhubuti ya Umoja, Amani na Mshikamano wao, bali pia ni daraja lisilotetereka la kuwafikisha katika azma yao ya kuondokana na umaskini na kuharakisha maendeleo yao na Taifa kwa jumla. Hii ndio changamoto kubwa inayo ukabili Muungano wetu, ambayo Serikali zetu zinapaswa kuivalia njuga.

183. Katika kipindi cha Ilani hii, Chama kitazielekeza Serikali zake kuimarisha zaidi Muungano kwa faida ya pande zote mbili kwa kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kukamilisha ujenzi wa majengo na taasisi za Muungano ambazo zimeanzishwa Tanzania Zanzibar.

(b) Kuimarisha utendaji wa Kamati ya Pamoja ya kutatua kero za Muungano kwa kuandaa utaratibu madhubuti wa vikao vya Kamati na utekelezaji wa haraka wa maamuzi yanayofikiwa.

(c) Kuboresha uchangiaji na mgawanyo wa mapato ya Muungano.

(d) Kuzifanyia mapitio na uboreshaji Sheria na Kanuni za Fedha zinazotawala ukusanyaji wa mapato chini ya TRA na ZRB upande wa Tanzania Zanzibar kwa lengo la kukuza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato hayo.

(e) Kuboresha Sheria, Kanuni na taratibu za ajira ya watumishi katika Taasisi za Muungano ili utumishi huo uwe na sura muafaka ya ki - Muungano.

(f) Kuimarisha utaratibu wa kuandaa na kutekeleza mikakati na mbinu za pamoja zenye lengo la kuinua uchumi wa pande zote mbili za Muungano.

(h) Kuendeleza miradi ya pamoja ya kiuchumi, miundombinu na ya kijamii iliyokwishaanzishwa ikiwemo ya TASAF, MACEMP n.k.

184. Aidha, CCM inatambua kuwa, Mapinduzi ya Zanzibar ya tarehe 12 Januari 1964, ndilo tukio kubwa na muhimu la kihistoria kwa Visiwa vya Zanzibar lililowakomboa Wazanzibari wote kutoka makucha ya ukoloni na kujenga mazingira muafaka ya Zanzibar huru kuungana na Tanganyika huru na kuunda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani hii, CCM itahakikisha kwamba Serikali zake zinaendelea kuchukua hatua za kuyalinda, kuyaenzi na kuyaendeleza mafanikio yote yaliyopatikana kwa kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kuendelea kuyalinda Mapinduzi hayo ikiwa ndio msingi wa maendeleo kamili, uhuru, haki, usawa wa binadamu na heshima ya kweli kwa Wazanzibari.

(b) Kuendelea kuyalinda kwa nguvu zote na kuchukua hatua za kuyaendeleza mafanikio mbalimbali yaliyoletwa na Mapinduzi hayo, hususan ardhi, huduma za jamii (elimu, afya, maji) pamoja na kupiga vita aina zote za ubaguzi au upendeleo miongoni mwa wananchi.

(c) Kuendelea kuheshimu Haki za Binadamu Demokrasia na Utawala Bora.

## UTAWALA BORA

185. Chama Cha Mapinduzi kinatambua kwa dhati umuhimu wa utawala bora na katika kipindi cha Ilani hii ya 2010-2015, kitaielekeza Serikali kuendelea kudumisha utawala bora nchini kwa kuchukua hatua zifuatazo:-

(a) Kuwahamasisha viongozi wa vyama vya siasa kuendesha shughuli za kisiasa kizalendo, wakizingatia wakati wote kwamba na wao ni wadau wa mstari wa mbele wa maendeleo ya Taifa letu.

(b) Kujenga na kuimarisha zaidi matumizi ya dhana ya utatu baina ya Serikali, mwajiri na wafanyakazi katika kuleta utendaji kazi uliotukuka nchini mwetu.

(c) Kuendelea kuimarisha utoaji wa elimu ya demokrasia katika ngazi zote na kujenga uvumilivu wa kisiasa nchini.

(d) Kuhakikisha kwamba kuna usimamizi madhubuti wa matumizi ya fedha na rasilimali nyingine za umma kwa kusimamia ipasavyo uwajibikaji wa wote wanaohusika. Maadili ya viongozi wa umma yafuatwe kwa ukamilifu.

(e) Kuendesha Serikali kwa kufuata Katiba ya Nchi, Sheria, Kanuni na Taratibu zilizowekwa.

(f) Kutoa mafunzo ya Utawala Bora na Demokarasia.

(g) Kusimamia utekelezaji wa Haki za Binadamu kama zilivyoelezwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Katiba ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Tamko la Haki za Binadamu la Umoja wa Afrika na Tamko la Umoja wa Mataifa.

(h) Kuifanyia marekebisho Sheria ya Manunuzi ya Vifaa kwa kupunguza urasimu ili kuharakisha uamuzi juu ya vitu vinavyotakiwa kununuliwa na kuchochea maendeleo ya nchi.

(i) Kuona kuwa Serikali inateua Watendaji ambao ni wazalendo, waaminifu na waadilifu.

(j) Kuimarisha nidhamu, uwajibikaji na kupiga vita urasimu katika maeneo yote ya uongozi na utendaji Serikalini.

**Sekta ya Sheria**

186. Katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani hii ya 2010-2015, Chama kitaitaka Serikali iendelee kuimarisha Sekta ya Sheria kwa kuchukua hatua zifuatazo:-

(a) Pamoja na kuipongeza Serikali ya Awamu ya Nne kwa kuteua Majaji wengi wakiwemo Wanawake, jitihada hizo za Serikali ziendelee pamoja na kuona kwamba Mahakama zote zinajengewa mazingira yatakayowawezesha kutimiza majukumu yake kwa ufanisi.

(b) Kuhakikisha kuwa wanakuwepo pia wataalamu waliobobea katika Sheria za Mikataba na kwamba wanatumika ipasavyo wakati Serikali inapoandaa mikataba mbalimbali ya kitaifa na kimataifa.

(c) Kuyatafutia ufumbuzi endelevu masuala ya mlundikano wa kesi mahakamani na la msongamano wa wafungwa magerezani.

(d) Kupanua mafunzo ya Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo na kuwapangia kazi ili utoaji wa haki katika ngazi za chini usicheleweshwe.

(e) Kuboresha posho za Wazee wa Mahakama na kuhakikisha kwamba zinatolewa kwa wazee wote kwa wakati unaotakiwa.

(f) Kuzifanyia marekebisho sheria za mirathi na zile zinazoonekana kuwakandamiza wanawake.

(g) Kuanzisha na Kutekeleza Mpango maalum wa kuanzisha Ofisi za Mahakama Kuu katika kila Mkoa ili kusogeza huduma kwa wananchi.

(h) Kukamilisha Mchakato wa kutenganisha shughuli za upelelezi na uendeshaji mashtaka.

(i) Kutekeleza Mpango wa Uboreshaji wa Mfuko wa Sheria hususan ujenzi wa majengo ya Mahakama ya ngazi zote na kuajiri Majaji na Mahakimu wa kutosha. Mfumo wa elektroniki katika kuendesha mashauri na kuhifadhi nyaraka za mashauri utaanzishwa.

(j) Kuweka mfumo wa Kuwasaidia wananchi wasiojiweza kupata msaada wa Kisheria.

(k) Kupeleka huduma za Mahakama karibu na wananchi ikiwa ni pamoja na kujenga masjala ya Mahakama ya Biashara Dodoma.

(l) Kuendelea kuimarisha na kuongeza kasi ya usikilizaji wa migogoro ya nyumba na Ardhi ili kuwezesha wananchi kuendelea na shughuli za uchumi.

(m) Kuyawekea mfumo wa sheria maagizo mbalimbali ambayo hutolewa kama amri halali na viongozi wakuu wa nchi yetu kuhusu maendeleo yetu ili utekelezaji wa maagizo hayo upate nguvu ya sheria.

(n) Kuendelea kupunguza mlundikano wa mahabusu katika magereza.

**Demokrasia na Madaraka ya Umma**

187. Katika jitihada za kukuza na kuendeleza demokrasia nchini na kuimarisha madaraka ya umma, Chama Cha Mapinduzi kitaitaka Serikali kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kuhakikisha kwamba NGOs kutoka nje zinajishughulisha na majukumu ambayo zimeandikishwa kufanya na kwamba hazipati nafasi ya kujiendesha kinyume na makusudi hayo.

(b) Kuendelea kuzijengea uwezo Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kusimamia rasilimali watu na fedha ili zitumike kuharakisha maendeleo ya Wilaya au Manispaa inayohusika.

(c) Kuhimiza utekelezaji wa Sheria ya Ardhi namba 4 na 5 ya mwaka 1999 katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

(d) Kuboresha usimamizi na udhibiti wa fedha katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

188. **Mapambano Dhidi ya Rushwa**

Rushwa ni kikwazo cha maendeleo ya Taifa na utoaji wa haki nchini. Usipodhibitiwa kwa dhati, uovu unaotendwa na watoaji na wapokeaji rushwa unaweza kuenea katika sekta zote za maisha ya jamii na kusababisha mmomonyoko mkubwa wa uwajibikaji na maadili ya uongozi.

189. Ili kukomesha madhara ya rushwa, Chama Cha Mapinduzi katika kipindi hiki cha 2010-2015 kitaitaka Serikali kuimarisha na kuendeleza mapambano dhidi ya rushwa kwa kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kuendelea kuimarisha na kuboresha kwa kiwango kikubwa mfumo wa upelelezi wa makosa, uendeshaji wa kesi na utoaji wa haki mahakamani kwa lengo la kudhoofisha vishawishi vya rushwa.

(b) Kuendesha mafunzo ya elimu ya uraia kwa wananchi ili kuwahamasisha wajue madhara ya rushwa na kuwataka waichukie rushwa katika sura zake zote.

(c) Kutoa mafunzo kwa watumishi wa umma juu ya maadili ya kazi na mbinu za kupambana na rushwa ili waweze kujiepusha na rushwa katika ofisi zote za umma.

(d) Kuendelea kuimarisha uwezo wa vyombo vyote vya dola vinavyopambana na rushwa ili viweze kutoa mchango mkubwa zaidi.

## Ulinzi na Usalama

190. Vyombo vya Ulinzi na Usalama vinavyojumuisha JWTZ, JKT, JKU, Polisi na Magereza ni vyombo vyenye dhima na jukumu kubwa la kulinda uhuru na mipaka ya nchi yetu, usalama wa raia na mali zao. Aidha, vinadumisha mazingira ya amani na utulivu yanayovutia wawekezaji wa ndani na nje na

kuwezesha utekelezaji ulio kamili wa mipango ya maendeleo toka ngazi ya familia hadi Taifa.

191. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita 2005 – 2010, Vyombo hivi vilitekeleza majukumu yake kwa ujasiri, uzalendo na uadilifu wa hali ya juu. Katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani hii ya 2010-2015, Chama Cha Mapinduzi kitazitaka Serikali zetu kulinda mafanikio yaliyopatikana na kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kuendelea kuimarisha na kuboresha zaidi mafunzo ya aina zote ya vyombo vya ulinzi.

(b) Kuwapatia wananchi mafunzo juu ya ulinzi shirikishi ili wawe tayari kujilinda katika maeneo yao.

(c) Ili kukabiliana na tatizo linalowafanya wanajeshi wetu kuishi uraiani, mpango maalumu unaolenga katika kulitatua tatizo hili utaanzishwa.

(d) Halmashauri za Majiji, Manispaa na Miji zitakiwe kuanzisha vikosi vyao rasmi vya usalama wa raia ili kuimarisha ulinzi katika maeneo hayo.

(e) Kujenga vituo vya Polisi katika kila Tarafa nchini.

(f) Kuimarisha shughuli za uzalishaji mali na wa mbegu bora za mazao na mifugo katika maeneo ya Magereza na JKT.

(g) Kuendelea na mpango wa kuimarisha na kupanua mafunzo ya JKT na JKU kwa vijana wa mujibu wa sheria ili kuwapatia fursa ya kujifunza juu ya ulinzi, kujenga Taifa, uzalendo na umoja wa kitaifa.

## Hifadhi ya Mazingira

192. Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili Alhaj Ali Hassan Mwinyi aliwahi kusema, "**Umaskini na uharibifu wa mazingira ni watoto pacha na mama yao ni ujinga**" Tamko hilo linaashiria siyo tu umuhimu wa jukumu la kuhifadhi mazingira ya hewa, maji, udongo na uoto wa asili wa nchi yetu bali pia hatari zinazosababishwa na uchafuzi wa mazingira tunamoishi. Hatari kubwa zaidi ni umaskini wa wananchi.

193. Katika kipindi cha miaka ya 2010-2015, Chama Cha Mapinduzi kitaitaka Serikali iendelee kufanya yafuatayo ili kuhakikisha kazi iliyoanza ya hifadhi ya mazigira inakuwa endelevu:-

(a) Kuimarisha zoezi la kitaifa la kupanda miti na miti ya asili kila mwaka katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili hiyo. Viongozi wa Vitongoji, Mitaa, Vijiji na Kata watakiwe kukagua mara kwa mara miti iliyopandwa ili kuhakikisha inakua. Aidha, miti ipandwe katika maeneo ya shule, barabara, zahanati ya kijiji, Kituo cha Afya na makazi ya watu. Wakuu wa maeneo hayo wahakikishe lengo la kupanda miti linafanikiwa.

(b) Serikali za Vijiji na Halmashauri za Wilaya na Manispaa zitunge sheria ndogo za hifadhi ya misitu.

(c) Kusimamia utekelezaji wa sheria ya hifadhi ya mazingira katika vyanzo vya maji na kusimamia utekelezaji wa mkakati wa usafi katika fukwe.

(d) Serikali ichukue hatua ya kuandaa sera na kutunga sheria itakayosimamia matumizi ya nishati mbadala ili kupunguza uharibifu wa mazingira.

(e) Kupunguza gharama ya vifaa vya nishati mbadala ili wananchi wanaojenga nyumba za kisasa vijijini watumie nishati hiyo badala ya kuni na mkaa wa miti.

(f) Kuhimiza na kuhamasisha ufugaji wa kisasa vijijini ili uwe kichocheo cha hifadhi ya mazingira.

(g) Serikali iimarishe usimamizi wa viwanda na biashara kutochafua mazingira.

(h) Kutekeleza mradi wa vijiji vya mfano vya hifadhi ya mazingira (eco village).

(i) Vipeperushi vyenye mafunzo rahisi ya hifadhi ya mazingira viandaliwe, vichapishwe kwa wingi na vitumike kwenye mafunzo ya Elimu Yenye Manufaa nchini kote.

(j) Kufanya tathmini ya athari za kimazingira katika miradi ya ujenzi.

**Kujenga Uwezo wa Kukabili Majanga**

194. Majanga ni matukio yenye uwezo mkubwa wa kuhatarisha maisha ya watu, mifugo, mazao, barabara, reli, madaraja na makazi ya watu mijini na vijijini. Majanga makubwa husababishwa na vimbunga, mafuriko, matetemeko ya ardhi, volkano, ukame, nzige, kwelea-kwelea, mioto mikubwa, kuvuja kwa mafuta mengi, kuzama kwa meli, kupasuka kwa tenki au bomba la gesi, n.k.

195. Kwa kuwa tunaishi katika kipindi ambacho janga lolote kati ya hayo linaweza kuikumba nchi yetu wakati wowote, Chama Cha Mapinduzi kupitia Ilani ya 2010-2015 kitaitaka Serikali ijizatiti katika kujenga uwezo mkubwa wa kukabiliana na majanga kwa kuchukua hatua zifuatazo:-

(a) Kuhakikisha kwamba wakati wote Taifa lina chakula cha kutosha kwenye hifadhi yake.

(b) Kuimarisha vikosi vya Zimamoto vyenye uwezo mkubwa wa wataalamu na zana za kisasa katika kukabiliana haraka na mioto mikubwa.

(c) Kuimarisha vikosi vya uokoaji majini vyenye zana bora za kazi na kuwapanga katika mikoa inayopakana na bahari na maziwa makuu tayari kwa kutoa huduma hiyo.

(d) Kuandaa vikosi vya wahandisi wa ujenzi jeshini na uraiani ambao watakuwa tayari wakati wa mafuriko kupambana ipasavyo na majanga mbalimbali.

(e) Kushirikiana na Halmashauri za Jiji, Manispaa, Miji na Wilaya kujenga uwezo wa vyombo vya dola katika kudhibiti na kukabiliana na majanga ya aina mbalimbali.

(f) Kuimarisha Idara ya Maafa iwe na uwezo mkubwa wa kushughulikia maafa nchini kwa kuiwezesha iwe Taasisi inayojitegemea na yenye ofisi za Kanda.

(g) Kuimarisha ushirikiano baina ya nchi yetu na nchi nyingine katika kupambana na maafa hususani katika nchi za Afrika Mashariki.

(h) Kuanzisha utaratibu wa kawaida wa kuuza nchini maboya madogo yanayovaliwa ili wavuvi na wananchi wanaosafiri kwa mitumbwi waweze kuyanunua kwa ajili ya usalama wa safari zote za majini.

**Vyombo vya Habari**

196. Vyombo vya Habari vina jukumu la kuhabarisha, kuburudisha na kuelimisha wananchi kuhusu kuhusu masuala muhimu kwa jamii. Chama Cha Mapinduzi katika kipindi cha Ilani hii ya 2010-2015 kitasimamia Serikali kulinda mafanikio yaliyopatikana na kuendeleza uhuru wa vyombo vya habari kwa kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kuhakikisha kwamba matangazo ya Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) yanasikika nchini kote.

(b) Kuandaa Sheria ya kusimamia Vyombo vya Habari ambayo pamoja na mambo mengine itaondoa mianya inayosababisha ukiukwaji wa maadili ya uandishi wa habari.

(c) Kutilia mkazo mafunzo kwa Maafisa wa Habari na Wasemaji wa Wizara na Taasisi nyingine za Serikali.

(d) Kuendelea kuimarisha uwezo wa Idara ya Habari (MAELEZO) kama Msemaji Mkuu wa Serikali.

(e) Kuendelea kuhamasisha Halmashauri kuanzisha Vituo vya Radio na Televisheni.

**Mambo ya Nje**

197. Mwelekeo wa sasa wa Sera ya CCM ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, unaendelea kuongozwa na **Sera ya Diplomasia ya Uchumi**. Hivyo ofisi zetu za Ubalozi zitaendelea kuimarishwa kwa ajili hiyo.

198. Katika kipindi cha miaka ya 2010 -2015, Chama kitaielekeza Serikali iendelee kuboresha utekelezaji wa Sera ya Diplomasia ya Uchumi kwa kuchukua hatua zifuatazo:-

(a) Kuendelea kuitangaza nchi yetu kama moja ya nchi duniani zenye mazingira muafaka kwa ajili ya uwekezaji kutokana na historia yake ya miaka mingi ya **amani, umoja, utulivu na mshikamano wa kitaifa.**

(b) Kuendelea kutangaza na kutetea utajiri mkubwa wa vivutio vya utalii tulivyonavyo na kuvutia watalii wengi kutoka mabara yote ya dunia waje kuviona.

(c) Kuendelea kuzitafutia masoko bidhaa zetu zenye ubora unaotakiwa katika nchi za nje kwa kushauriana na wazalishaji wa ndani wa bidhaa hizo.

(d) Kuendelea kuzielewa vema athari na fursa za utandawazi kwa nchi changa na kutoa ushauri kwa nchi yetu kwa kadri itakavyoonekana inafaa.

(e) Kuendelea kudai haki ya uwakilishi wa Afrika katika Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kwa kuzingatia hoja ya wingi wa agenda zinazojadiliwa na kuamuliwa na Baraza hilo bila ya uwakilishi wetu.

(f) Kuongeza uwakilishi wetu nje kwa kufungua Balozi mpya na kuongeza umiliki wa nyumba za makaazi na ofisi za Ubalozi katika Balozi zetu nje kwa kadri hali itakavyoruhusu.

(g) Kuendeleza Sera ya Ujirani Mwema na nchi jirani.

(h) Kujenga mahusiano ya kirafiki na ushirikiano wa kiuchumi na vyombo mbalimbali vya Kikanda na Kimataifa, unaozingatia maslahi makubwa ya Taifa letu.

(i) Kuendelea kuzishinikiza nchi tajiri kutekeleza ahadi yao ya kutenga asilimia 0.7 ya Pato la Taifa la nchi zao kwa ajili ya misaada kwa nchi maskini.

(j) Kuendeleza mchakato wa kuitambua Jumuiya ya Watanzania wanaoishi ughaibuni na kuweka utaratibu utakaowawezesha kuchangia maendeleo ya Taifa lao.

**Utamaduni na Maendeleo ya Michezo**

199. Chama Cha Mapinduzi kinaamini kwamba vijana wa Tanzania wana vipaji vya michezo mbalimbali kama walivyonavyo wenzao wa mataifa mengine duniani. Mafanikio yaliyopatikana katika fani ya michezo yameonyesha wazi kwamba mbele ya safari nchi yetu itachukua nafasi yake stahiki katika michezo ya aina mbalimbali.

200. Katika miaka mitano ijayo ya utekelezaji wa Ilani hii, Chama kitaitaka Serikali kuweka msukumo mkubwa katika maendeleo ya utamaduni na michezo kwa kuchukua hatua zifuatazo:-

**Utamaduni**

(a) Kuona kwamba maeneo yote muhimu ya kihistoria nchini (historical sites) yanaimarishwa na kutunzwa ili kukuza utalii na maendeleo ya vizazi vijavyo.

(b) Kuendeleza utekelezaji wa uamuzi wa kuanzisha Makao Makuu ya”**Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika”.**

(c) Kuhakikisha kwamba lugha ya Kiswahili ambayo ni kielelezo cha utaifa na utamaduni wetu, inaendelezwa nchini na kimataifa na kuona kwamba kinatumiwa kwa ufanisi.

(d) Kuendelea kufanya tafiti za amali za tamaduni na kusambaza matokeo.

(e) Kuanza mchakato wa kujenga Jumba la Utamaduni Kiromo (Bagamoyo).

(f) Kubaini wasanii mahiri na wenye vipaji na kuwaendeleza.

(g) Kufanya utafiti wa lugha za asili ili kuzihifadhi na kupata misamiati kwa kukuza Kiswahili pamoja na kusambaza istilahi za Kiswahili zinazokidhi mahitaji ya taaluma mbalimbali.

**Michezo**

(a) Kuonesha wazi kibajeti umuhimu wa michezo katika mipango yetu ya maendeleo ikizingatiwa kwamba zama hizi zimeufanya utamaduni na michezo kuwa sehemu ya Diplomasia ya Uchumi wa nchi inayohusika.

(b) Kuishirikisha kwa ukamilifu sekta binafsi katika kuendeleza fani mbalimbali za michezo.

(c) Kuweka mkakati endelevu wa kuinua na kuendeleza michezo ya riadha nchini.

(d) Kuandaa mkakati wa kuwatambua vijana wenye vipaji mbalimbali vya michezo na kuwaendeleza.

(e) Kuendelea kufundisha walimu wa michezo mbalimbali.

(f) Kuandaa mashindano ya michezo kwenye ngazi ya vijiji, kata, tarafa hadi Taifa.

(g) Kuendelea kutenga maeneo ya wazi kwa ajili ya michezo.

(h) Kuanza kutekeleza Awamu ya Pili ya Ujenzi wa Uwanja wa Taifa.

(i) Serikali kwa kushirikiana na Sekta binafsi kutoa utaalamu na mafunzo ya miundombinu na vifaa vya michezo kwa Halmashauri na wadau mbalimbali.

(j) Kuendelea kukiimarisha Chuo cha Michezo Malya pamoja na kuendeleza michezo katika Shule na Vyuo.

(k) Kuitumia michezo kama nyenzo ya kuwaunganisha vijana wenye vipaji mbalimbali katika kufanya mambo makubwa ya kitaifa.

(l) Kulinda na kudumisha sheria ya viwanja vyote vya michezo nchini na kudhibiti uvamizi.

**Kuyaendeleza Makundi Mbalimbali**

201. Makundi yatakayoendelezwa katika kipindi hiki ni ya watoto, wanawake, watu wenye ulemavu na wazee.

**Watoto**

202. Kila mtoto wa Tanzania ana haki ya kuishi, kukua na kulelewa vema ili Taifa lipate kijana mwadilifu na raia mwema.

203. Katika kipindi cha Ilani hii ya 2010-2015, Chama kitaielekeza Serikali kuendeleza malezi ya watoto kwa kuchukua hatua zifuatazo:-

(a) Kukamilisha Sera ya Malezi na Makuzi ya Mtoto.

(b) Kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Mtoto (2009) kwa ajili ya ustawi na maendeleo ya mtoto.

(c) Kuwahamasisha akina Mama wajawazito kujifungulia kwenye Vituo cha Afya ili kupunguza vifo vya akina mama na watoto.

(d) Kutilia mkazo matumizi ya vyandarua ili kuwalinda dhidi ya malaria na kupunguza vifo vya watoto.

(e) Kuimarisha huduma ya chanjo kwa watoto dhidi ya magonjwa. Vituo vya afya na zahanati viandaliwe kutoa huduma hiyo kwa watoto kwa kuzingatia umri unaokubalika kitaalamu.

(f) Kushirikisha sekta binafsi na mashirika ya hiari katika kuanzisha na kuendesha vituo vya kulelea watoto na shule za awali.

(g) Kuboresha viwanja vya kuchezea watoto katika ngazi za Mitaa, Vijiji na Vitongoji.

(h) Kupitisha Sera Jumuishi ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto ili watoto wote nchini waweze kunufaika kutokana na utekelezaji wake.

(i) Kuendeleza vita dhidi ya ajira ya watoto.

(j) Kutekeleza mikataba ya haki za mtoto iliyoridhiwa na Bunge.

(k) Kuwahamasisha watumishi wa Afya juu ya kuwaelimisha Wazazi madhara ya madawa ya kulevya dhidi ya watoto.

**Wanawake**

204. Chama Cha Mapinduzi kinatambua mchango wa wanawake katika ujenzi wa Taifa letu. Katika kipindi cha Ilani ya 2010-2015, Chama kitaendelea kuitaka Serikali iwahusishe wanawake katika siasa, uongozi na modenaizesheni ya uchumi wetu kwa kuchukua hatua zifuatazo:-

(a) Kuongeza nafasi na fursa katika kuwateua wanawake kushika nafasi mbalimbali za uongozi, utawala na menejimenti ndani ya Serikali na taasisi zake.

(b) Kuongeza nafasi za uwakilishi wa wanawake kwa lengo la kufikia asilimia 50.

(c) Kuimarisha mifuko mbalimbali ya uwezeshaji wa wanawake na kuhamasisha vyama vya kuweka na kukopa (SACCOS na VICOBA).

(d) Kuendelea kuwahamasisha wanawake kutumia fursa za kiutendaji na kisiasa ambazo zipo katika nyanja mbalimbali kitaifa, kikanda na kimataifa.

(e) Kuimarisha mifuko iliyopo ya mikopo ili wanawake wengi zaidi waweze kufaidika kutokana na mifuko hiyo.

(f) Kuimarisha Benki ya Wanawake Tanzania (TWB) kwa kuongeza mtaji ili iweze kutoa huduma zake katika maeneo mengi zaidi nchini.

(g) Kuendelea kupiga vita mila na desturi zinazowabagua wanawake na kutekeleza Mikataba ya Kimataifa inayohusu maendeleo ya wanawake.

(h) Kuendelea kuimarisha Vitengo vya Jinsia katika Wizara, Taasisi na Idara za Serikali.

**Watu Wenye Ulemavu**

205. Chama Cha Mapinduzi kinaamini kwamba watu wenye ulemavu wanastahili kupata haki zote za kiraia na kibinadamu chini ya Katiba na Sheria za Nchi.

206. Katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani hii ya 2010-2015, Chama kitaitaka Serikali kuendelea kuitafsiri imani hiyo kwa vitendo kwa kuchukua hatua zifuatazo:-

(a) Kuendelea kupanua na kuimarisha fursa za kisiasa, kiuchumi na ajira kwa watu wenye ulemavu.

(b) Kuimarisha na kuboresha mbinu za ulinzi wa watu wenye ulemavu wa ngozi.

(c) Kuhakikisha kwamba ujenzi wa majengo yanayotoa huduma kwa umma yanajengwa kwa kuzingatia mahitaji ya raia hao.

(d) Kuendelea kuboresha shule za watu wenye ulemavu kwa kuwapatia walimu wenye taaluma ya kuwafundisha na zana za kufundishia.

(e) Kubaini watu wenye ulemavu wanaoweza kufanya kazi za uzalishaji mali katika maeneo wanakoishi na kuwawezesha ili waweze kujiajiri.

**Wazee**

207. Tangu nyakati za kupigania uhuru wa nchi yetu, TANU na ASP vilitambua na kuenzi ipasavyo nafasi ya wazee katika harakati hizo. Hekima na busara zao pamoja na mshikamano wa dhati uliokuwepo baina yao na vijana waliokuwa msitari wa mbele katika kudai uhuru wetu, viliijengea nchi mazingira ya ushindi wa uhakika. Wazee waliounda Baraza la Mapinduzi la Zanzibar baada ya Mapinduzi ya Zanzibar, ni kielelezo hai cha umuhimu wa michango ya wazee katika maendeleo ya nchi yetu. CCM imerithi hazina ya uzoefu huo.

208. Katika miaka ya 2010-2015, Chama Cha Mapinduzi kitazitaka Serikali ziendelee kuimarisha na kuboresha mipango na taratibu za utoaji wa huduma kwa wazee kwa kufanya yafuatayo:-

(a) Kutunga sheria itakayotawala utoaji wa haki ya matibabu bure kwa wazee wasiojiweza katika vituo vya matibabu huko wanakoishi. Chini ya sheria hiyo kila mzee apatiwe kitambulisho kwa ajili hiyo ili wazee waweze kutibiwa kwa uhakika bila ya usumbufu wowote.

(b) Kuendelea kuboresha mafao ya wazee wanaostaafu ili yaendane na hali halisi ya gharama za maisha na matakwa ya soko ili maisha yao tulivu yachangie vema katika amani ya nchi kwa ujumla.

(c) Kuendelea kutumia uzoefu, hekima na busara zao kwa kadri inavyowezekana.

(d) Kuendelea kuwawezesha kiuchumi kwa kiwango fulani wazee ambao wataonekana kuwa bado wana nguvu za uzalishaji mali.

**Kuhamia Makao Makuu Dodoma**

209. Uamuzi wa kuhamishia Dodoma Makao Makuu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, uliotangazwa na **Baba wa Taifa Mwl. Julius Kambarage Nyerere** mwaka 1973, ulifanywa kwa kuzingatia sababu za kudumu.

210. Pamoja na kwamba hatua za kutekeleza uamuzi huo zimekumbana na matatizo mbalimbali, yapo mafanikio yaliyopatikana. Mafanikio hayo ni: Makao Makuu ya CCM, Ofisi za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wizara ya TAMISEMI tayari vimehamia Dodoma. Kujengwa kwa Chuo Kikuu cha Dodoma ni sehemu ya mafanikio ambayo yameongezea mazuri ya kuhamia Dodoma.

211. Katika kipindi cha miaka mitano ijayo (2010-2015) Chama Cha Mapinduzi kitaitaka Serikali kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kuandaa mpango thabiti wa kuhamia Dodoma hatua kwa hatua. Katika mpango huo, Mpango Mji wa Dodoma (Master Plan) utazamwe upya ili kuhakikisha kuwa majengo ya Serikali yanajengwa upya Chamwino kwa kuanzia na majengo ya ofisi na makazi ya Rais (Ikulu).

(b) Kuihamasisha Sekta binafsi kushiriki katika ujenzi wa hoteli za kisasa, viwanda, hospitali, n.k. katika maeneo ya Manispaa yaliyotengwa na yatakayoendelea kutengwa.

(c) Kutunga sheria ya kutambua mji wa Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi.

(d) Kuanzia sasa majengo mapya ya Wizara za Serikali yajengwe Dodoma badala ya Dar es Salaam.

## SURA YA TISA

## CHAMA CHA MAPINDUZI

212. Chama Cha Mapinduzi katika miaka mitano ijayo kinaelekeza nguvu kubwa katika kutimiza lengo la msingi la Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025 kwa kuendeleza jitihada za ujenzi wa uchumi wa kisasa na taifa linalojitegemea. Katika kuzingatia jukumu hilo Ilani hii ya CCM ya 2010 hadi 2015 inatangaza nia ya modenaizesheni ya uchumi. Modenaizesheni ya uchumi ndiyo njia ya uhakika itakayobadili na kuleta mapinduzi katika uchumi wa nchi, kujenga msingi wa uchumi wa kati unaoongozwa na viwanda, kuondoa umasikini wa wananchi wetu kwa kiwango kikubwa na hivyo kuwezesha nchi yetu kujitegemea. Ni ahadi ya CCM kuwa ikichaguliwa tena itaongoza Mapinduzi hayo ya Kiuchumi kwa kutumia Mkakati wa Kuwashirikisha Wananchi kupitia Sera ya Kuwawezesha Wananchi Kiuchumi na Usimamizi wa Dola wa Mipango ya Uchumi wa Nchi.

213. Utekelezaji wa majukumu ya Ilani hii ni changamoto ya kihistoria kwa kizazi cha sasa cha viongozi na wanachama wa Chama Cha Mapinduzi. Changamoto hii inahitaji viongozi na wanachama wanaoongozwa na nadharia ya mapambano, kutekelezwa kwa vitendo, kuhamasisha umma na kufanya tathmini ili kufikia malengo yaliyokusudiwa. Mtindo huu wa utekelezaji tunajifunza kutoka kwa viongozi walioongoza harakati za ukombozi wa TANU na Afro katika kuung’oa ukoloni Tanganyika na kuupindua utawala wa Sultani Zanzibar. Waliongoza kwa vitendo kwa kuhamasisha wananchi na kwa kupima matokeo yake.

214. Kizazi cha sasa cha viongozi wa Chama chetu lazima kibadilike kiutendaji, katika msimamo na mtazamo. Jukumu lililo mbele yetu ni hatua ya pili ya ukombozi wa nchi yetu na watu wake kiuchumi. Badala ya kulalamikia tu umasikini na utegemezi wetu, tuchukue hatua kivitendo, kimsimamo na kimtizamo. Jukumu la kujenga uchumi wa kisasa na taifa linalojitegemea linahitaji viongozi wa Chama kuongoza kivitendo katika uhamasishaji wananchi na usimamizi madhubuti wa Serikali katika utekelezaji wa Sera za Chama, Ilani na Mwelekeo.

215. Katika kuzingatia usimamizi kivitendo Ilani ya Chama ya mwaka 2010-2015 inaainisha majukumu ya kimethodolojia yafuatayo:-

(a) CCM lazima kiongoze kwa kuonyesha njia na kwamba hii ni changamoto ya kihistoria kwa kizazi cha sasa cha viongozi wa Chama chetu;

(b) Wajibu wa kimsimamo na mtazamo wa viongozi na wanachama wetu wenye dhamira ya kupambana na umasikini mpaka watakapoushinda; na

(c) Wajibu wa vitendo kwa viongozi na wanachama wetu kwa kuwa mfano wa kuigwa kwenye utendaji na utekelezaji wa majukumu mbalimbali k.m. Wakulima bora, Wafugaji bora, Wavuvi bora n.k.

216. Hivyo, ni muhimu kwa Chama kudumisha na kuimarisha utaratibu wa kusimamia, kufuatilia na kusukuma utekelezaji wa Ilani kwa viongozi na wanachama wake na kwa upande wa pili kwa Serikali zake mbili. Chama chetu hadi sasa bado kipo imara na hakitayumba na kimejipanga vizuri katika kusimamia utekelezaji wa Ilani.

217. Malengo makuu ya Ilani ya miaka 2000-2010 yanatuunganisha na majukumu ya Ilani ya CCM ya 2010 hadi 2015. Katika kipindi hiki, Chama kitaendelea kusimamia na kuchochea utekelezaji wa malengo ya miaka mitano iliyopita kwa kuzingatia uzoefu uliopatikana ili ifikapo mwaka 2015 Sera ya Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi iwe inashirikisha wananchi wengi zaidi katika ujenzi wa uchumi wa kisasa nchini.

(a) **Chama Cha Mapinduzi na Muungano**

218. Zimeanza kujitokeza dalili kwamba wanasiasa wanapandikiza mbegu za udini, ukabila na hisia nyingine zinazowatenganisha Watanzania. Lengo lao ni kupata madaraka ya kisiasa bila kujali madhara makubwa kwa Taifa yanayoambatana na sera hizo za kibaguzi. TANU na ASP na sasa CCM chini ya uongozi wa waasisi wake vimefanya jitihada kubwa kujenga umoja wa Taifa. Wanachama ndio wamekuwa kichocheo cha umoja, udugu na mshikamano wa Watanzania. Katika kipindi cha Ilani (2010-2015) Chama Cha Mapinduzi kitahakikisha viongozi wake wanakuwa mstari wa mbele katika kuongoza vita dhidi ya ubaguzi wa Watanzania kwa misingi ya dini, kabila, eneo, jinsia n.k. ili kuendeleza ujenzi wa misingi imara ya umoja, udugu na mshikamano wa kitaifa.

219. Muungano wa Tanganyika na Zanzibar sasa umefikisha umri wa miaka 46, tangu kuasisiwa kwake hapo tarehe 26, Aprili 1964. Katika kipindi hiki Muungano wetu umezidi kuimarika na kupiga hatua kubwa katika nyanja za kisiasa, kiuchumi na kijamii. Sambamba na mafanikio hayo, zipo changamoto nyingi ambazo bado

zinahitajika kufanyiwa kazi. Hii ni pamoja na kujenga mazingira endelevu na kuimarisha fursa za kiuchumi miongoni mwa wananchi wa kila upande, ili waone na kuamini kwamba, Muungano wa Tanganyika na Zanzibar sio tu ni ngao madhubuti ya Umoja, Amani na Mshikamano wao, bali pia ni daraja lisilotetereka la kuwafikisha katika azma yao ya kuondokana na umaskini na kuharakisha maendeleo yao na taifa kwa jumla. Hii ndio changamoto kubwa inayo ukabili Muungano wetu, ambayo Serikali zetu zinapaswa kuivalia njuga.

220. Katika kukabiliana na changamoto ya kuulinda, kuuenzi na kuendeleza Muungano wetu, sera za CCM katika miaka ya 2010-2015 zitaendelea kusisitiza na kusimamia utekelezaji wa yafuatayo:-

(a) Kuendeleza muundo wa Serikali mbili zilizopo sasa na kudumisha ushirikiano mwema kati ya Serikali hizi.

(b) Kuendeleza dhamira ya kweli ya kujenga utamaduni wa kukaa pamoja ili kujadili changamoto mbalimbali za Muungano, kwa lengo la kuzipatia ufumbuzi wa haraka kwa faida na maslahi ya pande zote mbili za Muungano.

(c) Kuendelea kujenga na kukuza msimamo na uelewa wa pamoja wa wananchi (Watanzania) juu ya masuala ya Muungano, hususan historia, misingi, utaifa na malengo yake ili kuwawezesha wananchi kufahamu umuhimu na uhalali wa Muungano wetu pamoja na kuimarisha umoja wa kitaifa na mshikamano miongoni mwa Watanzania.

(d) Kuimarisha Taasisi zilizowekwa kwa mujibu wa Katiba na Sheria, za kushughulikia masuala ya Muungano pamoja na kuimarisha mkondo wa mawasiliano na urejeshaji wa taarifa kwa wakati ili kasi ya kuimarisha Muungano isipungue.

## (b) Chama Cha Mapinduzi na Kutoa Uongozi kwa Taifa

221. Mwalimu J.K. Nyerere, Baba wa Taifa, aliwahi kusisitiza "Pasipokuwa na haki hapawezi kuwa na amani". Tanzania imefanikiwa kuwa nchi yenye amani na utulivu kutokana na sera zake zinazoweka mbele uhuru, haki, usawa na utu. Lazima CCM iendeleze sera hizi kwa nguvu zote. Katika kipindi hiki ambapo uchumi wa soko ndiyo unaotawala dunia na kufanya watu wachache kupata nafasi ya kujilimbikizia mali na kuwaacha watu wengi kwenye kingo za umaskini, Chama Cha Mapinduzi kimekuwa mstari wa mbele kuendelea kuibua sera ambazo zinalenga katika kuwawezesha watu wake kiuchumi na kupambana na umasikini kama inavyoainishwa katika Mwelekeo wa Sera za Chama chetu wa miaka 2010-2015. Chama Cha Mapinduzi kimekuwa wakati wote mstari wa

mbele katika kujali maslahi ya wanyonge ambao ndiyo wengi katika nchi hii kwa kuweka wakati wote sera zinazozingatia maslahi yao.

222. Kwa mantiki hii Chama Cha Mapinduzi bado ndiyo Chama kinachotegemewa na watu wengi kuendelea kutoa uongozi unaozingatia maslahi yao. Na maslahi ya watu wengi yakilindwa na kutekelezwa, nchi inadumu katika amani na utulivu. Ilani ya CCM katika miaka ya 2010-2015 inakusudia kuendeleza amani na utulivu huo.

(c) **Chama Cha Mapinduzi Kuongoza Ujenzi wa Uchumi wa Kisasa na Kuutokomeza Umaskini**

223 Chama Cha Mapinduzi kitaongoza ujenzi wa uchumi na kutokomeza umaskini kwa kuchukua hatua madhubuti zifuatazo:-

(a) Kuhakikisha kwamba, Chama na Serikali zina uelewa na msimamo wa pamoja kuhusu utekelezaji wa Ilani na Sera hizi.

(b) Mafunzo ya siasa, itikadi, maadili na malengo ya Ilani hii yataimarishwa katika ngazi zote za uongozi wa Chama.

(c) Ngazi zote za uongozi wa Chama kufanya kazi ya Chama ndani ya Chama na kazi ya Chama ndani ya Umma kwa kuzingatia Kanuni ya kukosoa, kujikosoa na kukosoana kama njia ya kujijenga na kujiimarisha wakati wote. Vikao vya Chama vitatekeleza kanuni hii.

(d) Chama kutekeleza kwa ukamilifu Ibara ya 18 ya Katiba ya CCM kuhusu "**Mwiko kwa Kiongozi**" ili kuhakikisha kwamba ndani ya Chama na ndani ya Dola madaraka ya kiongozi hayatumiwi kinyume cha lengo lililokusudiwa madaraka hayo.

(e) Kuweka msukumo mkubwa katika ujenzi wa Chuo cha Chama kitakachotoa mafunzo kwa viongozi, watendaji, makada, makamisaa wa Chama na wanachama kwa jumla kama hatua ya uhakika ya kujenga uongozi na utendaji wa pamoja ndani ya Chama na dola.

(f) Chama Cha Mapinduzi kitaendelea kuimarisha uhusiano na ushirikiano mwema baina yake na vyama vingine vya siasa duniani kwa kadri itakavyoonekana inafaa.

(g) Chama kuendelea kuimarisha usimamizi wa kazi na shughuli za Serikali kupitia Bunge, Baraza la Wawakilishi na Halmashauri zinazohusika.

(d) **Chama Kusimamia Utekelezaji wa Ilani**

224. Mara kwa mara Chama Cha Mapinduzi kimekuwa kinaelekeza vyema kazi ya Chama ya kuongoza na kusimamia kwa vitendo shughuli za Chama na Serikali. Pamoja na ukweli kwamba maelekezo yatolewayo ni mazuri, utekelezaji wake umekuwa ukilalamikiwa. Moja ya sababu ya mapungufu katika utekelezaji ni Chama kutotimiza jukumu lake la kuongoza kikamilifu kwa kuweka methodolojia sahihi za kufuatilia, kudhitibi na kufanya tathmini. Mwelekeo wa Sera za Chama Cha Mapinduzi katika Miaka 2010 hadi 2020 unaelekeza tuondokane na tatizo hili kwa kuweka utaratibu wa ufuatiliaji. Kwa hakika jukumu la Chama ni pamoja na kutoa lengo, lakini ili lengo hilo lifanikiwe Chama lazima kihakikishe uhamasishaji umma, usimamizi wa utekelezaji na kufanya tathmini.

225. Katika kutekeleza jukumu la kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa Ilani katika kipindi cha Ilani hii 2010 hadi 2015 Chama Cha Mapinduzi kitatumia utaratibu na methodolojia ifuatayo:-

(a) Viongozi wa Chama na Serikali watawezeshwa kupata uelewa wa pamoja wa Sera na dhana husika. Chama kitasimamia suala hili kwa kuendesha Mafunzo Elekezi na vikao kwa Watendaji Wakuu wa Serikali (Baraza la Mawaziri, Makatibu Wakuu wa Wizara, Wakuu wa Mikoa). Aidha, mara baada ya uchaguzi Ilani itajadiliwa kwa kina na Serikali itaandaa programu au ajenda ya utekelezaji wa Ilani.

(b) Aidha kwa upande wa Chama mjadala wa Utekelezaji wa Ilani utaendeshwa kupitia kikao cha Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC), Halmashauri za Mikoa (REC), na Wilaya (DEC). Chama kitajadili programu ya utekelezaji wa Ilani na kazi ya kufanya na uhamasishaji wananchi katika ngazi zote.

(c) Chama kitaweka utaratibu wa kufanya mapitio ya utekelezaji wa Ilani mara moja kila mwaka, kwa Halmashauri Kuu (NEC) kujadili na kufanya tathmini ya utekelezaji. Aidha Chama kitasimamia utekelezaji wa jukumu la kikatiba la Serikali kutoa taarifa kila mwaka.

226. Kimsingi utekelezaji wa Ilani hii utafanikiwa kama Chama kitatekeleza jukumu lake la kusimamia kwa kuhakikisha kuwa programu ya utekelezaji inaandaliwa na kusimamiwa ipasavyo. Inawezekana kujenga Maisha Bora kwa kila Mtanzania na Tanzania yenye Neema Tele kama Uongozi wa sasa wa Chama utabadilika kiutendaji, kimsimamo na kimtazamo.